**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 3 Julai, 2006**

*Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kuendelea na mtiririko wa Orodha ya Shughuli za leo, ninayo matangazo yanayohusu wageni. Kwanza katika Ukumbi wa *Public Gallery* upande wa kushoto ni Madiwani na Viongozi wa Wilaya ya Dodoma, wageni wa Waheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa John Malecela, Mheshimiwa Ezekiah Chibulunje na Mheshimiwa Mariam Mfaki. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani.

Pia wapo wageni wa kutoka Jimbo la Nachingwea, ambao ni Madiwani 24 wa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea wageni wa Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mbunge na Naibu Waziri, wale pale mkono wa kulia. Waheshimiwa Wabunge, wanaongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri Mama Joyce Mtauka, namtaja makusudi kwa sababu mama huyu hakupita kwa kubabaisha ni wale ambao ameshinda uchaguzi kwa kura nyingi kuwa Diwani. Pengine zuri zaidi amemshinda mwanaume. Hongera sana Mama Mtauka. (*Makofi/Kicheko*)

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa James Musalika, ambao ni walimu wa shule ya msingi na wapiga kura kutoka Jimbo la Nyang'wale wale pale. Karibuni sana. Tunaye pia mhubiri maarufu mwenye kituo cha *ATN* kule Dar es Salaam Mchungaji Fernandes, yule pale. Karibu sana Baba Mchungaji na ahsante kwa kazi yako njema ya kuongoza vijana katika njia iliyonyooka. *(Makofi)*

**HATI ZA ZILIZOWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Miundombinu kwa mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MHE. PAUL P. KIMITI – ((K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):**

Maoni ya Kamati ya Miundombinu, kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makaridio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2006/2007.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2006/2007.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 127

**Kufufua na Kujenga Barabara**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara itokayo Mkinga kupitia Dima, Kinyatu, Gombero hadi Mjesani ni miundombinu muhimu unaounganisha Makao Makuu ya Wilaya ya mpya ya Mkinga na sehemu kubwa sana za Wilaya hiyo na kwa kuwa ubovu wa barabara hiyo umekuwa kero muda mrefu.

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka kwa barabara hiyo kufufuliwa na kujengwa angalau kwa kiwango cha changarawe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara itokayo Mkinga kupitia Dima, Kinyatu, Gombero hadi Mjesani ina urefu wa km. 43.1. Barabara hii hupitia kwenye miinuko na sehemu kubwa ya maeneo haya ni pori.

Mheshimiwa Slpika, ili kufufua na kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe, ni lazima pia kujenga Madaraja ya Msimbazi, Mkaka, Kombe na Ndoyo.

Tathmini iliyofanywa inaonyesha kwamba barabara hii mpaka ijengwe, inahitaji kiasi cha 863,815,000/= pamoja na na ujenzi wa madaraja.

Hata hivyo kwa sasa Halmashauri haina fedha za kuyajenga madaraja hayo, Halmashauri kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara inaendelea kuzifanyia matengenezo barabara mbadala za Doda- Mazola, Stakishari – Mkinga na Mjesani – Mapatano ambazo hutumiwa na wananchi wa maeneo hayo kufikia Barabara Kuu ya Tanga – Horohoro na barabara ya Mkoa wa Tanga – Mabokweni – Mtoni Bombo ambazo huhudumiwa na Serikali Kuu.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na jibu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda ieleweke kwamba barabara hizi zilizozungumzwa na ni za mzunguko sana na hiyo ni barabara muhimu ambayo ni mojawapo natumaini Mheshimiwa Rais Mstaafu, alipozindua Wilaya hiyo aliagiza kwamba miundombinu itengenezwe kwa maana mapendekezo kama Serikali ichukue hatua hizo zinazostahili kujenga hiyo haraka iwezekanavyo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Hilo lilikuwa ni pendekezo tu siyo swali kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Damas Nakei, kwa swali la pii.

Na. 128

**Ubora wa Miundombinu ya Barabara**

**MHE. DAMAS P. NAKEI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kuondoa umaskini na hatimaye kuleta maendeleo vijijini, uwepo wa ubora wa miundombinu ya barabara ni kichocheo muhimu sana na kwa kuwa, barabara za Dareda - Bacho na ile ya Dareda kati – Dohom – Kiru Six kuelekea Magugu ni viungo muhimu katika usafiri na usafirishaji:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani kuhusu hizo barabara?

(b) Kama Serikali inatambua umuhimu wa barabara hiyo, ni lini kazi ya ukarabati itaanza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Barabara ya Dareda hadi Bacho ni barabara ya kijiji inayoanzia Dareda Kati hadi Kitongoji cha Bacho kwenye Kituo cha Maonyesho ya Kilimo na Mifugo. Barabara za Dareda – Bacho na Dareda na Dareda Kati – Dohom – Kiiru Six kuelekea Magugu kwa ujumla ina urefu wa kilometa 3 na ipo chini ya Vitongoji vya Belmi na Bacho. Barabara nyingine ni ile ya Dareda Kati – Dohom hadi Kiru Six na kuunganisha barabara ya Wilaya ya Babati – Kiru – Err hadi Mbulu na kisha kuunganisha na barabara nyingine ya Wilaya ya Kiongozi hadi Kiru Six inayounga na Barabara Kuu ya Arusha – Babati. Barabara ya Dareda – Bicho na Dareda Kati – Dohom – Kiru Six inamilikiwa na Vitongoji vya Belimi na Bacho na barabara ya Dareda – Kati – Dohom hadi Kiru Six inamilikiwa na Vitongoji cha Hyasm na Vijiji vya Kiru Six na Kiru – Err. Wananchi wanaoishi katika maeneo yanakopita barabara hii wanashauriwa kuzifanyia matengenezo barabara hizi mara kwa mara ili ziweze kupitika.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu na barabara hizi kutokana na uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na biashara kama vile mahindi, maharage, kawawa, vitunguu, mbaazi na alizeti.

Vile vile barabara hizi zinaunganisha wananchi katika maeneo ya huduma za afya katika Kituo cha Dareda na Magugu na pia ni njia mbadala kwa magari yatokayo Arusha kwenda Dareda bila kupitia Babati Mjini. Gharama ya kuzifanyia ukarabati barabara hizo ambazo ni shilingi milioni 780. Gharama hizi ni kubwa kwa Halmashauri, hivyo taratibu zinafanywa ili barabara hizi ziweze kuingizwa katika barabara zinazohudumiwa na wakala wa barabara (*TANROADS*).

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo kubwa ni kujenga barabara kwa changarawe:

(a) Je, Serikali inaweza kujenga barabara hiyo kwa hatua (*stage construction*) kwa ikaanza na ujenzi kwa kuiweka katika hali ya kuwa barabara udongo ikawa gharama nafuu kuliko kusubiri upatikanaji hizo shilingi milioni 700?

(b) Kwa kuwa barabara ya *Dohom Kiru Six* hadi Magugu kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, mwenyewe kwamba ni *by pass* nzuri, je Serikali inaweza ikakubaliana na mimi kwamba ingefaa kupandishwa hadhi na kuwa Barabara ya Mkoa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali ina mpango wa kuangalia barabara zote ambazo zinahudumiwa na Halmashauri katika nchi nzima, ili itambue hali halisi na kilomita ngapi ambazo zinahitajika kutengenezwa na Halmashauri katika Tanzania nzima. Zoezi hili likiisha tutaainisha barabara zile ambazo ni muhimu sana kwa kufuata kipaumbele. Nafikiri zoezi hili likiisha barabara zote za vijijini zitakuwa zinatengenezwa kufuatana na kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, natambua kabisa kwamba barabara ya Dohom hadi *Kiru Six* kuelekea Magugu ni muhimu sana kwa sababu ni Magugu ni kama

*Commercial Centre* kwa ajili ya vijiji hivyo. Kwa hiyo, nafikiri tutaliangalia suala ili kuona kwamba tutatekeleza kwa kiasi gani. *(Makofi)*

Na. 129

**Gesi Asilia**

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY** aliuliza:-

Kwa kuwa gesi asilia ni jambo la Muungano chini ya Ibara ya 4(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na kwa kuwa kuna gesi inayopatikana Tanzania na imeshaanza kutumika:-

(a) Je, ni asilimia ngapi ya mapato yanayopatikana hupewa Zanzibar?

(b) Je, gesi hii itasaidiaje kutatua shida ya upungufu mkubwa wa umeme huko Tanzania Zanzibar?

**SPIKA:** Kabla ya Mheshimiwa Naibu Waziri, hajajibu swali nimemuona Mheshimiwa Kabwe Zitto, amekaa Kiti cha Kiongozi wa Upinzani sijataarifiwa, inaelekea kwa mkao huo sasa yeye kwa asuhuhi hii yeye ndio Kiongozi wa Upinzani. Naomba tulitambue hilo na kumpongeza kwa nafasi hii. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Uzalishaji wa gesi asilia ya Songosongo ulianza mwezi Julai mwaka 2004. kama nilivyojibu katika swali Na. 741 lililoulizwa na Mheshimiwa Hasanain Gulamabbasi Dewiji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kwenye mkutano huu tarehe 21/6/2006. Mauzo ya gesi asilia katika kipindi cha miezi 23 iliyoishia mwezi Mei, 2006 yalikuwa Shilingi 29,969,713,199/=. *(Makofi)*

Kati ya maduhuli yaliyokusanywa, jumla ya shilingi 11,663,702,459.25 zililipwa kwa *Pan African Energy Tanzania Limited* kufidia gharama za uzalishaji gesi, uwekezaji katika miundombinu na gawio lao kwa mujibu wa mkataba uliopo. Salio la jumla ya shilingi 18,306,010,739.75 zililipwa kwa Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania (*TPDC*) kulipa medani ya muda mrefu, gharama za uendeshaji, mrabaha wa gawio lao kwa mujibu wa mkataba uliopo. Kati ya kiasi kilicholipwa *TPDC*, shilingi 4,047,955,634.00 ni mrabaha (*royalty*) ambazo ni sehemu ya maduhuli ya Serikali. Kiasi hiki kiliwasilishwa kwenye Hazina ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar hunufaika kutokana na mchango wa jumla wa *SMT* kwa Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

(b) Mheshimiwa Spika, mitambo yenye uwezo wa kuzalisha megawati za umeme 190 iliyoko Ubungo Dar es Salaam, imeunganishwa na Gridi ya Taifa. Mwaka 2005 *TANESCO* ilinunua umeme kiasi cha Kwh 1,149,374,098 kutoka Songas na kutegemea mahitaji ya Zanzibar, *TANESCO* iliuza jumla ya Kw 185,584 kwa *Zanzibar State Fuel Corporation (ZSFC*). Pamoja na upungufu wa umeme unaosababisha asilimia 50 ya mgao wa umeme Tanzania Bara, Zanzibar haiathiriki, kwani hupewa kiwango chote kinachohitajika kwa mujibu wa mkataba wa umeme kati ya *TANESCO* na *ZSFC*. Tatizo la upungufu wa umeme linapojitokeza, mara nyingi hutokana hitilafu za kiufundi katika gridi ya Taifa au hitilafu ndogo ndogo kwenye mfumo wa njia ya *ZSFC*.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Je, katika mchakato mzima huu wa gesi ambayo ni ya Muungano Zanzibar imeshirikishwa kiasi gani?

(b) Je, ikiwa Zanzibar imepata katika mgao huo huo ambao unatokana na kilichopelekwa benki. Je, ina katika miradi yote hii ya Muungano gawio litakuwa linafuata *formula* hiyo hiyoo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwenye Bodi ya *TPDC* kuna ujumbe kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ina maana kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inawakilishwa kikamilifu katika shughuli zote ambazo zinahusiana na gesi hapa nchini. Nilivyoeleza katika jibu langu la msingi suala la gawio kutokana na gesi fedha zinafikishwa hazina na mgao unatokana na ile *formula* ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inavyopata fedha kutoka Serikali ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa gesi hii inatoka Mikoa ya Kusini na kwa kuwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, gesi ya *Mnazi Bay* inapaswa kutatua tatizo la umeme Mtwara na Lindi. Je, kuna mpango wowote ambao Serikali inao kwa ajili ya kutatua tatizo la umeme Mtwara na Lindi kutokana na gesi hii? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, suala la gesi na uzalishaji wa umeme katika Mikoa ya Mtwara na Lindi, linakaribia kukamilika, *GNT* iko katika harakati za mwisho ku- *negotiate* mkataba na wazalishaji tungeomba mvute subira ili *GNT* iandae mkataba ambao unafaa na umeme uje uzalishwe kutokana na gesi ambayo itapatikana. (*Makofi*)

Na. 130

**Uzalishaji wa Umeme**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO (K.n.y. MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mbinga ni miongoni mwa Wilaya za zamani zenye juhudi za kuchangia pato la Taifa kwa kiwango kikubwa, ambapo hutumiwa na Serikali likiwemo Shirika la *TANESCO* na kwa kuwa, mipango madhubuti ya Serikali ya Umeme Vijijini inayoashiria kuwa umeme ni muundombinu muhimu katika kusukuma gurudumu la maendeleo:-

(a) Je, kwa nini *TANESCO* iliridhia kuwashauri wananchi wa Mbinga kuzalisha umeme na kuuza kwa bei ya juu (*at cost*) bila ya kuangalia uwiano wa maeneo mengine, hii haikuwa ni kukwepa jukumu lao la msingi?

(b) Je, mpaka sasa Serikali imetenga jumla ya shilingi ngapi ili kuwekeza mitambo na kuendesha shughuli za uzalishaji umeme Wilayani Mbinga, wakati umeme wa gridi ukiendelea na hatua zake za msingi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Engineer Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, *TANESCO* haikuridhia kuwashauri wananchi wa Mbinga kuzalisha na kuuza umeme kwa bei ya juu au (*at cost*) bila ya kuangalia uwiano wa maeneo mengine isipokuwa hiyo ilitokana na hali halisi ya kifedha na kiundeshaji kwa wakati huo. Utaratibu wa kuanzisha Ushirika wa Umeme ulikuwa umechukuliwa na kutekelezwa na wananchi wenyewe wa Mbinga. Tatizo lililojitokeza lilikuwa ni la kiuendeshaji ambapo miliki ya mali na mapato yatokanayo na mradi huo yalileta kutoelewana kati ya Halmashari ya Wilaya na Ushirika hivyo kukwamisha ufanisi na uendelezaji wa mradi.

*TANESCO* ilishiriki kwa gharama zake katika kujenga mtandao wa usambazaji umeme, kushauri na kutoa mafunzo kwa mafundi wa kusimamia uendeshaji wa mifumo hiyo ya kusambaza umeme pamoja na kujenga kituo cha kuzalisha umeme (*power house*)

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga shilingi 2.5 bilioni kwa ajili ya kuzalisha umeme kwa Mji wa Mbinga, katika Bajeti ya 2006/2007 na iwapo Bunge lako Tukufu likipitisha Bajeti, basi kazi itaanza na kukamilika mwaka huu.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, niipongeze Serikali kwa hatua za dharura ambazo inachukua ili kuhakikisha Mji wa

Mbinga unapata umeme. Lakini *TANESCO* ina mpango wa kuleta umeme wa gridi katika miaka ya hivi karibuni. Je, Serikali inaweza kukubali kwamba umeme huo wa gridi utahusisha pia sehemu zile ambazo kuna mijiji midogo kama vile Kigonsera, Mbatili, Luanda, Maguu pamoja na Kata zote za Jimbo la Mbinga Mashariki?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi ni kwamba iwapo Bunge lako Tukufu, litapitisha Bajeti yetu ya mwaka 2006/2007 Wizara yangu ina mpango wa kufikisha umeme wa gridi pale Wilayani Mbinga.

Ili kupata orodha ya vijiji ambavyo vinaizunguka Wilaya ya Mbinga ambavyo vitapata umeme chini ya mradi huu ningemwomba Mheshimiwa Mbunge, tukutane baada ya kikao hiki cha Bunge, ili nimpatie orodha kamili ya vijiji ambavyo vitafaidika na mpango huu. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imetajwa kwenye swali la msingi kwamba umeme ni silaha muhimu ya kusuma maendeleo ya nchi.

Je, Serikali iko tayari kuwakopesha wananchi katika mpango wa uwezeshaji kwa wale wananchi ambao watapenda kuunganishiwa umeme? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI YA MADINI:** Mheshimiwa Spika, mawazo ya Mheshimiwa Mbunge, tumeyasikia siamini kama yanaweza yakafanyiwa kazi kwa kipindi hiki lakini tutayaangalia ili kuangalia kama suala la kukopesha katika kuunganisha mitambo ya umeme itawezekana.

Lakini naomba Mheshimiwa Mbunge, aelewe kwamba suala la kukopesha itabidi tuangalie uwezo wa kifedha wa Serikali na jukumu kubwa tulilonalo katika kipindi hiki kufikisha umeme kwa wananchi katika sehemu zote za Tanzania. (*Makofi*)

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, kwa vile Serikali inajitahidi kusambaza nguvu za umeme katika sehemu ningi za nchi kama tulivyoona huko Mbinga.

Je, kuna mpango gani wa kufikisha umeme katika makampuni ya machimbo kama vile Pariki kule Mara ambayo inatumia fedha nyingi sana za kigeni za nchi hii kuagiza lita nyingi sana za mafuta kutoka nje wakati ambapo fedha hizi zingeweza kulipwa katika kampuni yetu ya *TANESCO* na pia wananchi wa maeneo wakapata huduma hiyo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI YA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inafanya majadiliano na makampuni ambayo yanachimba madini hapa nchini. Kati ya haya majadiliano tumewaomba makampuni hayo yawe yanatupatia ratiba yao ya kufungua migodi katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, hii ni ili pale ambapo Serikali inaweza kupeleka miundombinu kama umeme katika migodi hiyo katika muda muafaka, ili kuwanufaisha wanakijiji wa eneo hilo na wananchi kwa ujumla pamoja na migodi hiyo, kutokana na mapato makubwa ambayo tunaweza tukayapata kutokana na kuwauzia umeme tunapeleka. *So* inategemea tukipata taarifa mapema na nia yetu ni kuhakikisha kwamba tunawauzia umeme ili shirika letu la *TANESCO* linafaidika na mauzo hayo. (*Makofi*)

Na.131

**Ukarabati wa Majosho ya Mifugo**

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA (K.n.y. MHE. MWADINI ABBAS JECHA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika jitihada za Serikali za kukabiliana na maradhi ya mifugo nchini hasa yanayosababishwa na kupe, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, kupitia mpango wa *DADP's* imelenga kujenga na kukarababti majosho 150 kila mwaka kati ya majosho 2,050 yaliyoko nchini na kwa kuwa katika mpango huo Serikali Kuu, itachangia asilimia 50 ya gharama ya kila josho na asilimia iliyobaki zichangiwe na Halmashauri zenyewe pamoja na wananchi:-

Je, ili kuhakikisha ukarababti wa majosho hayo, Serikali imejiandae kuona kwamba michango inayotokana na Halmashauri pamoja na wananchi inapatikana kwa wakati ili kukamilisha malengo yaliyokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Wete, kama ifuatavyo:-

Udhibiti wa kupe kwa njia ya kuogesha mifugo kwenye majosho ndiyo njia kubwa ambayo inatumika hapa nchini kwa muda mrefu. Katika maeneo mengi uogeshaji wa mifugo umekwamishwa na upungufu na uchakavu wa majosho, uhaba na ughali wa madwa ya kuogesha na ukosefu wa maji. Ili kutatua matatizo haya Serikali tangu mwaka 2003/2004 imekuwa ikitenga fedha kama mchango wake kwa ajili ya kujenga na kukarabati majosho vijijini. Kwa mfano mwaka 2003/2004 Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kujenga shilingi milioni 975 ya kukarabati majosho 195 mwaka 2004/2005 shilingi milioni 641 zilitengwa na kukarabati majosho 141 na mwaka 2005/2006 shilingi milioni 341.8 zilitengwa kwa ajili ya kukarabati majosho 84.

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumiwa na Serikali katika kukarabati majosho ni tofauti na ule wa malambo ambapo Halamashauri huchangia asilimia 30 na wananchi kuchangia asilimia 20 ya gharama ya kujenga ama kukarabati lambo.

Hali ilivyo ni kuwa, ukarabati wa majosho unazingatia makisio halisi yaliyowasilishwa na Wilaya ili kupatiwa fedha kupitia mpango wa *DADP's.* Kwa hiyo, Halmashauri na wananchi hawachangii fedha zozote katika ujenzi au ukarabati wa majosho yaliyotengewa fedha na Serikali chini ya *DADP's* bali kwa kushiriki kwao tu.

Mheshimiwa Spika ili kuhakikisha kwamba ujenzi au ukarababti wa majosho hayo unafanyika kwa wakati uliopangwa, Serikali imekuwa ikishirikiana na Halmashauri na wananchi kufuatilia kwa karibu na kwa pamoja utekelezaji wa kazi husika.

Aidha, Serikali imekuwa ikiwahamasisha wadau mbalimbali kuchungia ufufuaji wa majosho mengi zaidi ya yale yanayogharamiwa na Serikali. Kwa kuitikia wito huu wafugaji wenyewe na mashirika binafsi walikarabati majosho 47 katika mwaka 2003/2004 na majosho 31 mwaka 2004/2005.

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa ruhusa hii ya kuuza swali moja la nyongeza zaidi. Kwa kuwa kuna majosho yanayozidi zaidi 2,000 katika nchi hii, na kwa vile Serikali hujitahidi na kutengeneza majosho 150 tu kila mwaka. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuandaa mikakati ya kuzidisha zaidi 150 kwa vile kama utachukua 150 itatuchukua miaka 12 kuweza kumaliza kutengeneza majesho hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Kwa sasa Tanzania ni majosho 2,141. Lakini ukizingatia kuwa josho moja linahitaji kuhudumia ng'ombe 5,000 na kwa kuwa tuna ng'ombe 18.5 milioni tunahitaji majosho 3,700. Kwa hiyo, upungufu uliopo sasa hivi wa majosho 1,559 katika mkakati wa Serikali kupitia Wizara yetu suala la majosho limezingatiwa sana ili kuhakikisha kuwa tatizo la magonjwa ya mifugo linadhibitiwa. Wiki ijayo Waziri wangu atawasilisha matumizi ya Bajeti ya Wizara yetu na mkakati huu utaelezwa vizuri zaidi.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika na mimi nataka niulize swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa Naibu Waziri alisema kwamba tatizo kubwa la majosho ni dawa ya kuogea kwamba ni ghali. Je, Serikali sasa haiwezi kutoa ruzuku kwa dawa ya kukogeshea mifugo ili tatizo hili la kupe liweze kuondolewa kabisa kama inavyotoa ruzuku kwa mbolea kwa wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, niliwahi kusema kwamba ilikuwa ni azma ya Serikali kuweka ruzuku kwenye madawa ya mifugo. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa katika bajeti ya mwaka huu ruzuku hiyo itatolewa, Mheshimiwa Waziri ataieleza kwa kiasi gani. *(Makofi)*

Na. 132

## Uvunaji wa Wanyamapori kwa Ajili ya Nyama

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania imejaaliwa kuwa na mbuga nyingi za wanyamapori na kwa kuwa baadhi ya maeneo hapa nchini yana uhaba wa upatikanaji wa nyama, mfano Mtwara, Lindi, Ruvuma, Visiwa vya Mafia na Zanzibar:-

Je, Serikali haioni kuwa wakati umefika sasa wa uvunaji wa nyama itokanayo na wanyamapori ili Watanzania wa maeneo yenye uhaba huo wafaidike na wanyamapori hao badala ya kutegemea nyama za wanyama wanaofugwa pekee?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haina mpango wa kuwinda na kuwapatia wanyamapori wananchi wanaoishi maeneo yenye uhaba wa nyama. Hata hivyo, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi wanayo nafasi ya kujipatia nyamapori kwa bei nafuu kwa kutumia taratibu mbalimbali kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori ya mwaka 1974 kama ifuatavyo:-

1. Kukata leseni ya kuwinda wanyamapori kulingana na taratibu za uwindaji wa wananchi na wageni hapa nchini. Ada za leseni na maelekezo mengine kwa ajili ya kupata wanyama kwa ajili ya nyama zinatolewa chini ya taratibu ambazo ziko kule Wilayani.

2. Kuanzisha Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori *yaani Wildlife Management Areas (WMAs)* kwenye ardhi za vijiji. Mpango huo, tayari unatekelezwa kwa majaribio katika sehemu mbalimbali nchini ikiwemo Wilaya ya Liwale katika Mkoa wa Lindi, Tunduru na Namtumbo katika Mkoa wa Ruvuma. Uanzishaji wa maeneo hayo, utawezesha wananchi kushiriki katika uhifadhi na kupanga matumizi endelevu ya uhifadhi wa wanyamapori.

3. Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ni ya ufugaji wanyama wadogo wadogo hususan kwa wananchi waishio vijijini na miji midogo kwa ajili ya kitoweo na hata kusafirisha nje ya nchi kama biashara.

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa upatikanaji wa nyamapori kwa taratibu nilizozieleza, hauwezi kutosheleza mahitaji ya nyama yaliyopo na kutokana na ukweli huo, bado kuna haja ya kuendelea kuwahamasisha wananchi hasa wanaoishi katika

maeneo yenye uhaba wa nyama kuimarisha zaidi shughuli za ufugaji wa mifugo ya kawaida.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Waziri nilitaka kuiuliza Serikali kwa nini wananchi wa Mara wamekoseshwa haki hiyo ya kuweza kuwinda katika mbuga ya Serengeti ambapo Serikali inaweza kupata mapato na wao wakaweza kupata kitoweo na sasa hivi hawaruhusiwi kuwinda kwa sababu ya mipango isiyoeleweka ya Halmashauri ya Serengeti. Je, ni lini Serikali itaruhusu na wao wapate hiyo haki kama wananchi wengine wa Tanzania? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, sehemu anayoieleza Mheshimiwa Mbunge ya Serengeti ni hifadhi ya wanyamapori kwa ajili ya uwindaji wa kitalii na wa nyara za Serikali. Kwa hiyo, sehemu ambazo zipo upande wa Wilaya au Jimbo lake ni sehemu ambazo ni *Reserve Land*s kwa ajili ya uwindaji wa wanyama wa kawaida lakini maeneo yale mengi sana kwa sababu ya uwindaji haramu na kutokufuata taratibu wanyama wale wameshamalizika.

Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Mbunge kwa kufuata taratibu hizo nilizozieleza wanaweza kuanzisha *Wildlife Management Area* kwenye maeneo hayo na baada ya muda wanyama wanaweza kurudi. Lakini inahitaji usimamizi wa karibu na wananchi wakishirikishwa pamoja.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kama lilivyo swali la msingi, Wilaya ya Mpanda inayo mapori mengi na takriban yote yametengwa kwa ajili ya uwindaji wa kitalii na kuwakosesha wananchi maeneo ya kuweza kuwindia na kuweza kujipatia kitoweo. Je, Serikali inaweza kutazama upya ili kutenga maeneo wananchi waweze kufaidika na rasilimali hii?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, sehemu anayoieleza ya Wilaya ya Mpanda tuna mbuga au tuna eneo moja tu ambalo liko chini ya Sheria ya Wanyamapori ambalo ni Hifadhi ya Katavi.

Lakini hata hivyo sehemu anayoieleza Mheshimiwa Mbunge kumekuwepo na uwindaji haramu sana hasa Kaskazini mwa Katavi kwenye mto licha ya kwamba ule mto unatumika sana kwa ajili ya wanyama kuleta maji ndani ya mbuga. Lakini Wakimbizi wameharibu sana maeneo anayoyaeleza Mheshimiwa Mbunge.

Ni vizuri sana Mheshimiwa Mbunge kushirikiana na Halmashauri yake waweze kuangalia uwezekano wa kulinda wanyamapori walioko kwenye *Game Reserve* ambayo

inaweza ikawasaidia baadaye katika kupata wanyama kwa matumizi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameeleza.

Na. 133

**Semina, Vyombo vya Uvuvi na Mikopo kwa Wavuvi**

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA** aliuliza:-

Kwa kuwa zaidi ya asilimia 90 ya wakazi wa Delta ya Mto Rufiji katika Kata za Salale, Maparoni, Mbuchi na Kiongoroni ni wavuvi na kwa kuwa wananchi hao hutumia mitumbwi isiyo na mashine na kwa kuwa, eneo hilo ndilo pekee katik am wambao wa Bahari ya Hindi kunakopatikana samaki aina ya kamba *(prawns)* kwa wingi na kwa kuwa katika Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 imeeleza kuwapatia utaalam, vifaa vya kisasa wavuvi wadogo wadogo ili waendelee kuongeza pato la Taifa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi wa maeneo hayo semina kuhusu uvuvi bora wa kisasa?

(b) Kwa kuwa mikopo hutolewa kwa vikundi mbalimbali, Je, Serikali itatoa mikopo hiyo kwa vikundi vya uvuvi vilivyopo katika maeneo hayo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabir Marondwa, Mbunge wa Kibiti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali chini ya mradi wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari na Pwani *(MACEMP)* itaendesha semina kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali ya uvuvi kwa Wilaya tatu za Rufiji, Mafia na Kilwa.

Chini ya mradi huo wa *MACEMP* ambao unalenga katika kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo kuboresha hali zao kiuchumi, wananchi watapatiwa mafunzo na zana za uvuvi kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge. Mradi huo ambao unahusisha pia kilimo cha mwani, ukaangaji wa samaki, fedha hizo zitatolewa pia kupitia *TASAF* chini ya mradi ambao tumekubaliana nao.

Namwomba Mheshimiwa Mbunge awasisitizie jamii ya mwambao katika jimbo lake ikiwemo jamii ya wavuvi kuhusu kutumia ruzuku watakayopatiwa kwa busara katika kutekeleza shughuli zilizolengwa. Aidha, matumizi ya busara ya ruzuku hiyo yatawawezesha jamii hiyo kuendesha miradi midogo midogo iliyolengwa kwa mafanikio na hivyo kufikia malengo ya mradi kwa manufaa yao na taifa kwa ujumla.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sehemu kubwa ya wavuvi hao ni wanawake, ambao wao uvuvi wao ni mdogo mdogo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweza kuinua wanawake hao waweze kuwa na uvuvi wa kuweza kujipatia kipato kikubwa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, chini ya mradi ambao unalenga kwenye maeneo niliyotaja ya Wilaya hizo tatu, wanawake wanahusishwa moja kwa moja kama nilivyoeleza kuna shughuli za kukaanga samaki na kadhalika vyote hivyo vinalenga kwa jinsia zote mbili, kwa hiyo wanawake wana fursa sawa na wanaume wana fursa sawa kwenye mradi huo.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, nataka nimwulize Waziri huu mpango wa RUMAKI Rufiji Mafia na Kilwa naona huu mpango mpaka sasa hivi unasua sua na huu mpango ulikuwa ni wa miaka mitatu na mpaka sasa hivi mwaka mmoja umekwisha. Je, mpango huu utakuwaje na mwaka umeshakwisha na bado imebaki miaka miwili. Tutaweza kumaliza kwa miaka hii miwili iliyobaki? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, RUMAKI maana yake ni Rufiji, Mafia na Kilwa na Wilaya hizi zote kama nilivyosema ni za mwanzo katika mpango mzima wa *MACEMP* utahusisha Wilaya nyingi zaidi za Pwani kuanzia Mtwara hadi Tanga na baadhi ya Wilaya za Zanzibar, Tanzania Visiwani. Huo mradi kwa Wilaya hizo tatu tunautoa kwa *WWF* ambao ndiyo wanau-*manage* na taarifa tulizonazo bado wako ndani ya muda ambao tumekubaliana nao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi mradi utaendeshwa na utaendelezwa kama kawaida.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ninalo swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sasa hivi Serikali yetu inahimiza kuweza kubadilisha mazao yetu yawe katika hali bora zaidi ya kusindika ili watu wapate manufaa zaidi. Je, huoni wakati umefika pia sambamba na kuwapa mikopo wavuvi ili wavue zaidi pia kuhimiza wawekezaji kuweka kiwanda kikubwa katika Kanda hii kwa ajili ya usindikaji samaki wadogo wadogo na wakubwa wa maji chumvi badala ya wale maji baridi peke yake?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: N**apenda nikubaliane naye kuwa ni vema tukatoka kwenye shughuli ndogo ndogo kama za kukaanga samaki na kadhalika kama nilivyoeleza ili twende kwenye shughuli kubwa zaidi. Lakini hilo linahitaji kwanza uzoefu linahitaji na mtaji. Na kwa kufanya hivyo kwa Wizara yangu ikishirikiana na sekta binafsi tutafanya hilo ambalo Mheshimiwa Mbunge analisemea. Mojawapo ni mradi wa ufufuaji wa kamba ambao sasa hivi ambao ni mkubwa katika eneo hili la Afrika Mashariki ambao unafanyika kule Kisiwa cha Mafia. Mradi huo utakuwa na manufaa mengi sana kwa wananchi pamoja na kuwafundisha pia ufugaji wa kamba kwenye mashamba ambayo wananchi wanaweza kuyamiliki. Kwa hiyo, ni mwanzo

nzuri na napenda nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwamba tuhimize wananchi tuanze lazima uanzie mahali kabla hujafika sehemu au kipeo cha juu zaidi. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 134

**Huduma kwa Watoto na akina Mama wajawazito**

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa huduma za watoto na akina mama wajawazito na wanaojifungua bure na kwa kuwa huduma hiyo imekuwa haitolewi kisahihi kama inavyokusudiwa:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba huduma za watoto na akina mama wajawazito na wanaojifungua hutolewa bure. Serikali inajitahidi kuboresha huduma hizi kwa kufanya yafuatayo:-

1. Kwanza kwa kuhakikisha viongozi wa hospitali, vituo vya afya na Zahanati za Serikali wana nakala ya mwongozo unaobainisha huduma ambazo hazitakiwi kuchangiwa gharama na wananchi, hii ni pamoja na vituo kuagizwa kubandika mwongozo huo hadharani katika maeneo ya kutolea huduma zote ambazo wananchi wanatakiwa kugharamia.

2. Pili, Serikali inaendelea kugharamia upatikanaji wa dawa zote, vifaa chanjo kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano na dawa za uzazi wa mpango. Pale ambapo Bodi za Huduma za Afya za Wilaya zimeanzishwa zinasimamia utekelezaji wa sera mbalimbali ikiwa ni pamoja na huduma hii kutolewa bila malipo kwa walengwa.

Mheheshimiwa Spika, tunaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane katika kuwaelimisha wananchi kuhusu utaratibu huu. Aidha pale itakapobainika kuwa huduma hii haipatikana, Wizara ingependa kupata taarifa mara moja, na vile vile kuziarifu mamlaka za ajira kuwachukulia hatua za kinidhamu wahusika bila kusubiri kikao hiki.

**SPIKA:** Kabla sijaruhusu maswali ya nyongeza, nimeletewa taarifa kwamba kuna Waheshimiwa Wabunge ambao wanavaa baraghashia na suti za Ulaya na Kaunda suti pia. Natafuta ushauri wa kisheria hivi sasa. Ikigundulika kuwa hiyo ni kinyume cha Kanuni nitawaondoa humu Bungeni.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri yenye matumaini lakini hata hivyo nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa huduma ya kujifungua ni huduma nyeti na inahitaji faragha sana na yenye usiri mkubwa. Na kwa kuwa akina mama wengi wamekuwa wakijifungulia

katika eneo yasilokuwa la faragha kwa mfano akina mama wengi wanajifungulia katika eneo moja.

Je, ni lini Wizara itabadilisha taratibu hizi za kujifungulia sehemu moja akina mama wote wakiwa wanatazamana?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa kwamba akina mama wanapojifungua wanatakiwa wajifungulie katika sehemu yenye faragha. Katika hospitali zetu katika majengo ambayo wanaenda kujifungulia kawaida huwa wanajifungulia katika *ward* ambazo zinaitwa *Martenity Ward* au *Labour Ward* wanakwenda katika yale majengo ni kwamba katika lile jengo kuna sehemu ambayo imetengwa ambayo inaitwa Kizimba ambapo kule kizimbani ndiyo huyo mama anapokuwa anafikia hatua ya kujifungua anahamishwa katika wodi ile ya akina mama ambao wana uchungu anapelekwa katika kile chumba maalum ambapo kule anapata usaidizi wa *Nurse* lakini ni kweli kwamba mama anajifungulia pale ambapo wenzake wanasubiria na yeye anajifungulia pale. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nasikitika lakini nabanwa na Kanuni, wale wote ambao wamevaa baraghashia na suti za Kaunda Mheshimiwa Arfi toka, Mheshimiwa hapo lazima utoke, Mheshimiwa pale lazima utoke. Nikisema utoke, Mheshimiwa simama na utoke. Na wengine wa aina hiyo ambao sijawaona waende watoke, ama wakavae.

Kinachoruhusiwa na baraghashia ni vazi rasmi la mwambao Kanuni inasema hivi vazi la kimwambao yaani kanzu koti na kofia. *(Makofi)*

Tunaendelea na *Order Paper* Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu maruzi ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini nilikuwa na swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa mara nyingi akina mama wajawazito wanapopatwa na uchungu wakifika hospitalini huwa wanarudishwa kwa kukosa vifaa vidogo kama pamba na wembe na wakati huo huo akina mama hao wanakuja na ujauzito mkali sana saa nyingine hawana hata uwezo wa kununua wembe. Na vitu hivi binafsi ni vidogo sana kiasi kwamba Serikali inaweza ikavitoa bure.

Je, Serikali inasemaje kama mama mjamzito anafika wodini pamba na wembe na ameshikwa na uchungu au kuna mpango gani wa kutoa hivi vifaa vinavyodaiwa hospitali na si lazima mama aende navyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimesema kwamba Serikali inagharamia vifaa vyote vinavyotakiwa kuhudumia akina mama na watoto wanapokwenda hospitalini. Sasa ni kweli panatokea tuhuma kwamba akina mama wakifika kule wanaombwa kununua *gloves*, nyembe, pamba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hili ni kosa. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba Serikali inawajibika na ndiyo tutaendelea kununua vifaa vyote. Kwa maana hiyo basi kuanzia sasa hivi napenda kuliarifu Bunge lako tukufu na wananchi wote wanaonisikiliza kwamba kila hospitali katika ngazi ya Taifa, katika ngazi ya mkoa na katika ngazi ya wilaya wanatakiwa wakina mama wanapokwenda kujifungua hawaruhusiwi wala hawapaswi kununua *gloves,* kununua nyembe, wala kununua pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iwapo hiyo itaendelea hatua kali zitachukuliwa za kinidhamu na ninasema kwamba kuanzia sasa hivi Waganga Wakuu wa Hospitali zote wahakikishe kwamba vifaa hivi vinapatikana katika wodi za wazazi na wale ambao watakiuka wachukuliwe hatua mara moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge baada ya bahari nzuri hizi kwa akina mama wanyonge mamilioni wa nchi yetu, sioni haja ya kuendeleza swali la nyongeza. Sasa swali linalofuata ni Wizara hiyo hiyo. *(Makofi)*

Na. 135

**Mkojo kama Dawa ya Kutibu Magonjwa**

**MHE. MWAKA ABRAHAMAN RAMADHANI** aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya watu huamini kuwa kunywa mkojo wao wa asubuhi hutibu magonjwa:-

(a) Je, kuna ukweli gani katika imani hiyo?

(b) Kama kuna ukweli wowote. Je, mkojo huo unatibu magonjwa gani?

(c) Je, kuna madhara yoyote yanayoweza kutokea kutokana na mkojo huo kwa mtumiaji?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwaka Abrahaman Ramadhan, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkojo ni uchafu unaozalishwa na usiotakiwa mwilini ambao una mchanganyiko wa vitu vingi ikiwa ni pamoja na *ammonia* na *formaldehyde* ambazo ni sumu mwilini. *(Makofi)*

Kutokana na mapokeo na ya imani ya tiba mbalimbali katika maeneo ya nchi za Kiasia kumekuwa na imani kuwa mkojo ni dawa ya maradhi mbalimbali.

Maelezo ya imani hizo unaweza kuyapata hata katika mtandano (*Internet*). Aidha, katika mapokeo yetu ya Kiafrika na Tanzania ikiwemo, hakuna imani ya tiba inayouelezea mkojo kama dawa ya kutibu magonjwa mbalimbali.

Baada ya kutoa maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwaka Abrahman Ramadhan, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehem (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hakuna utafiti wowote wa kisayansi unaothibitisha kuwa mkojo ni dawa ya kutibu magonjwa mbalimbali na hivyo hakuna ukweli wowote katika imani hiyo.

(b) Matumizi ya mkojo yanaweza kumletea mtumiaji madhara makubwa ya kujiambukiza magonjwa yaliyo katika njia ya mkojo na kuenea mwili mzima.

Kwa mfano mtu akiwa na ugonjwa wa kaswende au kisonono na akawa anakunywa mkojo wake wenye vijidudu vya magonjwa hayo anaweza kusababisha ugonjwa huo kuenea kwenye utumbo na baadaye mwili mzima.

(c) Aidha, napenda kuwatahadharisha wananchi kuwa siyo kila kitu kilichopo kwenye mtandao *(Internet)* ni lazima itumiwe kama taarifa ilivyo. Ni vizuri wananchi wakaomba ushauri kutoka kwa wataalamu wetu kuhusu jambo lolote linalohusu afya zao likiwemo kutumia mkojo kama tiba.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kuniruhusu kuuliza swali dogo la nyongeza, kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kwamba mkojo ni sumu, na wako wananchi wanatumia mkojo huo wa kunywa wa asubuhi.

Je, Wizara itatoa taaluma maalum ili kuwafunza wananchi hawa wasitumie mkojo huo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba mkojo ni simu, sasa kama kuna watu wanaendelea kunywa mkojo wa asubuhi au wamchana au wa jioni. Mkojo.......

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri hebu rudia Spika, hakusikia. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi nimesema mkojo ni sumu na unaweza kueneza magonjwa mtu atakapo kunywa. Sasa kama Mheshimiwa Mbunge anasema kuna watu wanakunywa mkojo uwe wa asubuhi, uwe wa mchana uwe wa jioni, napenda kusema kwamba mkojo sio tiba kwa ugonjwa wowote ule.

Naomba kupitia Bunge lako Tukufu kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wanaonisikiliza kuwa mkojo sio dawa, kwa maana hiyo wale wanaotumia mkojo wa asubuhi kama tiba waache mkojo sio dawa. Kwa maana hiyo, kama wana matatizo ya kiafya waende wakaone wataalam wa afya na watawaelewesha vizuri badala ya kutumia mkojo kwa imani potofu, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa nadhani kwanza muda wa maswali umefika, lakini itabidi tulimalize swali linalofuata kwa sababu kipindi cha maswali kiliingiliwa na matangazo mengi sana. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Anna Lupembe, ili aulize swali la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. *(Makofi)*

Na.136

**Kusitishwa Mashindano Mashuleni**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa muda mrefu sasa Serikali imesitisha michezo na mashindano ya Shule za Msingi na Sekondari ambayo hapo zamani yalikuwa yakitoa wachezaji chipukizi na wazuri:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kurudisha mashindano hayo hasa katika awamu hii ya nne inayolenga kufufua na kuiboresha michezo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kufuta michezo hiyo imepoteza vipaji vingi na Taifa kukosa wachezaji wazuri?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe , Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa michezo na mashindano ya michezo katika Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu na Ufundi. Michezo shuleni haikusitishwa, kilichositishwa ni mashindano yaliyohusisha wanafunzi na walimu kwenda mbali kupiga kambi kwa muda mrefu na kwa gharama zilizohusisha wazazi. Hata hivyo Wizara yangu kwa sasa inaandaa mikakati itakayowezesha kurudisha mashindano hayo kwa utaratibu mzuri zaidi. Wakati mikakati hiyo ikifanyiwa kazi, Wizara yangu inahimiza mashindano kati ya darasa na darasa, Bweni na Bweni na shule zilizo jirani. Aidha, Wizara yangu inasisitiza shule zizingatie vipindi vya michezo katika ratiba za masomo.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) ya jibu langu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inaandaa mikakati ya kuboresha michezo shuleni ili kubaini na kuibua vipaji vya michezo kuanzia Shule za Awali. *(Makofi)*

**MHE. ANA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize. Je, lini sasa mashindano hayo yataanza rasmi ili na sisi tuweze kuwasaidia walimu katika maandalizi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majikbu yangu ya msingi kwamba tumeshaanza mikakati naomba niriharifu Bunge lako Tukufu kwamba, ili mashindano hayo yaanze kuna mambo kadhaa ya kuzingatia, na ni pamoja na kuhakikisha kwamba vifaa viko, walimu wa kufundisha michezo, fedha za kugharamia ili wazazi wasihusishwe tane na pia kuhakikisha kwamba chakula, maradhi, na usafiri wa wanafunzi hao unakuwa mzuri. Kwa maana hiyo basi naomba sasa hivi Waheshimiwa Wabunge tushirikiane katika kuhakikisha mashindano ya shule kwa shule zilizo jirani ndani ya shule zenyewe kwenye mabweni kama ni za shule za bweni, na madarasa kwa madarasa ili kuweza kuibua vipaji hivi. Hata hivyo tutaweka kipau mbele zaidi katika bajeti yetu ya mwaka 2007/2008, kwa sababu tunakwenda kwa vipaumbele.

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Spika, licha ya majibu yasiyoridhisha ya Mheshimiwa Waziri, Taifa linafahamu kabisa kwamba UMISHUTA na UMITASHUTA ilifutwa na Serikali iliyopita, kwa sababu sasa ni miaka mitatu hakuna UMISHUTA, hakuna UMITASHUTA, naomba Serikali isikanganye maneno, ni lini UMISHUTA na UMITASHUTA zitarudi ili kukuza vipaji vya watoto wetu?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niongezee kwa yale ambayo Naibu Waziri ameshaongea vizuri. Kwa kweli hata kwenye majibu nakazia yale yale ambayo amezungumzia Naibu Waziri kwamba, Serikali haikusitisha swali la msingi alilouliza Mheshimiwa Mbunge Anna Lupembe, ni kwamba kurudishwa lini mashindano ya michezo yatarudishwa.

Kwa kifupi michezo shuleni inaendelea kama kawaida na iko ndani ya ratiba, shule zote za msingi na sekondari, vyuo vyote vya ufundi na vya ualimu, kilichositishwa ilikuwa mashindano ya UMITASHUMTA, UMISETA yale yote ambayo yalikuwa yanahusisha vijana.

Kama alivyoeleza Naibu Waziri yalikuwa yanahusisha vijana na walimu kufunga safari kwenda kuweka kambi mbali, jambo ambalo lilikuwa linahitaji gharama kubwa na shule nyingi zilikuwa zinahusisha wazazi kuchangia ndicho kilichositishwa, na akajibu katika jibu la msingi kwamba Serikali inaanda mikakati ili sasa mashindano hayo hayo yatakaporudishwa yasiwe katika aina ile ile iliyokuwa ikifanyika kwa gharama. Ningependa kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge baada ya swali la nyongeza kwamba kwa hali ilivyokuwa ikiendeshwa michezo ile huwezi kuirudisha kwa aina ile ile hasa ukizingatia pia tusisahau kuna janga la UKIMWI hapa. Kwa hiyo, inataka tuwe makini sana katika kuandaa mashindano ya aina kwa wakati huu, na hasa pia kama ulivyosema gharama, lazima tuone fedha zitatoka wapi. Kama unakumbuka hapo mwanzoni ilishakataliwa kabisa michango mingi inakatisha tamaa wazazi. Kwa hiyo, mashindano tutakayoleta sasa, kwa vyovyote vile havitahusisha wazazi tena kuchangia.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha, na pia saa ya maswali imekwisha. Matangazo, kwanza Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Gideon Cheyo, anaomba wajumbe wake wote wa Kamati ya Kilimo na Ardhi wakutane leo saa saba mchana katika ukumbi namba 219 jengo la utawala, anaomba wote muwepo. Kamati ya Kilimo na Ardhi, saa saba chumba Na. 219.

Mheshimiwa Job Ndugai anaomba wajumbe wa Kamati yake ya Maliasili na Mazingira, wakutane leo tarehe 3 Julai, 2006 saa tano asubuhi, kikao katika ukumbi Na. 133 gorofa ya kwanza. Kwa hiyo, Kamati ya Maliasili na Mazingira, saa tano asubuhi chumba Na. 133.

Nawaharifu kwamba Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir amelazwa jana usiku wa manane *Dodoma Regional Hospital*, akisumbuliwa na maradhi ya tumbo, ni vizuri kama tunapopata nafasi, tuweze kwenda kumwona na kumsaidia. Afisa wa Bunge yuko pale wakati wote tangu jana saa nane akiwa ni kiungo kati ya hosipitali na sisi ili kujua maendeleo yake. Nasikitika vile vile kukuwaarifu kwamba Mheshimiwa Naibu Spika, amefiwa na mdogo wake na amekwenda Njombe kwa ajili ya mazishi. Naye tumtakie safari njema na yote yaweze kukamilika ili kuweza kumhifadhi huyo mdogo wake. Nimearifiwa kwamba hizi saa zinakanganya kwa mfano ile inaonekana kama imesimama kwa sababu haifuati muda ambao ni wa kawaida.

Sasa Waheshimiwa Wabunge napenda kusema tu tuvumiliane, jengo hili halijakamilika kwa asilimia 100 tutakuwa na saa mbili nzuri za *digital* za rangi nyekundu, ambazo zitakuwa zinaonekana mahali popote na herufi kubwa kabisa. Kwa sasa tumechukua tu kama ufumbuzi wa muda ambao tunaona nao unaleta matatizo. Lakini naomba tuwaharakishe kwa tangazo hili wenzetu wajezi waharakishe vitu mbalimbali ambavyo vinahitajika ili ukumbi wetu ukamilike asilimia 100. Naona huu ndio mwisho wa matangazo. Waheshimiwa Wabunge hadi sasa kwa Hotuba ya

Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu nimepata hapa wachangiaji 22 leo asubuhi. Hotuba hii itajadiliwa kwa siku mbili. Kwa hiyo, bado kuna uwezekano wa kupokea maombi mengine ya kuchangia katika hoja hii. Lakini ninao sasa 22. Kwa hiyo, tuna kazi ya kutosha kwa siku ya leo.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2006/2007
### Wizara ya Miundombinu

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Miundombinu kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Jakaya M. Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana na wananchi wa Tanzania kuwa Rais wetu wa Awamu ya Nne katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika nchini kote mwezi Desemba mwaka 2005. Aidha napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ushindi huu kwa Chama cha Mapinduzi unadhihirisha jinsi Chama hicho pamoja na sera zake nzuri zinavyokubalika kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kukipongeza Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kufanikisha uchaguzi wake mkuu ambao umefanyika hapa Dodoma hivi karibuni. Aidha, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais Jakaya M. Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuwa Mwenyekiti wa CCM. Kuchaguliwa kwake kunadhihirisha imani kubwa waliyonayo wanachama juu yake. Pia, napenda kumpongeza Mheshimiwa John S. Malecela (Mb), Makamu Mwenyekiti wa CCM (Bara), Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Makamu Mwenyekiti wa CCM (Zanzibar), Mheshimiwa Luteni Mstaafu Yusuf R. Makamba (Mb) kwanza kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na pili kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu mpya wa CCM. Viongozi wengine wa CCM ambao napenda kuwapongeza kwa kuchaguliwa kwao ni Kapteni Mstaafu Jaka Mwambi, Naibu Katibu Mkuu wa CCM (Bara), Mheshimiwa Salehe Ferouz, Naibu Katibu Mkuu (Zanzibar), Mheshimiwa Agrey Mwanri (Mb), Katibu wa Itikadi ya Uenezi ya CCM, pamoja na viongozi wote wa Sekretarieti Mpya ya CCM.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuchukua fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nina hakika kuwa uzoefu wake katika uongozi ni rasilimali na nyenzo muhimu kwa Taifa letu. Mimi binafsi na Wizara tuna matumaini makubwa kwake na tunaahidi kumpa ushirikiano wa dhati katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais na Mwenyekiti Mstaafu wa CCM, kwa kuiongoza nchi kwa umahiri na mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Kwa hakika uongozi wake umeweka msingi mzuri wa uchumi na uongozi ambao unaipa Serikali ya Awamu ya Nne mazingira mazuri ya kuanzia katika kuendelea kukuza uchumi na kuondoa umaskini nchini. Nachukua nafasi hii kumtakia Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu na familia yake maisha mema na marefu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua pia nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Spika katika awamu hii ya nne ambapo umeahidi kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa kutumia falsafa ya *standards and speed*. Bila shaka waheshimiwa Wabunge wenzangu watakubaliana nami kuwa kuchaguliwa kwako kunatokana na uzoefu wako mkubwa Bungeni na uwezo mkubwa katika kuendesha shughuli za kisiasa na kitaalamu ukitumia busara ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, binafsi sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwanza kwa wapiga kura wa jimbo la uchaguzi la Rombo kwa kuniamini na kunichagua kwa mara ya nne kuwa Mbunge wao.

Aidha, napenda kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuiongoza Wizara hii mpya na nyeti. Ninaahidi kuwa nitajitahidi kutekeleza majukumu niliyopewa ili kusukuma maendeleo ya kiuchumi na kijamii hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushindi walioupata katika majimbo yao, uwakilishi wao na kwa kuteuliwa kwao. Aidha, napenda kuwapongeza waheshimiwa Wabunge walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara mbalimbali na Mikoa kadhaa katika Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kutoa hoja za Wizara zao hapa Bungeni. Mawaziri hao ni Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa (Mb) na Waziri wa Fedha Mheshimiwa Zakia Meghji (Mb). Kwa ujumla hotuba zao zimefafanua utekelezaji wa sera na malengo ya uchumi na fedha, uimarishaji wa huduma za kijamii na kutaja malengo ya Bajeti kwa kipindi cha mwaka 2006/2007. Aidha, napenda kumpongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward N. Lowassa (Mb) kwa hotuba yake ambayo imefafanua kwa kina utekelezaji wa mipango na mikakati ya Serikali yenye lengo la kuimarisha na kuboresha huduma za jamii na utawala na hivyo kupunguza kero za wananchi zinazosababishwa na umaskini, ujinga, maradhi na utawala dhaifu.

Mheshimiwa Spika, Mwisho napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Bunge ya Miundombinu, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, kwa ushauri, maoni na maelekezo ambayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa katika maandalizi ya hotuba hii na mazingatio ya kiutendaji kwa kipindi cha Bajeti hii.

Katika kipindi hiki, Kamati ilitembelea miradi na kukutana na viongozi wa maeneo muhimu ili kutambua maendeleo na matatizo yaliyopo katika sekta ya Miundombinu. Kamati pia ilipata fursa ya kupitia taarifa za utekelezaji na mahesabu yaliyokaguliwa ya mwaka 2004 ya Bodi, Makampuni na Wakala mbali mbali za Serikali. Kamati ilishauri na kutoa maelekezo ambayo kwa kiasi kikubwa yatasaidia kuboresha na kuimarisha huduma zitolewazo na sekta za Ujenzi, Mawasiliano, Uchukuzi na Hali ya Hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Utendaji wa Jumla Katika Kipindi cha Mwaka 2005/2006 na Malengo ya Kisera, Wizara ya Miundombinu ni kati ya Wizara mpya zilizoundwa na Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuunganisha zilizokuwa Wizara ya Ujenzi na ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Wizara imepewa majukumu yafuatayo:-

Sera ya Ujenzi na usimamizi wake: Shughuli za ufundi na umeme; bohari kuu; majengo ya serikali; barabara, madaraja na vivuko; shughuli za usanifu na ujenzi na maabara ya vifaa vya ujenzi.

Sera za Mawasiliano na Uchukuzi na utekelezaji wake: Leseni za uchukuzi; viwanja vya ndege; usalama wa anga; hali ya hewa; posta na simu; reli; ndege za serikali; usafiri wa anga; bandari na huduma za zima moto katika viwanja vya ndege.

Maendeleo ya watumishi katika Wizara.
Idara zinazojitegemea katika Wizara.
Wakala za Serikali zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Ubunifu wa Sera, Wizara imekuwa ikitekeleza majukumu iliyorithi kutoka zilizokuwa Wizara ya Ujenzi na ya Mawasiliano na Uchukuzi pindi ikijipanga upya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005. Aidha, Wizara imekuwa ikibuni au kukamilisha Sera na kutoa miongozo ya utekelezaji. Sera hizo ni pamoja na Sera ya Ujenzi, Sera ya Uchukuzi, Sera ya Mawasiliano ya Simu, Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*ICT*) na Sera ya Taifa ya Posta. *(Makofi)*

Aidha, Wizara iko kwenye maandalizi ya Sera ya Taifa ya Huduma za Hali ya Hewa, Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani, Sera ya Majengo ya Serikali na nyumba za watumishi wa umma, Sera ya uwezeshaji wa makandarasi wadogo kila mkoa, Sera ya ajira na uwezeshaji wananchi kwa njia ya miundombinu na Sera ya ajira kwa wahandisi chipukizi na mafundi wa vijijini. Kwa mfano, katika Sekta ya Mawasiliano mkakati ulioainishwa ni ule wa kuhakikisha kwamba huduma za mawasiliano zinafika vijijini ambapo Wizara inaendelea na mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Mawasiliano (*Universal Communication Access Fund)* ili kufanikisha lengo hilo kwenye maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara. *(Makofi)*

Mkakati mwingine unaopewa kipaumbele ni pamoja na ule wa ujenzi wa Mkongo wa Kitaifa wa Mawasiliano ya Simu (*National Communications Infrastructure*

*Backbone*) wenye urefu wa km 6,000 utakaoweza kuunganisha Wilaya zote nchini na ambao unakadiriwa kugharimu dola za Kimarekani milioni 200.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine iliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na ile ya kuendeleza huduma ya mawasiliano ya simu yenye lengo la kuwa na simu 6 kwa watu 100 na pia kuwezesha angalau watu 2000 vijijini kote kufikiwa na simu moja ifikapo mwaka 2018, kuweka lami kwenye barabara zote kuu nchini, ifikapo mwaka 2018, kuhakikisha kuwa makao makuu ya Mikoa yote yanaunganishwa kwa barabara za lami, na Makao makuu ya Wilaya zote yanaunganishwa kwa barabara za changarawe au lami nyepesi zinazopitika wakati wote ifikapo mwaka 2015. Kuhusu huduma za Posta mkakati unaotekelezwa ni ule wa kuwa na huduma bora za posta hadi ngazi ya vijijini ifikapo mwaka 2015.

Kuhusu bandari zetu kuu, mkakati uliopo ni kuhudumia mizigo tani 9,777,141 ifikapo mwaka 2015 ikilinganishwa na tani 6,856,101 za hivi sasa. Kwa upande wa sekta ya anga mkakati unaotekelezwa ni ule wa kuishirikisha sekta binafsi ili iweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi ikiwa ni pamoja na kukifanya kiwanja cha ndege cha Mwalimu J.K. Nyerere kuwa kiungo (*hub*). Kwa upande wa sekta ya reli mkakati unaotekelezwa ni kuongeza uwezo wa reli kwa kuondoa mataruma yenye uwezo mdogo (ratili 50 kwa yadi) na kuweka yenye uwezo mkubwa (ratili 80 kwa yadi au zaidi). Kuhusu utoaji wa ajira, sekta ina mkakati wa kubuni nafasi mpya za ajira zaidi ya laki mbili na nusu ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Uendelezaji wa Miundombinu ya Uchukuzi (*TSIP*), Wizara ya Miundombinu ina lengo la kuwa na huduma za sekta ya uchukuzi ambazo ni endelevu, zenye ufanisi wa hali ya juu na zenye gharama nafuu ifikapo mwaka 2016. Ili kufikia malengo haya, Wizara imeandaa Programu ya Uendelezaji wa Miundombinu ya Uchukuzi *Transport Sector Investment Programme* (*TSIP*).

Programu hii imezingatia umuhimu wa kuendeleza yale yaliyokuwemo kwenye mpango wa miaka kumi wa sekta ya barabara yaani *Ten Year Road Sector Development Program* na kutoa kipaumbele katika uendelezaji wa miundombinu na huduma za uchukuzi na mawasiliano kwa lengo la kuibua uchumi na kuondoa umaskini. Kuna haja ya kuwa na miundombinu bora inayotosheleza maendeleo ya uchukuzi na mawasiliano na inayokidhi matakwa ya ushirikiano wa kibiashara katika jumuia za Afrika ya Mashariki na *SADC* kwa ujumla.

Tanzania ni nchi yenye rasilimali nyingi sana lakini bado hazijatumika kwa kiwango kinachostahili kwa kukosekana mtandao mzuri wa miundombinu. Kwa hiyo *TSIP* ina lengo la kuhakikisha kuwa hadi kufikia mwaka 2018 barabara kuu zote ziwe zimewekwa lami na barabara za mikoa ziwe zinapitika mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, *TSIP* ina lengo pia la kuhamasisha biashara ya nje. Hivi sasa bandari ya Dar es Salaam ni lango kuu kwa biashara ya nje kwa nchi za Zambia, *DRC*, Burundi, Rwanda, Malawi na kwa kiasi Uganda. Bandari nyingine ni Mtwara ambayo inaweza kuwa lango kuu kwa bidhaa zinazotoka au kwenda Malawi na Zambia; bandari

ya Tanga kwa bidhaa zinazotoka au kwenda nchi za Uganda, Rwanda, Burundi kupitia Arusha na Musoma. Kwa mantiki hiyo hiyo na ili kufanikisha azma hiyo, programu ya *TSIP* inalenga kuboresha reli ya kati, kwanza kwa kuiimarisha ili imudu uzito mkubwa zaidi; kuongeza mizigo itakayobebwa na reli ya kati kutoka kiwango cha sasa cha tani 1,129,000 kwa mwaka hadi tani 2,000,000 kwa mwaka ifikapo mwaka 2015. Hatua nyingine ni pamoja na kufanya upembuzi yakinifu wa reli ya Tanga-Arusha-Musoma na hatimaye kuijenga; kufanya uchunguzi na hatimaye kupanua geji ya reli ya kati kufikia kiwango cha mita 1.4; kuimarisha reli ya *TAZARA* ikiwa ni pamoja na kushirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wake; kuendeleza na kukamilisha mitandao ya barabara hasa zile zinazounganisha bandari na nchi jirani, kuimarisha viwanja vya ndege hasa vile vinavyowezesha kuendeleza biashara ya nje mfano, viwanja vya ndege vya Mwalimu J.K. Nyerere, Kilimanjaro, Mwanza, Kigoma, Songwe na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo litapewa mkazo ni lile linalosaidia katika kuendeleza sekta ya uzalishaji; mfano usafirishaji wa pembejeo za kilimo, usafirishaji wa mazao kwenda kwenye masoko ya ndani na nje, kufika kwenye maeneo ya utalii na uzalishaji vijijini hasa kwa lengo la kujitosheleza kwa chakula na kuondoa adha za uchukuzi kwenye miji mikubwa. Malengo mengine ya programu hii ni kuwa na miundombinu endelevu, salama, yenye gharama nafuu, ya kuaminika na inayozingatia uhifadhi wa mazingira, kuhamasisha na kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi katika uendelezaji wa miundombinu na kuhakikisha kuwa maendeleo ya sekta ya uchukuzi yanazingatia makundi maalum ya jamii kama vile wanawake. Utekelezaji wa *TSIP* unatarajiwa kufanyika kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza itaanza mwaka huu wa 2006/2007 hadi 2010/2011 na awamu ya pili inatarajiwa kuanza mwaka 2012/2013. Awamu ya kwanza inakadiriwa kugharimu jumla ya dola za Kimarekani bilioni 5.59. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tuna tatizo la msongamano mkubwa wa magari katika miji yetu hasa Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya. Katika jiji la Dar es Salaam, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine ina mpango wa kuzifanyia ukarabati baadhi ya barabara ambazo zimeonekana zitasaidia kupunguza msongamano huo. Aidha, Wizara inawahamasisha watu binafsi kuwekeza katika usafiri wa majini katika mwambao wa bahari ya Hindi. Matarajio ya Wizara ni kuwa wawekezaji hao watapatikana katika mwaka 2006/2007. Katika mpango wa muda mrefu, Serikali itafanya upembuzi yakinifu utakaoainisha njia zote za usafiri ikiwa ni pamoja na reli na maji kwa kuhuishwa na Mpango Kamambe (*Master Plan*) wa Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miundombinu bora ya *ICT* inakuza uchumi kwa kuwezesha wawekezaji kuja kuwekeza katika maeneo mbalimbali ya uchumi hapa nchini. Hivi sasa mpango umekamilika wa jinsi mkongo mkuu wa Kitaifa utakavyokuwa. Ili mkongo huo wa kitaifa uweze kuunganika vema na mikongo ya aina hiyo duniani, tunashiriki ipasavyo katika utekelezaji wa mradi wa *East African Submarine Systems* (*EASSY*) ambao unaendelezwa chini ya Jumuia ya Afrika Mashariki na *NEPAD*. Lengo ni kuwa na mhimili wa mawasiliano nafuu ya kimataifa ambao utaunganishwa na km 6,000 za kitaifa

yaani *National Communications Infrastructure Backbone,* hivyo kutoa huduma za mawasiliano ya kimtandao kwa ufanisi na kwa bei nafuu hadi vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebisho ya Sheria, Wizara inaendelea kuzirekebisha sheria nane za sekta ili ziendane na sera na mwelekeo wa uchumi wa soko. Sheria ambazo ziko katika taratibu za kufanyiwa mapitio ni Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*TAA*), Mamlaka ya Hali ya Hewa (*TMA*), Bodi ya Usajili wa Makandarasi (*CRB*), Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (*AQSRB*), Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa *(NBMM),* Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (*ERB*) na ile ya Baraza la Taifa la Ujenzi (*NCC*).

Aidha, Wizara inachukua hatua ya kuandika upya Sheria ya Barabara (*Highway Ordinance*). Wizara imeendelea kuishirikisha sekta binafsi katika kuendeleza miundombinu na kuboresha utoaji huduma za sekta.

Mheshimiwa Spika, Usafiri wa Anga, katika kuendeleza huduma za usafiri wa anga Wizara, imeendelea kufanya mapitio ya Makubaliano ya Usafiri wa Anga (*Bilateral Air Service Agreements*) kati ya Tanzania na nchi nyingine duniani. Hivi karibuni tumefikia makubaliano na China, India na Rwanda. Aidha, Wizara inaendelea na mikakati ya kuboresha viwanja vya ndege kwa kushirikisha sekta binafsi katika uwekezaji na utoaji wa huduma nyingine. Viwanja ambavyo vina mpango wa kushirikisha sekta binafsi ni Mwalimu J.K. Nyerere, Kilimanjaro, Mwanza, Mtwara, Arusha, Shinyanga, Bukoba, Kigoma, Mafia na Tabora. Wizara pia ina mpango wa kupata msaada kutoka Shirika la Kimarekani (*Millenium Challenge Coperation - MCC*) kwa ajili ya kuendeleza viwanja vya ndege vya Mafia na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuboresha huduma za usafiri wa anga, Serikali imekubaliana na Shirika la Ndege la Afrika Kusini (*SAA*) kuvunja mkataba wa ubinafsishaji wa uendeshaji wa *ATCL*.

Majadiliano ya madai kati ya wabia hao yanaendelea. Serikali kwa upande wake imeendelea kuisaidia *ATCL* kwa kuipatia ruzuku ya Shilingi bilioni 6.0 katika mwaka 2005/2006. Katika mwaka 2006/2007 Serikali imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 13.0 ili kuimarisha huduma za usafiri wa ndege nchini.

Mheshimiwa Spika, mchakato mzima wa kubinafsisha Kitengo cha Kontena ulipelekea kuangalia upya muundo mzima wa iliyokuwa Mamlaka ya Bandari ambapo Mamlaka yenyewe ilibadilishwa na kuwa *Ports Authority* ambayo ni *Land Lord Port.* Mamlaka hii mpya ilipewa majukumu kadhaa mapya ambayo ni pamoja na kuwa msimamizi wa vitengo vyote ambavyo vitaendeshwa chini ya sekta binafsi, kuwa mwendeshaji wa vile vitengo ambavyo havijawekwa chini ya sekta binafsi na kusimamia shughuli za kiundeshaji za bandari zote nchini.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Usafiri wa Barabara, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, sekta ya usafiri na uchukuzi kwa njia ya barabara imeendelea kuimarika katika kufanikisha shughuli za kiuchumi na kimaendeleo katika nchi yetu. Uchukuzi wa

mizigo unaochangiwa na sekta ndogo ya barabara ni zaidi ya asilimia 70, na kwa abiria ni zaidi ya asilimia 90. Hivi sasa utoaji wa huduma hizi unakabiliwa na tatizo la kupanda kwa nauli, bei ya mafuta na vipuri kunakotokana na kupanda kwa bei ya mafuta ghafi na kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania. Suala la kupanda kwa nauli linashughulikiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Uchukuzi wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*).

Mheshimiwa Spika, Huduma za Mawasiliano. Matumizi ya teknolojia za kisasa za mawasiliano yameleta mabadiliko makubwa katika maendeleo ya nchi. Mamlaka ya Mawasiliano (*TCRA*) ambayo ndiyo mdhibiti wa sekta ya mawasiliano nchini imeendelea na utaratibu mpya wa utoaji wa leseni ambao unaruhusu muingiliano wa teknolojia. Utaratibu huu unaruhusu utoaji wa leseni kwa wawekezaji katika ngazi za kimataifa, kitaifa, mkoa, wilaya na jamii (*Community Service*).

Hii ina maana kuwa mwekezaji mwenye mtaji mdogo ataweza kuwekeza katika eneo kama vile Wilaya na kutoa huduma pasipo kusubiri hadi kujenga uwezo mkubwa. Inategemewa kuwa utaratibu huu utawezesha kufikiwa kwa lengo la taifa la kufikisha huduma kwa wananchi wote hususani wa vijijini. *TCRA* imeendelea kudhibiti mwenendo wa kampuni za simu na kuandikisha Kampuni mpya. Sekta hii inakua kwa kasi ambapo wateja wa simu za mkononi wamefikia 3,855,190 mwaka 2006 kulinganisha na wateja 126,646 tu mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, Ubinafsishaji/Urekebishaji wa Taasisi za Wizara, katika kipindi cha 2005/2006 Wizara kwa kushirikiana na Tume ya kurekebisha Mashirika ya Umma (*PSRC*) na wadau wengine imeendelea na zoezi la kubinafsisha taasisi zilizo chini yake. Kwa upande wa uendeshaji wa Shirika la Reli (*TRC*) hatua iliyofikiwa hivi sasa ni kuwa Serikali inakaribia kumaliza majadiliano na mkodishwaji, Kampuni ya *RITES* toka India, atakayeendesha Reli hiyo kwa miaka 25 kuanzia mwezi Agosti, 2006.

Kuhusu Shirika la Posta Serikali inaendelea na zoezi la kulirekebisha ili liweze kujiendesha kibiashara zaidi. Jitihada hizo zinaendelea pia kwa Kampuni ya Huduma za Meli katika Maziwa (*MSCL*), Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA),* Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) na Kampuni ya Kukodisha Mitambo (*PEHCOL*). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na juhudi za kuimarisha huduma za hali ya hewa nchini ili utoaji wa tahadhari dhidi ya hali mbaya ya hewa na majanga ya asili ufanyike kwa wakati na kwa usahihi zaidi.

Aidha, Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa kufunga mitambo na vifaa mbalimbali vipya katika maeneo kadhaa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kuongeza ajira kwa Watanzania, Wizara imeendelea kuainisha maeneo yanayoweza kutoa ajira katika sekta ya miundombinu. Maeneo yaliyoanishwa ni pamoja na viwanja vya ndege, ujenzi na ukarabati wa barabara, shughuli za posta, huduma za mawasiliano ya simu, huduma za ufundi na umeme, huduma za bandari, huduma za reli, huduma za hali ya hewa na huduma za usafiri wa

anga. Kwa ujumla inatarajiwa kuwa zaidi ya nafasi 250,000 za ajira au kujiajiri moja kwa moja zitapatikana katika Wizara hii ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Ushiriki kwenye Taasisi za kimataifa, katika kuiwezesha Tanzania kufikia viwango vya kimataifa katika utoaji wa huduma za kisekta, Wizara imeendelea kushirikiana na taasisi na mashirika ya kimataifa yanayohusika na sekta. Ushirikiano huu umesaidia kuboresha viwango vya utendaji katika sekta zetu. Taasisi hizo ni pamoja na Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri wa Majini, *International Maritime Organisation (IMO),* Shirika la Kimataifa la Mawasilino ya Simu *International Telecommunications Union (ITU),* Shirika la Hali ya Hewa Duniani *yaani World Meteorological Organisation (WMO),* Shirika la Posta Duniani *International Postal Union (IPU),* Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga yaani *International Civil Aviation Organisation (ICAO)* na kadhalka.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Sekta kwa Mwaka 2006/2007, napenda sasa kueleza kwa undani zaidi utendaji katika kipindi cha mwaka 2005/2006 na malengo kwa mwaka 2006/2007 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2005, Dira ya Taifa ya Maendeleo *(Vision 2025),* MKUKUTA, Mkakati wa Kushirikiana na Wahisani (*JAS*) pamoja na utekelezaji wa ahadi za viongozi wakuu wa Serikali.

Maeneo yaliyoainishwa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 katika Wizara ni kama ifuatavyo:-

- Kuendelea kuliimarisha Shirika la Reli Tanzania (*TRC*) kwa lengo la kulipa uwezo wa kutoa huduma bora kwa bidhaa na abiria wa ndani na wa nchi jirani. Kwa kufanya hivyo Shirika la Reli litawezeshwa kuwa mhimili wa maendeleo ya Ukanda wa Kati.

- Kuendelea kuimarisha Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA)* ili iweze kuhimili majukumu makubwa zaidi iliyonayo ya kuboresha huduma kwa bidhaa na abiria na kusaidia shughuli za uendelezaji wa Mpango wa Ukanda wa Mtwara.

- Kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa reli mpya za Arusha-Musoma, Isaka-Kigali na Ukanda wa Mtwara ambazo zitaunganisha Bandari ya Mtwara, na mji wa Songea, *Mbamba-Bay,* Mchuchuma na Linganga.

- Kuimarisha Bandari za Kigoma na Kasanga.

- Kuvutia uwekezaji katika miundombinu ya usafiri na uchukuzi wa reli, barabara, maji na anga katika Kanda za Maendeleo ili kuimarisha biashara kati ya nchi yetu na nchi jirani na kufanya wawekezaji kuvutiwa na soko kubwa la bidhaa na huduma zitakazozalishwa.

- Uwekezaji katika kanda hizi utaiwezesha Tanzania kutumia nafasi yake ya kijiografia na kuendeleza wajibu wake wa kuzihudumia nchi jirani zisizo na bandari.

- Kuendelea kuutengenezea mazingira mazuri ya kibiashara Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu J.K.Nyerere yatakayofanya uwe kiungo *(hub)* cha usafiri wa anga kitaifa, kikanda na kimataifa.

- Kulisaidia Shirika la Ndege la Tanzania ili lichukue nafasi yake ipasavyo kuwa Shirika la Ndege la Taifa kwa lengo la kuliwezesha Taifa kufaidika zaidi na mapato yatokanayo na Utalii.
- Kukamilisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe na kuimarisha Viwanja vya Ndege vya Kigoma, Tabora na Shinyanga.

- Kutekeleza mradi wa mabasi ya usafiri wa haraka jijini Dar es Salaam.

- Kuboresha mtandao na huduma za simu nchini.

- Kuendelea kupanua huduma za simu za mezani na za mkononi hadi ngazi ya vijijini.

- Kuhakikisha kuwa huduma za posta nchini zinapanuliwa hadi vijijini ili kuongeza kasi ya usambazaji barua na vifurushi. Aidha, kuimarisha na kupanua mfumo mpya wa mawasiliano unaotumia teknolojia ya kompyuta.

- Kukuza Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili kujenga uwezo wa kuratibu na kuimarisha mfumo huo na kuanzisha Mfuko maalum kwa ajili ya kupeleka huduma za simu na intaneti hadi vijijini.

- Kuifanya Tanzania kuwa kiungo kikuu cha mawasiliano kikanda na kimataifa *(ICT hub)* kupitia *sub marine optic fibre system.*

- Kukamilisha ukarabati unaondelea wa barabara zote kwa kiwango cha lami katika barabara kuu. Barabara hizo ni:- Dodoma – Manyoni, Manyoni – Singida, Singida-Shelui, Nzega-Ilula, Nangurukuru-Mwemkulu-Mingoyo, Mkuranga – Kibiti, Dodoma-Morogoro, Kigoma-Biharamulo-Lusahunga, Tabora-Kaliua-Malagalasi-Kigoma, Usagara-Chato-Biharamulo na Ndundu-Somanga.

- Kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara zifuatazo: Tunduma – Sumbawanga, Marangu – Tarakea – Rongai, Minjingu – Babati – Singida, Rujewa – Madibira – Mafinga, Mbeya– Chunya – Makongorosi, Msimba – Ikokoto – Mafinga, Arusha – Namanga, Tanga-Horohoro na Ukarabati

wa barabara ya Kilwa (DSM), Barabara ya Mandela na Barabara ya Sam Nujoma.

- Kuhimiza maandalizi ya Ujenzi wa daraja la Kigamboni chini ya uongozi wa Shirika la Hifadhi ya Jamii ili kuunganisha Kigamboni na Jiji la Dar es Salaam.

- Kukamilisha Ujenzi wa daraja jipya la Mpiji ambalo litawezesha njia mbadala ya Dar es Salaam - Tanga.

- Kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na ujenzi wa daraja la Mto Kilombero na kukamilisha ujenzi wa daraja la Mto Mwatisi katika mkoa wa Morogoro.

- Kufanya Usanifu wa ujenzi wa daraja jipya la Ruvu.

- Kuanza ujenzi wa Daraja la Umoja (Tanzania na Msumbiji).

- Kuanzisha programu ya Taifa ya usafiri Vijijini.

- Kujenga mwamko wa kuzingatia mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu katika ujenzi wa majengo yanayotumiwa na Umma.

- Kuendelea kujenga nyumba za watumishi wa Serikali kwa ajili ya kuwauzia.

- Kujenga uwezo wa vyombo vya dola kudhibiti na kukabiliana na majanga ya kimaumbile kama tsunami, tetemeko la ardhi, tufani na mvua za kimbunga, mafuriko na ukame mkubwa.

- Kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Iringa-Dodoma-Arusha na kukamilisha ujenzi wa barabara ya Dar es salaam-Dodoma-Mwanza kama mkakati wa kuendeleza mji wa Dodoma ili uweze kuvutia vitega uchumi.
- Kuendelea kuimarisha Mfuko wa Barabara *(Tanzania Road Fund).*

- Kuweka vivutio kwa sekta binafsi ili ishiriki uwekezaji kwenye ujenzi wa miundombinu inayohitajika katika ukuaji wa mji, na katika uwekaji wa huduma mbalimbali zinazokidhi mahitaji ya watumishi wa Serikali na wananchi kwa ujumla.

- Utekelezaji wa baadhi ya maelekezo haya ya Ilani ya Uchaguzi pamoja na ahadi mbali mbali za Viongopzi wa kitaifa yataendelea kujumuishwa katika mipango ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake kwa miaka mitano ijayo.

- Kanda za Maendeleo *(Development Corridors)*

Mheshimiwa Spika, mpango wa maendeleo ya kikanda *Spatial Development Initiative (SDI)* ni mkakati wenye lengo la kuleta maendeleo ya haraka kwenye kanda ambazo hazina mvuto kiuwekezaji bila kuwepo utaratibu wa kuunganisha nguvu na rasimali zilizopo kwenye ukanda husika.Mhimili wake ni katika kuweka miundombinu bora na inayofaa. Mpango huu una lengo la kuibua uchumi wa nchi, kufungua milango ya uwekezaji na kuchochea biashara katika maeneo ambayo hayakuwa na usafiri mzuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali imebuni kanda nne za kusukuma maendeleo haya yaani Ukanda wa Kati, Ukanda wa Mtwara, Ukanda wa Tanga na Ukanda wa Dar es Salaam. Ukanda wa Kati *(Central Development Corridor)* unaunganisha bandari ya Dar es Salaam na nchi za Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC)* na Uganda.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuendeleza Ukanda wa Kati, Meneja wa mradi wa maendeleo ya Ukanda wa Kati aliteuliwa na kuanza kazi rasmi Juni 2005. Aidha, katika ukanda huu Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB),* imetoa msaada wa dola za Marekani milioni 2.5 sawa na asilimia 95 ya gharama ili kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli ya kutoka Isaka hadi Kigali. Asilimia tano (5%) iliyobakia itachangiwa sawa na Serikali za Tanzania na Rwanda.

Mtaalamu mwelekezi *(Consultant)* anatarajiwa kuanza kazi mwezi Septemba 2006. Miradi mingine inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na kubadilisha mataruma ya reli ya kati yenye uzito wa ratili 50 kwa yadi na kuweka yenye uzito wa ratili 80 kwa yadi chini ya msaada wa Benki ya Dunia; mradi wa kuboresha mawasiliano katika reli ya kati *(TRC Telecoms Network)* kwa ushirikiano na Serikali ya Uholanzi, na ujenzi wa bandari za nchi kavu Shinyanga na Mwanza. Mikoa iliyoko katika ukanda huu ni Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza na Kigoma.

Miradi ya barabara kuu za Ukanda wa Kati ni barabara za Morogoro-Dodoma, Dodoma -Manyoni, Manyoni - Singida, Singida - Shelui, Ilula - Tinde - Isaka/Tinde - Nzega, Mwanza -Shinyanga Border, Usagara-Bwanga-Kyamiorwa, Mwandiga-Manyovu, Kigoma-Nyakanazi, Uvinza-Ilunde – Malagarasi/Tabora - Kaliua na usanifu wa barabara toka Kigoma hadi Kidahwe na Tabora hadi Nzega. Barabara hizi nazo ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ukanda wa Tanga, miradi itakayotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa barabara ya Tanga – Horohoro, upembuzi yakinifu wa barabara ya Bagamoyo –Sadani – Tanga, na Bagamoyo – Msata, ukarabati wa Same – Mkumbara – Korogwe, Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga ili kuunganisha na Kenya, uimarishaji wa Kivuko cha Pangani na bandari ya Tanga. Aidha, mchakato wa kujenga reli ya Tanga – Arusha – Musoma unaendelea chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mikoa inayohusishwa na ukanda huu ni Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Mara.

Mheshimiwa Spika, ukanda wa Maendeleo wa Mtwara *(Mtwara Development Corridor)* unaanzia bandari ya Mtwara hadi Mbamba Bay na kuhusisha mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Iringa na Mbeya. Ukanda huu unaunganisha nchi za Tanzania, Msumbiji, Malawi na Zambia. Utekelezaji wa Programu ya Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara unaendelea kupitia miradi mhimili (*Anchor Projects)* ambayo ni pamoja na barabara ya Mtwara – Masasi – Songea – *Mbamba Bay,* Daraja la Umoja baina ya Tanzania na Msumbiji na mradi wa Makaa ya Mawe ya Mchuchuma.

Kuhusu Barabara ya Mtwara – Masasi – Songea – *Mbamba Bay,* kazi ya usanifu wa kina inaendelea katika sehemu ya Songea-Matemanga yenye urefu wa kilometa 200 ikiwa ni maandalizi ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Pia Serikali ya Japan imekubali kugharamia ujenzi wa sehemu ya barabara ya Masasi – Mangaka yenye urefu wa kilomita 54 kwa kiwango cha lami. Serikali inaendelea kutenga fedha za ndani na pia kutafuta fedha kutoka kwa Wahisani mbalimbali ili kuweza kukamilisha ujenzi wa barabara hii. Tunategemea kupata fedha za utekelezaji wa sehemu tofauti tofauti kati ya Matemanga hadi Songea katika mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Mkataba wa Makubaliano, mradi wa Daraja la Umoja *(Unity Bridge)* unatekelezwa kwa gharama ya dola za Kimarekani 26,884,283 zitakazochangiwa kwa pamoja na Serikali za Msumbiji na Tanzania. Katika mwaka 2006/2007 Serikali ya Tanzania imetenga jumla ya shilingi milioni 3,800.00 na Serikali ya Msumbiji imetenga kiasi cha shilingi milioni 4,500.00 kwa ajili ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, ukanda wa Maendeleo wa Dar es Salaam unaenda sambamba na reli ya *TAZARA* na barabara ya Dar es Salaam-Tunduma. Ukanda huu unahusisha mikoa ya Pwani, Morogoro, Iringa na Mbeya. Miradi itakayoendelea kutekelezwa katika kipindi cha mwaka 2006/2007 ni pamoja na ukarabati wa barabara ya Msimba-Ruaha/Ikokoto-Mafinga, Songea-Makambako, Mafinga-Mgololo na Daraja jipya la Ruvu. Aidha, reli ya *TAZARA* kati ya Kitete-Mpanga itaendelea kufanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi na Ukarabati wa Barabara Kuu na za Mikoa, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara iliendelea kutekeleza miradi ya ukarabati na ujenzi wa Barabara Kuu mpya katika mfumo wa kanda kuu za usafirishaji (*Trunk Roads Transport Corridors*). Utaratibu huu utahakikisha kwamba barabara zote za kila ukanda zinapitika na kutoa usafiri wa uhakika kati ya kanda moja na nyingine na hivyo kuiwezesha Tanzania kutumia kwa ukamilifu faida ya kijiografia iliyo nayo katika kuziunganisha bandari zetu na nchi tunazopakana nazo.

Mheshimiwa Spika, Mradi Maalum wa Ujenzi wa Barabara Kuu (*Special Project*), katika kupunguza tatizo la kuwa tegemezi kwa wahisani na kuongeza kasi ya ujenzi wa barabara nchini, Serikali ilianzisha mpango maalum wa kutekeleza miradi ya barabara kwa kutumia fedha za ndani. Mpango huu ulianza rasmi katika mwaka 2001/2002 ambapo Wizara yangu imekuwa ikitekeleza miradi ya ujenzi wa barabara

zifuatazo; Somanga-Masaninga na Daraja la Mto Matandu (km 33), Nangurukuru-Mbwemkulu-Mingoyo (km 190) na barabara ya Dodoma-Manyoni-Singida (km 245).

Mikataba ya ujenzi wa barabara hizi ilisainiwa mwezi Februari 2003 na tayari ujenzi wa barabara ya Somanga-Masaninga na Daraja la Mto Matandu umekamilika. Ujenzi wa barabara ya Nangurukuru-Mbwemkulu-Mingoyo na barabara ya Dodoma - Manyoni - Singida unaendelea na uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, Daraja la Umoja kati ya Tanzania na Msumbiji ambalo mkataba wake wa ujenzi ulisainiwa mwezi Oktoba, 2005 linajengwa kwa kutumia fedha za serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 Wizara itaendelea na utekelezaji wa miradi ya barabara kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005.

Katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2005 hadi 2010 maeneo yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na kukamilisha miradi yote ya barabara inayoendelea ambayo ilianzishwa wakati wa Serikali ya Awamu ya Tatu pamoja na kazi za matengenezo ya barabara, na kuanza miradi mingine mipya. Orodha kamili ya miradi ya barabara itakayotekelezwa katika mwaka 2006/07 ni kama ilivyoonyeshwa katika Kiambatisho Na. 1 (Barabara Kuu) na Kiambatisho Na. 2 (Barabara za Mikoa).

Mheshimiwa Spika, Usalama Barabarani na Udhibiti wa Uzito wa Magari, Wizara inaendelea kudhibiti uzito wa magari kwa kutumia mizani zisizohamishika na zinazohamishika katika barabara zote kuu. Aidha, Wizara inafanya utafiti wa aina mpya ya teknolojia na mbinu za kupambana na makosa yanayosababisha ajali za barabarani, hasa kutokana na tabia za madereva na ubovu wa magari, kwa lengo la kufanya mabadiliko ya sheria na kanuni za sheria ya barabarani ili ziweze kukidhi matakwa ya hali ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Matengenezo (*Maintenance*) ya Barabara. Sera ya Wizara kuhusu kazi za barabara ni kutoa kipaumbele kwa kazi za matengenezo ya barabara kwa lengo la kutunza na kulinda rasilimali iliyowekezwa kwenye ujenzi na ukarabati ili kuhakikisha barabara zinakuwa katika hali nzuri kwa muda mrefu kabla ya kuhitaji kufanyiwa ukarabati au kujengwa upya na hivyo kulipunguzia Taifa gharama kubwa zinazoambatana na kazi hizo. Kadhalika, ni dhahiri kuwa kudumisha ubora wa barabara kwa wakati wote kuna manufaa makubwa kiuchumi na kijamii hususan katika kudhibiti gharama za uchukuzi, kudumisha maisha ya vyombo vya uchukuzi, kupunguza ajali za barabarani na kuhakikisha kufikika kwa sehemu zote nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia manufaa makubwa yanayotokana na matengenezo hayo ya barabara, Wizara ya Miundombinu inaendelea na utekelezaji wa mikakati iliyojiwekea ya matengenezo ya kawaida (*routine maintenance*), matengenezo maalum (*periodic maintenance*), matengenezo ya sehemu korofi (*spot improvement*), matengenezo ya dharura (*emergency*), matengenezo makubwa (*backlog maintenance*) na matengenezo ya madaraja (*bridges maintenance*). Mwelekeo wa sasa ni kutekeleza sehemu kubwa ya kazi za matengenezo ya barabara kwa kutumia makandarasi ili kuongeza ufanisi. Hivyo, Wizara inafanya jitihada kuimarisha matumizi ya taratibu za

zabuni za usimamizi wa mikataba ikiwa ni pamoja na kusaidia kuinua utendaji wa makandarasi nchini katika mpango mzima wa kuimarisha mtandao wa barabara nchini. Hivi sasa zaidi ya asilimia 90 ya kazi za matengenezo ya barabara zinafanywa na makandarasi.

Mheshimiwa Spika, usafiri na uchukuzi kwa njia ya Barabara, katika kipindi cha mwaka 2005/2006. Sekta ya usafiri na uchukuzi kwa njia ya barabara imeendelea kuimarika katika kufanikisha shughuli za kiuchumi na kimaendeleo nchini.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA), Shirika la UDA liliendelea kutoa huduma za usafiri katika Jiji la Dar es salaam. Katika kipindi cha 2005/2006 Shirika lilikuwa na wastani wa mabasi 22 yaliyoenda barabarani kwa siku. Shirika lilinunua mabasi mapya na kufufua mabasi 10 yaliyokuwa yamesimama. Jumla ya abiria 1,661,296 walibebwa katika mwaka 2005/2006, ikilinganishwa na Mwaka 2004/2005, ambapo jumla ya abiria 1,428,798 walibebwa hii ikiwa ni ongezeko la asilimia 16. Jumla ya mapato kwa kipindi hiki yalikuwa Shilingi milioni 660.397 ikilinganishwa na Mwaka 2004/2005 ambapo jumla ya Shilingi milioni 545.209 zilipatikana.

Hii ni ongezeko la asilimia 21. Katika kipindi cha 2006/2007 Wizara itaendelea na taratibu za kurekebisha mfumo wa utendaji wa shirika ili liweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Usafiri na Uchukuzi kwa Njia ya Reli, Shirika la Reli Tanzania (*TRC*), katika mwaka 2005/2006, Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kuimarisha *TRC*. Hatua hizo ni pamoja na kukodisha injini 10 kutoka India, kuagiza reli, mataruma na vifaa vya kutosha kutandika upya kilometa 47 za njia ya reli. Vifaa hivi vinatarajiwa kuwasili nchini mwaka 2006/2007. Katika kipindi hicho Shirika lililenga kusafirisha abiria 648,800 lakini likaweza kusafirisha abiria 674,029 na kupita lengo kwa asilimia 4 ikilinganishwa na mwaka 2004/2005 ambapo Shirika lilisafirisha abiria 627,969. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2005 Shirika lilisafirisha tani 1,128,508 na kupita lengo kwa asilimia 3, licha ya upungufu mkubwa wa mabehewa na vichwa vya treni, pamoja na ubovu wa njia ya reli.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha 2006/2007, Shirika litaendelea na utekelezaji wa mradi wa kutandika nyaya *(optic fibre)* za mawasiliano ya simu kati ya Dodoma na Tabora. Aidha Shirika litaendelea kutekeleza mradi wa kutandika upya reli za uzito wa ratili 80 badala ya 56 ambapo jumla ya kilometa 26.5 katika sehemu zilizochakaa zaidi kati ya Tabora na Kigoma zitakarabatiwa. Shirika kwa msaada wa Serikali ya Ubeligiji litaendelea na mradi wa kuimarisha kitengo cha kontena cha Ilala na kujenga vitengo vingine katika miji ya Mwanza na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA),* katika mwaka 2005/2006, *TAZARA* ilisafirisha tani 315,718 za mizigo ikilinganishwa na tani 350,000 zilizopangwa kusafirishwa, sawa na asilimia 90.2% ya lengo. Mamlaka pia ilisafirisha abiria 478,292 kati ya abiria 550,000 waliopangwa kusafirishwa, sawa na

asilimia 87.0 ya lengo. Mamlaka pia inaendelea kukamilisha makubaliano ya ushirikiano na Kampuni ya *Konkola Copper Mine* (*KCM*) ya Zambia ili kukarabati injini za treni 6 kwa lengo la kukidhi mahitaji ya usafirishaji wa abiria na mizigo.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, lengo la Mamlaka ni kuongeza ufanisi katika kutekeleza lengo la kusafirisha mizigo tani 700,000 na abiria 1,100,000 na hivyo kuiongezea Mamlaka mapato zaidi. Aidha, Serikali za Tanzania na Zambia zinaendelea na mazungumzo na Serikali ya Watu wa China kuhusu kuboresha utendaji wa Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, Usafiri na Uchukuzi Kwa Njia ya Maji. Huduma za Usafirishaji kwa njia ya maji zimegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni uchukuzi baharini, huduma za bandari na uchukuzi katika maziwa. Uchukuzi wa baharini katika kipindi cha 2005/2006 umekuwa ukiendeshwa na kampuni kutoka nje ya nchi na kwa kiasi kidogo kampuni za ndani ya nchi kama Kampuni ya Meli ya China na Tanzania (*SINOTASHIP*). Huduma za bandari zimekuwa zikitolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*). Uchukuzi katika maziwa unaendelea kutolewa na Kampuni ya Huduma za Meli katika Maziwa (*MSCL*) pamoja na sekta binafsi. Serikali imefanya juhudi za kuimarisha na kuboresha miundombinu ya huduma za usafiri majini na kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha sekta binafsi kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*), Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*) imeendelea kupata mafanikio makubwa katika kuziendeleza bandari za mwambao kwa kuzifanya kuwa za kisasa na zenye kuhimili ushindani mkubwa kibiashara kikanda.

Hata hivyo, Mamlaka iliendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa miundombinu chakavu katika bandari hizi, kuzorota kwa hali ya uchumi na kisiasa katika nchi zitumiazo bandari za Mamlaka zikiwemo *DRC* na Burundi, uwezo mdogo wa vyombo vya usafirishaji wa nchi kavu ambao unaathiri uondoshaji wa bidhaa zinazopitia bandarini, kuongezeka kwa ushindani wa kibiashara katika bandari za ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika pamoja na mabadiliko ya kibiashara. Changamoto hizi zimekuwa zikipunguza utendaji wa Mamlaka kibiashara na kimapato kwa karibu asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, kipindi cha 2006/2007 Mamlaka itafanya utafiti kubaini mahitaji muhimu *(Ports Master Plan Study).* Aidha, Mamlaka itaboresha maeneo ya kazi ili kulinda ufanisi na ubora wa rasilimali iliyopo, kuinua uwezo wa bandari kwa kukarabati na kubadilisha vifaa na maeneo ya kuhudumia meli na mizigo. Mpango mwingine ni ununuzi wa pantoni ya kupokelea abiria na mizigo kutoka kwenye meli *(landing pantoon)* katika bandari ya Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Uchukuzi wa Masafa Marefu Baharini, Kampuni ya Meli ya Serikali ya China na Tanzania (*SINOTASHIP*), Kampuni ya meli ya *SINOTASHIP*

inayojishughulisha na usafirishaji kwa meli wa masafa marefu baharini inamilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China. Katika mwaka 2005 kampuni ilikuwa na meli tatu zenye uwezo wa kubeba jumla ya tani 46,645 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2005, kampuni ilifanya biashara pungufu kwa asilimia 17.6 kutokana na mfumuko mkubwa wa bei ya mafuta na uhaba wa mizigo toka pwani ya Mashariki mwa Afrika. Kampuni ina mpango wa kuongeza meli moja katika kipindi cha mwaka 2006/2007 na kusafirisha tani 250,000 na kupata faida ya dola milioni 1.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Usafiri na Uchukuzi katika Maziwa, katika mwaka 2005/2006 Kampuni ya Huduma za Meli kwenye Maziwa (*MSCL*) iliendelea kutoa huduma za uchukuzi na usafiri kwenye maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa ikishirikiana na sekta binafsi. Katika kipindi hicho *MSCL* ilisafirisha asilimia 28 zaidi ya mizigo ikilinganishwa na mwaka 2004/2005. Aidha, kampuni ilisafirisha abiria pungufu kwa asilimia 1.0 ikilinganishwa na mwaka 2004/2005. Kampuni iliweza kukusanya jumla ya mapato ya shilingi bilioni 6.66 ikilinganishwa na shilingi bilioni 5.64 zilizokusanywa mwaka 2004/2005. Katika mwaka 2006/2007 Kampuni imekusudia kuzifanyia matengenezo meli zake ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, uchukuzi katika maziwa ulikabiliwa na changamoto ya kushuka kwa kina cha maji katika maziwa makuu na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa wakati wa kuegesha meli, na kushindwa kubeba abiria na mizigo kwa uwezo wake. Hali hii ilisababisha kushuka kwa shehena za mizigo na abiria katika bandari zetu hasa ziwa Tanganyika. Pia, kuna tatizo la ajali linalohusisha vyombo vidogo vya abiria, mizigo na uvuvi. Kwa kuzingatia umuhimu wa usalama wa vyombo vya majini, *SUMATRA* imeendelea kuimarisha ukaguzi wa usalama wa vyombo hivi na kuwaelimisha Wadau umuhimu wa kuzingatia sheria za usalama wa vyombo vya usafiri majini.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*), katika mwaka 2006/2007, Mamlaka inatarajia kutekeleza majukumu kwa kuandaa semina, warsha na kutumia redio, television, magazeti, vipeperushi, na pia kwa kushirikiana na wadau ili kuweza kuboresha ufanisi wa utoaji mizigo bandarini, kuimarisha ukaguzi wa vyombo vya usafiri majini, kuandaa mpango wa usalama wa usafiri wa reli na kutoa leseni za vyombo vya usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, *SUMATRA* itaendelea kutekeleza majukumu ya ukaguzi wa ulinzi na usalama wa vyombo vya usafiri majini kwa kuzingatia sheria ya *Merchant Shipping Act* 2003 na kusimamia viwango vya huduma na sheria za kimataifa zinazosimamiwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini (*IMO*). Mamlaka inajenga kituo cha kuongozea meli na kutafuta meli zilizopotea au kupata ajali katika eneo la bandari ya Dar es Salaam kwa kutumia vifaa vya mawasiliano vya ubora wa kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Usafiri wa Anga. Huduma za usafiri wa anga ziliendelea kutolewa katika kiwango cha kuridhisha. Abiria waliosafiri kwa ndege ndani na nje ya nchi walikuwa 2,218,594 ikilinganishwa na abiria 1,950,383 mwaka uliopita. Hili ni ongezeko la asilimia 13.7. Aidha, idadi ya abiria waliosafiri humu nchini katika kipindi cha mwaka 2005/2006 iliongezeka kwa asilimia 12.4 ambapo idadi ya safari za ndege za kimataifa na za ndani iliongezeka na kufikia safari za ndege 188,594 mwaka 2005/2006, sawa na ongezeko la asilimia 7.8.

Mheshimiwa Spika, Usalama wa Usafiri wa Anga. Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga (*TCAA*) imeendelea kutoa taarifa za usalama wa anga (*aeronautical information services*) kwa saa 24 katika uwanja wa kimataifa wa Mwalimu J. K. Nyerere na kwa saa 13 katika viwanja vya Arusha, Dodoma, Mwanza na Zanzibar. Aidha imeendelea kutoa huduma za kuongoza ndege saa 24 katika kituo kikuu cha mawasiliano ya kuongoza ndege (*ACC*- Dar es Salaam) kinachojumuisha nchi za Tanzania, Burundi na Rwanda; uwanja wa ndege wa kimataifa wa Mwalimu J. K. Nyerere, uwanja wa Mwanza, na uwanja wa kimataifa wa Zanzibar; kwa saa 13 katika viwanja vya Arusha, Dodoma, na Pemba na kwa saa 8 katika viwanja vya Kigoma, Tabora, Iringa, Mbeya, Mtwara, Songea na Tanga. Pia Mamlaka imekamilisha kufunga mtambo wa usambazaji wa mawimbi ya *radio* (*en-route VHF relay station*) huko Matogoro, Songea.

Mheshimiwa Spika, vifaa vya *radio* vya kuchunguza hali ya utendaji wa mitambo ya kuongozea ndege vilifungwa katika kiwanja cha Arusha na vifaa vya *radio* za dharura (121.500mhz) vilifungwa kwenye viwanja vya Dodoma na Kigoma. Mamlaka ilikamilisha zoezi la kuhakiki na kudhibiti viwango sahihi vya huduma ya mitambo ya kuongoza ndege kulingana na viwango vya Shirika la Kimataifa la Usalama wa Anga (*ICAO*) katika viwanja vya Mwalimu J. K. Nyerere, Kilimanjaro, Zanzibar na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, nchi za Afrika ya Mashariki kupitia mradi wa *Civil Aviation Safety Project;* zimeweza kuboresha sheria za usalama wa anga na kuzifanya ziwe linganifu kwa nia ya kutekeleza ibara ya 92 ya mkataba wa Jumuia ya Afrika ya Mashariki ya kuongeza ushirikiano katika matumizi ya rasilimali pamoja na watalaam. Ili kuhakikisha usalama wa viwanja vya ndege, ukaguzi wa mipangilio ya usalama (*airport security arrangements)* katika kiwanja cha Kimataifa cha Mwalimu J. K. Nyerere na programu ya usalama (*Civil Aviation Security Programme)* ulifanywa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (*ICAO*). *TCAA* inaendelea kufanya kaguzi kama hizi katika viwanja vyote nchini ili kutekeleza viwango vya usalama wa anga na kufunga mitambo na vifaa mbali mbali katika viwanja vya Dar es Salaam, Zanzibar, Mwanza, Kilimanjaro, Songwe, Tabora na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Viwanja vya Ndege, katika mwaka 2005/2006, Mamlaka ya viwanja vya Ndege Tanzania (*TAA*) iliendelea kuhudumia viwanja vya ndege kwa kuzingatia sera ya kuwezesha viwanja vya ndege kujiendesha kibiashara, kujitosheleza na kujitegemea. Mamlaka inaendelea na matengenezo ya miundombinu na uboreshaji wa mitambo katika kiwanja cha Mwalimu J. K. Nyerere kwa kukarabati njia ya kurukia ndege na maegesho ya ndege. Katika kuimarisha usalama wa viwanja vya ndege hatua

zilizochukuliwa ni pamoja na ununuzi wa mitambo ya kutambua mabomu, ukaguzi wa mizigo na abiria na ya kutambua vyuma na vitu vingine vya hatari. Kuhusu ujenzi wa kiwanja kipya cha Songwe, Mbeya kazi zilizotekelezwa ni pamoja na Ujenzi wa jengo la kufikia abiria (*arrival terminal),* kituo cha zimamoto na kituo cha kuongozea ndege. Kuhusu kiwanja cha ndege cha Mwanza, matengenezo yaliyofanywa ni ujenzi wa uzio kuzunguka kiwanja kwa ajili ya kuimarisha usalama na sehemu ya maegesho ya ndege za mizigo na abiria pamoja na viungio.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 Mamlaka inatarajia kutekeleza yafuatayo: Kuweka mtambo maalum wa kuona kwa njia ya televisheni (*CCTV*) katika kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Mwalimu J.K.Nyerere. Kufanya matengenezo ya miundombinu na uboreshaji wa mitambo katika kiwanja hicho kwa kushirikisha sekta binafsi katika uendelezaji wa viwanja vya ndege nchini katika matengenezo ya maeneo ya maegesho ya ndege za mizigo na abiria pamoja na viungio vyake kwenye uwanja wa Songwe. Kununua na kusimika mitambo kwa ajili ya kuhudumia na kuhakiki abiria na mizigo. Kazi za ujenzi wa kiwanja hicho inatarajiwa kukamilika ifikapo Julai 2007. Kampuni ya Ndege Tanzania (*ATCL*), iliendelea kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa kiwango cha wastani. Hadi kufikia mwisho wa mwaka 2005 *ATCL* iliweza kuhudumia vituo 8. Hivi sasa Kampuni ina ndege 2 aina ya *Boeing* 737-200 ambapo moja ni mali ya Kampuni na moja ni ya kukodi. *ATCL* inakabiliwa na changamoto kubwa ambayo ni kufanya biashara endelevu ili kukabili ushindani uliopo kwenye usafiri wa anga ndani na nje ya nchi ambapo mashirika mengine yanaendesha biashara ya usafiri wa anga. Hivi sasa Serikali iko katika hatua za kuvunja mkataba na Shirika la Ndege la Afrika ya Kusini (*SAA*) huku ikitafuta mustakabali wa biashara ya usafiri wa ndege wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kampuni inayosimamia Mali za iliyokuwa *ATC* (*ATHCO*), katika mwaka 2005/2006 *ATHCO* ilikusanya jumla ya Shilingi bilioni 1.24 kutokana na mauzo ya nyumba, ada ya tenda, makusanyo ya madeni na mauzo ya mali nyinginezo. Aidha, katika kipindi 2006/2007 Kampuni inatarajia kukamilisha taratibu za kuhamisha umiliki wa nyumba tano zilizoko Johannesburg, Lusaka na Nairobi, kuuza mali zisizohamishika zilizoko *KIA*, kukamilisha uuzaji wa nyumba zilizoko Dar es salaam, *KIA*, Harare na Lusaka. Pia kukamilisha kesi 27 zilizopo mahakamani na katika vyombo mbalimbali. Wakala wa Ndege za Serikali (*TGFA* katika kipindi cha 2005/2006 uliendelea kufanya kazi zake kwa ufanisi kwa kutumia ndege nne katika kutoa huduma zake kwa viongozi. Katika mwaka 2006/2007 Wakala una lengo la kudumisha na kuboresha usalama, aina na ubora wa huduma zake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006 Wakala wa Barabara *TANROADS* ilizifanyia matengenezo barabara kuu na barabara za mikoa zenye urefu wa kilomita 13,799 na madaraja 1,503. Kati ya hizo, kilometa 4,789.7 na madaraja 799 ni kwa upande wa barabara kuu na kilometa 9,009.6 na daraja 704 ni kwa barabara za mikoa. Fedha zilizotumika ni shilingi 22,893.772 milioni kutoka Mfuko wa Barabara ambapo shilingi 15,512.562 milioni zilitumika kwenye barabara kuu na shilingi 10,381.210 milioni kwenye barabara za mikoa. Aidha, Wakala utaongeza kasi ya kutoa ushauri wa kiufundi kwa Wahandisi wa Halmashauri za Wilaya na Miji, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kusimamia kazi za barabara Wilayani kwa kushirikiana na

Wahandisi wa Mikoa. Utaratibu huu una lengo la kuboresha utendaji na matumizi ya fedha (*Value for Money*).

Mheshimiwa Spika, Matengenezo kutokana na fedha za Wahisani. Wahisani mbalimbali wanashiriki moja kwa moja katika miradi ya matengenezo ya barabara; kama vile *EU* katika mikoa ya Ruvuma na Iringa chini ya mradi wa *Ruvuma and Sourthen Iringa Roads Maintenance* (*RUSIRM*), mradi wa *STABEX* unaohusisha mikoa minane inayolima zao la kahawa ya Arusha, Kilimanjaro, Kagera, Tanga, Mbeya, Ruvuma, Kigoma na Mara. Serikali ya Japan inafadhili mradi wa miaka mitatu wa kuongeza uwezo wa usimamizi wa matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Matengenezo ya Barabara mwaka 2006/2007, mpango wa matengenezo ya barabara pamoja na madaraja kwa mwaka 2006/2007, ni kuzifanyia matengenezo barabara kuu na barabara za mikoa zenye urefu wa kilomita 28,801.25 na madaraja 2,177. Kati ya hizo, kilometa 9,804.30 na madaraja 1,117 ni kwa upande wa Barabara Kuu na kilometa 18,996.95 na daraja 1,060 ni kwa Barabara za Mikoa. Fedha iliyopangwa kutumika ni shilingi 90,670.869 milioni ambapo shilingi 53,322.37 milioni ni za Mfuko wa Barabara, shilingi 870 milioni ni kutoka Serikali Kuu na shilingi 36,478.499 milioni ni kutoka kwa wahisani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo ya Serikali (*TBA*), katika mwaka 2005/2006 Wakala uliweza kukusanya jumla ya shilingi 11,998 milioni ambapo kati ya hizo, shilingi 8,092.3 milioni zilitokana na mauzo ya nyumba za Serikali. Aidha, Wakala uliweza kujenga majengo 3 ya ghorofa Dar es Salaam, kuendeleza ujenzi wa nyumba katika Wilaya mpya za Chato, Mkinga, Siha na Nanyumbu. Kukamilisha ujenzi wa nyumba kubwa 50 kati ya 300 Dodoma ambapo nyumba nyingine 250 ziko katika hatua za mwisho, kukamilisha ujenzi wa nyumba 10 za gharama nafuu Mkoani Manyara, nyumba 7 Mkoani Kagera na 10 Mkoani Singida. Aidha, Wakala uliendelea kukamilisha ujenzi wa nyumba 38 mikoani, ujenzi wa nyumba 91 za Viongozi Dar es Salaam, Ujenzi wa nyumba za Watumishi katika Mikoa yote Tanzania Bara, kukarabati nyumba za Serikali na kuendelea na ujenzi wa ofisi za Makao Makuu ya Wakala katika Mkoa wa Manyara. Jumla ya fedha zilizotumika ni shilingi 9,808.64 milioni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 Wakala umepanga kujenga majengo 4 ya ghorofa Dar es Salaam na majengo mawili Arusha. Kujenga nyumba za viongozi katika mikoa mbali mbali zikiwemo nyumba za Majaji. Kuendelea na matengenezo ya kawaida ya nyumba pamoja na ofisi za Serikali, kutafuta viwanja jijini Dar es Salaam kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na kuhifadhi jengo moja la kihistoria Mkoani Lindi. Wakala wa Ufundi na Umeme (*TEMESA*), Wakala wa Ufundi na Umeme *(Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency* (*TEMESA*), unashughulikia matengenezo ya magari na mitambo, pikipiki, mifumo ya umeme, mabarafu na vifaa vya Elektroniki. Aidha, Wakala unaendesha vivuko vya Serikali na ukodishaji wa magari na mitambo. Katika mwaka 2005/2006, Wizara itafanya mapitio ya majukumu ya *TEMESA* kwa lengo la kuainisha shughuli ambazo zitaendelea kufanywa na Wakala kulingana na malengo mapya ya Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) ni msimamizi mkuu wa shughuli za mawasiliano, posta na utangazaji nchini. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006. Mamlaka imeendelea na shughuli zake kwa ufanisi. Katika jitihada zake za kusogeza huduma karibu na wadau, Mamlaka imefungua ofisi za kanda katika mikoa ya Arusha, Mwanza na pia Zanzibar. Aidha, Mamlaka imenunua mitambo minne ya kudhibiti masafa ili kupanua vituo hivyo kwenye mikoa ya Arusha, Mbeya, Mwanza na Dar es salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mipango ya Mamlaka kwa mwaka 2006/2007 ni kuwa na wataalamu na vitendea kazi vya kutosha, kuhakikisha watoa huduma za takwimu *(data)* na intaneti (*Internet Service Providers*) wanajiunganisha kwenye mitambo ya kuunganisha mawasiliano hayo kitaifa (*Internet Exchange Points (IXPs*) ili kupunguza gharama kwa watumiaji kwa kutotumia njia na masafa ya kimataifa wakati wa kufanya mawasiliano ndani ya nchi, kuwezesha nchi kuwa na mhimili wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya kisasa na yenye uwezo mkubwa na kuendelea kushirikiana na Baraza la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano pamoja na jumuiya za watoa huduma za mawasiliano ili kuhakikisha kuwa viwango vinavyotozwa vinakuwa vya bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*), hadi kufikia Mei, 2006 *TTCL* ilikuwa na wateja wapatao 145,000 ikilinganishwa na wateja 154,420 kwa mwaka 2005. Kupungua kwa idadi ya watumiaji wa huduma ya simu za msingi kunatokana na wateja wengi kutumia zaidi huduma za simu za mkononi. Huduma hii ya simu za msingi imekuwa ikitumika zaidi sehemu za maofisini na nyumbani. Katika mwaka 2005/2006, Kampuni ilikamilisha mradi wa uboreshaji wa huduma kwa wateja kwa kutumia teknolojia ya *Asymetric Digital Subscriber Lines* (*ADSL*). Aidha, Kampuni imeweka mitambo mipya katika miji ya Nachingwea, Liwale, Ruangwa, Itigi, Malya, Ngudu na Misungwi. Kazi ya kuondoa mitambo 23 ya kukoroga *(manual boards)* iliyobaki kote nchini inaendelea. Ujenzi wa mitambo hiyo unategemewa kukamilika katika mwaka huu wa 2006/2007. Miradi mingine iliyokamilishwa ni ujenzi wa njia kuu (*Digital Microwave Backbone*) na uwekaji wa mitambo mipya ya *microwave* katika njia kuu mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa 2006/2007, *TTCL* imepanga kutumia jumla ya Shilingi bilioni 74 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wake wa maendeleo. Miradi itakayotekelezwa ni ujenzi wa Njia kuu za *Digital Microwave* kati ya Dar es Salaam na Dodoma na Dar es Salaam/Tanga/Arusha. Aidha, upanuzi utafanyika kutoka njia 1,890 za sasa kufikia njia 3,780. Pia mitambo mipya itawekwa kati ya Tanga na Arusha na kuondoa mitambo michakavu ambayo vipuri vyake havipatikani.

Hali kadhalika, mitambo itawekwa kati ya Dodoma na Arusha kupitia Babati na hivyo kuwezesha kupatikana njia nyingine mbadala kwenda na kutoka Arusha. Kazi nyingine itakayofanyika ni uwekaji wa mitambo ya kuwezesha kupata huduma bora za takwimu na intaneti katika makao makuu ya Mikoa na baadhi ya Wilaya. Uwekaji wa njia kuu kwa kutumia Mikongo ya Kigae (*Optical Fibre Cable*) ili kuboresha huduma za mawasiliano. Sehemu zitakazonufaika na huduma hii ni Dar es Salaam/Dodoma kwa kutumia njia iliyojengwa na *TRC*, Dar es Salaam/Arusha kwa kutumia njia inayokusudiwa kujengwa na *TANESCO* na Arusha/Musoma/Mwanza itakayojengwa na

*TTCL*. Miradi hii inategemewa kukamilika ifikapo Machi, 2007. Aidha, katika jiji la Dar es Salaam kutawekwa mtandao wa *optical fibre* ili kuimarisha uunganishaji wa majengo na wateja wakubwa ili wapate huduma bora na za kisasa.

Mheshimiwa Spika, *TTCL* ina lengo la kuboresha mawasiliano na nchi zingine kwa urahisi zaidi kwa kutumia mikongo ya kigae itakayopitishwa chini ya bahari ya Hindi (*Submarine Optical Fibre Cable*) kuanzia Durban hadi Djibouti kupitia Dar es Salaam. Huduma hii pia itaboresha njia za mawasiliano kati ya nchi za Afrika Mashariki na nchi za mabara ya Ulaya na Asia. Huduma hii itakuwa na uwezo mkubwa na itapunguza gharama za mawimbi ya sauti kupitia kwenye *satélite*. Aidha, *TTCL* itakamilisha uboreshaji wa huduma kwa kuondoa simu za kukoroga na kuweka mitambo ya kisasa kwenye vituo vya Mtera, Mvumi, Mwakaleli, Lwangwa, Litembo, Liuli, Itigi, Misungwi, Ngudu, Mallya, Malampaka, Urambo, Sikonge, Ruangwa, Nachingwea, Mikindani, Ndanda, Makiungu, Liwale na Kaliua. Kazi hii itakamilika ifikapo Juni, 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Kampuni ya Simu 2000, imeuza nyumba tisa na viwanja vitatu na kufanikiwa kulipa kiasi cha shilingi bilioni 3.97 kwa Shirika la Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* ambazo ni pensheni na kamisheni. Aidha, Kampuni iliweza kuchangia Hazina kiasi cha shilingi bilioni 2.0.

Kampuni imekamilisha ulipaji wa deni la shilingi bilioni 10.96 la pensheni la wafanyakazi wa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki, waliorithiwa na Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)*. Kampuni inaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuuza mali zilizobakia na kutatua matatizo yanayojitokeza ya wastaafu hao, ikiwa ni pamoja na kesi zilizorithiwa na zilizojitokeza katika uendeshaji wa kampuni na ukamilishaji wa miliki ya baadhi ya mali zenye utata, ambazo hazijauzika.

Mheshimiwa Spika, huduma za simu za mkononi zimeendelea kupanuka katika Mikoa yote Tanzania Bara na Visiwani. Huduma hizi zimeendelea kutolewa na Kampuni za *Vodacom, Celtel, Tigo* na *Zantel*. Hadi kufikia Mei, 2006 kampuni hizi zilikuwa na wateja 3,855,190 waliounganishwa na huduma ya simu za mkononi, ikilinganishwa na wateja 3,389,787 kwa mwaka 2005. Ongezeko hili linaonyesha kuwa, huduma ya simu za mkononi imekuwa sehemu ya mahitaji muhimu ya kila siku kwa wananchi katika shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005, Shirika liliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kiwango cha wastani. Katika kipindi hiki, barua zilizotumwa na kusambazwa kupitia mtandao wa Posta ndani ya nchi, zilikuwa milioni 17.7 zikiwa ni pungufu kwa asilimia nane, ikilinganishwa na milioni 19.4 zilizotumwa mwaka 2004. Barua zilizotumwa nje ya nchi zilikuwa milioni 7.9 ambazo ni ongezeko la asilimia 12. Vifurushi vilivyotumwa katika soko la ndani vimeongezeka kwa asilimia nane hadi kufikia vifurushi 44,277 vya mwaka 2005.

Vifurushi vilivyotumwa nje ya nchi vilipungua kwa asilimia tano kutoka vifurushi 6,921 vya mwaka 2004 hadi kufikia vifurushi 6,541 vya mwaka 2005. Barua zilizosajiliwa Posta zilizotumwa katika soko la ndani katika kipindi cha mwaka 2005, zilikuwa 428, 516 ambazo ni pungufu kwa asilimia 19 zikilinganishwa na rejista 529,158 za mwaka 2004. Pia rejista zilizotumwa katika soko la nje zilikuwa 60,368 zikiwa ni pungufu kwa asilimia 14 zikilinganishwa na rejista 70, 729 za mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Shirika limekusudia kutumia teknolojia ya kompyuta katika mawasiliano. Mradi huu utahusisha utoaji wa huduma kwa njia ya kompyuta katika ofisi zote kuu za posta za Mikoa na kuimarisha biashara za ki-electroniki *(e-business),* kuboresha Majengo ya Posta, kujenga majengo mapya ya Wilayani, kufungua posta ndogo katika maeneo ya Kicheba (Tanga), Bereko (Dodoma) na Posta kamili katika maeneo ya Nyakato (Mwanza) na Namanga (Arusha). Aidha, Shirika litakamilisha awamu ya mwisho ya Mradi wa *Counter Automation.*

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya uchumi wa soko, jamii inaweza kutumia huduma za *ICT* kuweza kupata masoko, biashara, elimu, huduma za afya, bei za mazao na pembejeo, hali ya hewa, taarifa za utalii na usafiri. Hii inadhihirisha kuwa *ICT* ni teknolojia mtambuka, inayotoa fursa katika maendeleo ya sekta zote za kijamii na kiuchumi.

Kwa kuzingatia mabadiliko ya mifumo yanayoendelea katika sekta ya mawasiliano, Tanzania imeweza kuwa na mafanikio mbalimbali katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT)* kwa kuwa na Kituo cha Kupitishia Mawasiliano ya *Internet (Tanzania Internet Exchange Point),* chenye lengo la kuhakikisha watumiaji wa intaneti wanabadilishana mawasiliano bila ya kupitia nchi mbadala na hivyo kupunguza gharama.

Katika mwaka 2005/2006, kituo kilikuwa kimewaunganisha watoa huduma za *internet* 25. Aidha, matumizi ya *ICT* katika utoaji wa huduma za benki, yamepiga hatua. Karibu benki zote zina huduma za *Automatic Teller Machine (ATM),* ambazo zimerahisisha sana huduma za benki kwa mteja. Huduma za mabenki zimerahisishwa pia kwa kuunganisha mabenki mbalimbali na matawi yao na mawasiliano ya benki moja kwenda benki nyingine. Aidha, taasisi nyingi za elimu zinatumia mtandao kwa ajili ya huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Jamii Habari ni moja ya Mikakati ya Kimataifa iliyobuniwa kwa lengo la kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kwa kupambana na umaskini duniani na kupunguza tofauti za kiuchumi zitokanazo na kutokupata habari. Hivi sasa Serikali inaandaa Programu ya kuhamasisha na kuelimisha wananchi katika ngazi zote, kuhusu umuhimu wa matumizi ya *ICT* katika kufanikisha ujenzi wa Jamii Habari; kuhimiza uwekezaji na uendelezaji wa miundombinu muhimu, ikiwemo ile ya *ICT,* kwa kushirikiana na wadau wa nje na wa ndani ya nchi; kuandaa na kutekeleza mkakati wa kujenga uwezo wa wataalam wa fani ya *ICT* wa ngazi zote *(Human Capacity Building)* na kufanya mapitio ya sheria, taratibu na kanuni zote nchini ili kufanya marekebisho kwa lengo la kuwezesha matumizi ya *ICT* katika mchakato wa ujenzi wa Jamii Habari

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)*, imeendelea kutekeleza wajibu wake wa kuhakiki na kuratibu huduma za hali ya hewa nchini. Katika mwaka 2005/2006, Mamlaka iliweza kuanzisha huduma za hali ya hewa katika kiwanja kipya cha Ibadakuli – Shinyanga na kuweka vituo vinavyojiendesha vyenyewe Tabora na Kibondo na kujenga uwezo wa watumishi wake. Katika mwaka 2006/2007, Mamlaka ina mpango wa kununua rada ya kisasa ili kuboresha utoaji huduma zake.

Mheshimiwa Spika, Wizara inasimamia Baraza na Bodi mbalimbali zinazohusika na uratibu wa shughuli za kisekta kama vile uhandisi, ukandarasi, usimamizi wa vifaa, ubunifu wa majengo na ukadiriaji wa majenzi.

Mheshimiwa Spika, katika 2005/2006, Baraza lilikamilisha programu ya utekelezaji wa Sera ya Ujenzi, kukamilisha rasimu ya miongozo ya kiufundi ya namna ya kupata wabia*,* kusimamia miradi na kufanya Marekebisho ya Sheria Na. 20 ya mwaka 1979. Aidha, Baraza limetayarisha Mkataba Mdogo kuhusu kazi za ujenzi wa majengo (*Sub-contract Agreement for Building Works)* na kusimamia mradi wa ujenzi wa nyumba kwa kutumia mianzi, unaotekelezwa katika Wilaya ya Kyela na Rungwe Mkoani Mbeya. Katika mwaka 2006/2007, Baraza litaendelea na jitihada za kuhakikisha Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ujenzi *(Construction Industry Development Fund – CIDF)* unaanza kufanya kazi na kuendeleza maandalizi ya mazingira mazuri ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa njia ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Bodi ilikusanya shilingi bilioni 80.413, ikilinganishwa na shilingi bilioni 73 za mwaka 2004/2005. Aidha, Bodi ilifanya utafiti wa jinsi ya kupanua mapato ya Mfuko wa Barabara, kwa ajili ya matumizi endelevu ya barabara. Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Bodi inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 77,123.9 milioni ikiwa ni mapato yanayotokana na vyanzo vyake mbalimbali na kuzigawa kwa watekelezaji ambao ni Wakala wa Barabara *(TANROADS),* Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Wizara ya Miundombinu, pamoja na Bodi yenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Bodi iliweza kusajili wahandisi 533 na makampuni ya ushauri wa kihandisi yalisajiliwa 17. Aidha, Bodi ilikamilisha maandalizi ya utekelezaji wa utaratibu wa mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi wote, kutembelea mikoa 11 na kukagua shughuli za kihandisi, pamoja na maendeleo ya wahandisi wahitimu, wanaofanya mafunzo ya vitendo na kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo ya vitendo kwa wahandisi wahitimu 521, kwa lengo la kuwawezesha kupata uzoefu wa kutosha wa kufanya kazi za kihandisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Bodi ina lengo la kusajili wahandisi 620 na kampuni za ushauri wa kihandisi 20, kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo ya vitendo kwa wahandisi wahitimu wapatao 700, kuendelea kufanya kaguzi ya shughuli za kihandisi nchini ili hatimaye shughuli zote za kihandisi ziwe zinafanywa na wahandisi waliosajiliwa kwa kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Bodi ilisajili wataalamu 89 na kuwatahini wataalamu 1,838 wa ngazi mbalimbali. Aidha, Bodi iliendesha mafunzo endelevu *(Continued Professional Development),* kwa njia ya warsha, semina na makongamano, ambapo jumla ya warsha na semina tisa, ziliendeshwa kwa wataalamu wa ununuzi na ugavi kutoka Serikali Kuu, Mashirika ya Umma, Idara za Serikali na Asasi zake.

Malengo ya Bodi kwa mwaka 2006/2007 ni pamoja na kuendelea na usajili wa wataalam, kuboresha kiwango cha sifa za kujiunga na mafunzo, vyuo kuajiri waalimu wenye uwezo mkubwa na kuboresha mitaala, kupanua huduma za Bodi kwa kufungua vituo vya kuendeshea mafunzo au mitihani katika mikoa mingi zaidi badala ya kutegemea huduma zitolewazo sasa kwenye Mikoa ya Mbeya, Arusha, Mwanza, Singida, Mtwara, Tanga, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Visiwa vya Zanzibar na Pemba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Bodi ilisajili makandarasi wa ndani 721 na ukaguzi wa miradi 1,215. Pia Bodi iliendesha programu ya mafunzo endelevu kwa ajili ya kujenga uwezo wa makandarasi *(Sustainable Structured Training Programme – SSTP)* ambapo jumla ya kozi tisa ziliendeshwa. Aidha, Bodi iliendelea kusimamia Mfuko wa *Assistance Fund.* Mfuko huu unahudumia makandarasi wenye uwezo mdogo, ambapo makandarasi 376 kati ya 426 waliojiunga na Mfuko huu walifaidika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Bodi ina lengo la kukuza uwezo wa makandarasi wa ndani. Katika Mkakati huu, Makandarasi wataendelezwa kwa lengo la kufikia viwango vya Kimataifa ili kujengwa uwezo wa Taifa katika kutekeleza miradi mikubwa na hivyo kuwezesha makandarasi wenzao wadogo kupata miradi kwa njia ya *sub-contracts*. Bodi itaendelea kusajili, kuratibu na kutoa mafunzo kwa makandarasi wa nguvu kazi ili kuwezesha Watanzania wenye mtaji kidogo, kushiriki katika kazi za ujenzi, kutekeleza Mpango wa Bodi wa miaka 10, kwa kuiendeleza Bodi katika nyanja za utawala bora, kuboresha huduma na vitendea kazi na kuendeleza rasilimali zake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Bodi iliweza kusajili wataalamu 29, wataalamu wa sifa za kati sita na makampuni ya ushauri 12. Aidha, Bodi iliendeleza mpango wa mafunzo maalum ya vitendo, kwa ajili ya kuwasaidia wahitimu wa taaluma husika ili waweze kusajiliwa kwa mujibu wa sheria, ambapo walengwa 40 walijiunga na mafunzo haya; kutekeleza mpango kabambe *(Strategic Action Plan 2002-2006)* na kufanya ukaguzi katika mikoa mbalimbali, ambapo jumla ya sehemu za majenzi 285 zilikaguliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Bodi inatarajia kusajili wataalam 35 na wale wenye sifa za kati 75, kusajili kampuni za kitaalamu 15, kutahini wataalamu watarajiwa 81, kuendeleza mpango wa mafunzo maalum ya vitendo kwa ajili ya kuwasaidia wahitimu 60 wa taaluma husika ili waweze kusajiliwa kwa mujibu wa sheria, kuangalia upya mfumo wa mitihani na mfumo mzima wa usajili, kwa lengo la kuimarisha na kuwavutia wataalamu wengi zaidi kujisajili, kuendelea kutangaza shughuli za Bodi

kwa wadau kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma zitolewazo na Bodi na pia kuweka msingi wa kuimarisha utekelezaji wa Sheria Na. 16 ya 1997.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Miundombinu, ina vyuo vinavyotoa mafunzo yanayohusika na sekta hizi. Vyuo hivyo ni pamoja na:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Chuo kilifanikiwa kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka 452 ikilinganishwa ya wanafunzi 365 mwaka 2004/2005, ikiwa ni ongezeko la asilimia 23.8. Aidha, Chuo kimeendelea kufanya kazi za utafiti na uelekezi na kuanzisha Idara ya Taaluma Jumuisho, kutayarisha na kuhifadhi takwimu katika nyanja za usafirishaji na uchukuzi, kuandaa na kutengeneza upya programu na kuziwasilisha Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(National Council for Technical Education)* ili kupata ushirikiano kwa kubadilishana wataalamu na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo cha Ufundi *(DIT),* Chuo cha Mabaharia mweleko na matarajio ya mwaka 2006/2007. Wizara inakabiliwa na changamoto nyingi katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku, lakini juhudi zinafanywa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuweza kukabiliana na changamoto.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wizara ya Miundombinu, napenda kuwashukuru kwa dhati, wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha 2005/2006 katika kutimiza malengo yetu. Shukrani zetu pia ziwaendee wahisani mbalimbali, wanaotusaidia katika kutekeleza programu na mipango yetu ya Sekta za Ujenzi, Uchukuzi, Mawasiliano na Hali ya Hewa. Wahisani hao wanajumuisha Mashirika na Taasisi za Kimataifa, zinazochangia katika kuboresha utoaji huduma na miundombinu ya sekta zetu. Nchi na mashirika haya ni pamoja na Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri wa Majini *(IMO),* Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri wa Anga *(ICAO),* Shirika la Kimataifa linalosimamia masuala ya Simu *(ITU),* Jumuiya ya Kimataifa inayosimamia huduma za Posta *(UPU),* Shirika la Hali ya Hewa Duniani *(WMO),* Benki ya Dunia *(WB),* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB),* Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA), OPEC Fund*, Umoja wa Nchi za Ulaya, *Third World Organization for Women in Science (TWOWS), UNESCO* nchi za Urusi, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Uholanzi, Japan, India, Denmark na wengine wengi.

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu hazitakuwa kamili bila kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, pamoja na viongozi wenzangu katika Wizara ya Miundombinu, nikianzia na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Makongoro M. Mahanga, Katibu Mkuu, Eng. John Kijazi, Naibu Katibu Mkuu, Omari A. Chambo na watendaji wote wa Wizara, kwa juhudi walizofanya tulivyokabidhiwa na Taifa ipasavyo. Napenda pia kuwashukuru Viongozi na watumishi wa Mashirika yote yaliyo chini ya Wizara, kwa ushirikiano mzuri ambao wamekuwa wakinipa. Ushirikiano wao ndio ulioniwezesha kuandaa na kuifikisha hoja hii mbele ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara ya Miundombinu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka 2006/2007, naomba Bunge lako liidhinishe jumla ya shilingi 463,881,945,000.00, ambapo kati ya hizo, shilingi 319,801,948,000.00 ni za ndani na

shilingi 144,079,997,000.00 ni za nje. Fedha za ndani zinajumuisha: Fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 183,133,955,000.00 na Fedha za Maendeleo shililngi 136,667,993,000.00. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Bunge lako Tukufu, kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha hotuba yangu. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara *www.infrastructure.go.tz* .

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 88(11) ya Bunge, Toleo la 2004, naomba nichukue fursa hii, niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, taarifa ya Kamati ya Miundombinu, kuhusu makadirio na matumizi ya Wizara ya Miundombinu, Fungu Na.98 kwa mwaka wa fedha 2006/2007, pamoja na maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Kamati yangu ya Miundombinu, namshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema, uongozi madhubuti, jengo jipya la Ukumbi wa Bunge, ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Vyote hivi kwa pamoja, nina hakika vitatuwezesha kutimiza majukumu tuliyopewa na wananchi wetu kwa kasi na viwango vinavyoendana na wakati na kukidhi matakwa yanayotarajiwa.

Naomba nitumie nafasi hii, kuwashukuru wapiga kura wangu, wananchi wa Jimbo la Singida Kusini, kwa kunirudisha kwa mara ya pili katika Bunge hili Tukufu, nawashukuru sana. Naomba nitoe pongezi za dhati, kwa niaba ya Kamati yangu kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa, pamoja na wanachama wote waliopata nafasi mbalimbali za uongozi katika CCM.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha maoni yangu kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Miundombinu, napenda kutoa pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Nne, kwa hatua iliyochukua ya kuunganisha Wizara mbili zilizokuwa za Mawasiliano na Uchukuzi na Wizara ya Ujenzi na kuzaliwa kwa Wizara mpya ya Miundombinu, ambayo inaendeleza kutekeleza majukumu ya Wizara zote mbili zilizovunjwa. Hatua hii, itatoa fursa ya kuweza kutekeleza kwa kiwango kikubwa, Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu iliridhishwa na maandalizi na mawasilisho yaliyofanywa na Wizara ya Miundombinu kwenye Kamati, kuhusu mpango na makadirio ya bajeti ya mwaka 2006/2007. Kazi ambayo haikuwa rahisi, ikizingatiwa kuwa Wizara hii ni mpya na ilichelewa kuanza utekelezaji wa majukumu yake kwa takriban miezi minne wakati wakisubiri mchakato wa *restructuring* ukamilike. Wizara iliwasilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa mpango wa mwaka 2005/2006 na kazi zilizopangwa

kufanyika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007 na maombi ya fedha kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati yangu, napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Miundombinu; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari na Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ndugu John Kijazi, Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Omari Chambo, pamoja na watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya maandalizi ya mpango huu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii, kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati yangu imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Wizara katika kutekeleza maelekezo yote waliyopewa na Kamati yangu mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Miundombinu, aliainisha mafanikio na matatizo kwa kipindi cha mwaka 2005/2006, kama yanavyoonyeshwa katika ukurasa wa pili na wa tatu.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefarijika kuona kwamba, Wizara imejipangia kutekeleza mipango ya maendeleo, hususan ujenzi wa miundombinu, ikiwemo viwanja vya ndege, magati, vivuko, reli, bandari, pamoja na upembuzi yakinifu wa miradi mbalimbali juu ya sekta hizo. Hizi ni jitihada ambazo zitasaidia katika kujitegemea na kusukuma mbele maendeleo ya nchi kama sera zinavyotutaka. Kamati inaipongeza Wizara kwa jitihada zake hizo. Hata hivyo, Kamati inashauri Wizara iandae Mpango Mkakati, utakaozingatia kutekelezwa kwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na ahadi za Mheshimiwa Rais ili kupunguza maswali mengi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Ilani ni ya miaka mitano na ahadi za Mheshimiwa Rais ni za miaka mitano sio za mwaka mmoja, kwa hiyo, Wizara ikipanga mpango wake kila mtu akaelewa, nadhani matatizo na maswali yatapungua.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu pia inaitaka Serikali katika kutekeleza mipango yake ya maendeleo ya muda mfupi, kati na ya muda mrefu, kuhakikisha kuwa, miradi hiyo ya maendeleo inasambazwa nchi nzima na hasa katika maeneo yaliyoko nyuma kimaendeleo na kuepuka lawama zinazotolewa na Waheshimiwa Wabunge kuwa, Serikali inapendelea baadhi ya Mikoa au baadhi ya maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubinafsishaji wa mashirika ya umma, Kamati yangu inaunga mkono hatua zinazochukuliwa na Serikali za kutekeleza sera ya ubinafsishaji wa mashirika na taasisi za umma zilizoko chini ya Wizara hii, kwa kushirikiana na Kamisheni ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)*. Hata hivyo, Kamati inaendelea kutoa tahadhari ya kuitaka Serikali kuwa mwangalifu katika zoezi la ubinafsishaji ili maslahi ya Taifa yatangulizwe na yalindwe. Kamati inaishauri Serikali kuwa macho na makampuni ya kigeni yaliyokabidhiwa taasisi au mashirika ya umma wakati wa ubinafsishaji kwa kuhakikisha kuwa vigezo muhimu vya ubinafsishaji

vinazingatiwa. Vigezo hivyo ni pamoja na uwezo wa mwekezaji kuongeza mtaji, kuwa na teknolojia ya kisasa, ukuzaji wa ajira na kupanua huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imezingatia ufanisi mzuri wa Kitengo cha Kontena, pamoja na matatizo waliyoyakabili na ufanisi kupungua, kwa sababu ya udogo wa eneo la kuhifadhi makontena. Kamati imekubaliana na hatua zilizochukuliwa na Serikali za kulipatia ufumbuzi tatizo hilo. Kamati pia inashauri Serikali ipitie upya mkataba wa Kitengo cha Kontena ili malipo yanayolipwa Serikalini yaendane na ufanisi wa kitengo hicho.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa, uwepo uwazi na ushirikishwaji wa wadau kabla ya kuingia mikataba na wawekezaji na wakodishaji wa sekta mbalimbali zinazotoa huduma nchini. Mikataba ambayo baadaye ikikosa uwazi na ushirikishwaji, huonekana kuwa na mapungufu makubwa kiasi cha kuleta manung'uniko na hisia za rushwa kwa mfano, mikataba ya *TTCL, ATCL* na mingine.

Mheshimiwa Spika, pamoja na azma ya Serikali kupanua wigo wa kodi katika eneo la simu za mkononi, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa waangalifu katika azma hiyo ili wananchi wa kawaida waweze kumudu kutumia huduma hiyo, hasa wale wananchi wa vijijini, kama Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inavyoelekeza. Vile vile inataka makampuni ya simu za mkononi kuendelea kupunguza gharama za simu za mkononi hasa baada ya *TCRA* kuwezesha kupunguzwa kwa gharama za *interconnection fees* kutoka senti 17.5 za Kimarekani hadi senti nane.

Kamati pia inayapongeza makampuni ya simu za mkononi, kwa kazi nzuri za kusambaza huduma nchini. Kamati inashauri kuwa huduma hiyo isiishie mijini, bali isambazwe hadi vijijini ili kuweza kupata wateja wengi, jambo ambalo litasaidia kupata uwezo zaidi na hivyo kupunguza malipo ya simu za mkononi. Aidha, Kamati inasisitiza makampuni ya simu za mkononi, kuchangia minara ya simu, jambo ambalo litasaidia kupunguza gharama za uendeshaji na hivyo kupunguza malipo ya simu za mkononi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kuwa, kwa kuwa njia zote za usafirishaji ni muhimu kwa maendeleo ya nchi, ni vema Serikali ikawekeza na kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuimarisha na kuboresha viwanja vya ndege, njia za reli na bandari ili miradi inayokusudiwa ikamilike kwa wakati. Kwa mfano, reli ya Isaka hadi Kigali ni muhimu kwa ajili ya kuunganisha Tanzania na nchi za Magharibi, kama Rwanda na Burundi, pamoja na ujenzi wa reli ya Tanga hadi Musoma, ambayo itahitaji upanuzi wa Bandari ya Tanga na hasa ujenzi wa bandari mpya ya Mwambani.

Mheshimiwa Spika, wakati mchakato wa kukodisha Shirika la Reli Tanzania kwa mwekezaji unakamilishwa, Kamati inashauri kuwa, suala la mafao ya wafanyakazi wa Shirika hilo, liangaliwe na kuandaliwa kwa umakini ili kuepuka kero kama walizozipata waliokuwa wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Serikali iangalie uwezekano wa kubakiwa na hisa walau asilimia 49 ili kuwa na *fallow back position,* kukidhi haja endapo mwekezaji atasuasua.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali ya China, kwa kuendelea kuisaidia na kuiimarisha *TAZARA* kwa kuipa vichwa, injini na mabehewa. Hata hivyo, Serikali zote mbili za Tanzania na Zambia, nao wanatakiwa kuonyesha nia ya kuiimarisha reli hiyo, ambayo ni muhimu kwa uchumi wa nchi zote mbili. Ingefaa pia Serikali hizi kuanza kulipa madeni kwa China walau kidogo kidogo ili kuwatia moyo ndugu zetu hawa wanaotusaidia. Ni maoni ya Kamati kuwa, suala la ubinafsishaji wa *TAZARA* liwe ni hatua ya mwisho kabisa, endapo Serikali zote mbili zitashindwa kuwekeza katika reli hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la msongamano wa magari Mjini Dar es Salaam, Kamati inashauri Wizara kushirikiana na mamlaka zinazohusika, kuangalia namna ya kushughulikia suala hilo kwa haraka, kwani imekuwa ni kero kwa wakazi wa mji huo. Iwekwe mikakati ya makusudi, kuanzisha treni za mijini na kuweka *fly overs* katika Jiji ili kurahisisha usafiri.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inashauri utekelezaji wa ujenzi wa Daraja la Kigamboni, upewe kipaumbele kama ilivyoahidiwa katika Ilani ya Uchaguzi wa CCM mwaka 2005. Kamati yangu na Kamati ya Maendeleo ya Jamii, zimeketi kwa pamoja kujadili jambo hili na kuipa Serikali muda usiozidi miezi miwili, kulishughulikia jambo hili pamoja na wataalam wao ili kazi ya ujenzi wa daraja hili ianze mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imezingatia hali mbaya inayolikabili Shirika la Posta kutokana na madeni makubwa iliyorithi, ukosefu wa mtaji na malipo ya pensheni kwa wastaafu wake na kuishauri Serikali kuharakakisha maamuzi ya kulinusuru Shirika hili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *Air Tanzania Holding,* haijakamilisha majukumu ambayo ilikabidhiwa na kwa kuwa muda walioongezewa unaishia Desemba, 2006 na kwa kuwa Serikali imetaarifu kwamba, hivi karibuni itaanzisha shirika jipya la ndege baada ya kuvunjika kwa Mkataba wa Serikali na Shirika la Ndege la Afrika Kusini, Kamati inashauri kuwa ili kulinda mali ya Serikali isipotee na madeni ya sasa yatakayoachwa na *ATCL*, ni busara *ATHCO* waongezewe muda ili kumaliza majukumu waliyopewa awali na mengineyo yatakayotokana na kuvunjika kwa *ATCL.*

Kamati inaipongeza Serikali kwa kubadilisha sura ya uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kwa kufanana na hadhi ya Kimataifa, kwa kununua magari sita ya zima moto, kuimarisha vifaa vya ulinzi na usalama, kuboresha mapitio ya wasafiri na kuongeza sehemu za kuchukulia mizigo, kukamilika kwa mtandao wa umeme *(power distribution)*, barabara ya kutua na kurukia ndege, *(run way)* na maegesho ya magari. Pamoja na hatua hizo, Kamati inaishauri Serikali iiwezeshe Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, kwa kutenga fedha za kutosha ili miradi ambayo imeshindwa kukamilishwa kwa wakati sasa ikamilishwe.

Mheshimiwa Spika, Kamati vile vile inaishauri Serikali kutoa kipaumbele katika ujenzi wa viwanja vya ndege katika maeneo ambayo yana matatizo sugu ya usafiri na

yenye umuhimu katika kuinua uchumi wa pato la Taifa. Viwanja vya ndege vya Mwanza, Mafia, Singida, Kigoma, Dodoma, Musoma, Tabora na Shinyanga, vitengewe fedha za kutosha kwa mwaka ujao wa fedha kwa minajili ya kuifanyia matengenezo ya kuridhisha. Serikali iandae mpango wa muda mfupi, kati na muda mrefu, wa kuonyesha kifua mbele katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosisitiza hapo awali kuwa, Mafia wapewe kipaumbele katika ujenzi wa uwanja wa ndege, Kamati vile vile inaitaka Serikali iharakishe ujenzi wa magati ya Mafia na Nansio ili kuwaondolea kero ya usafiri wakazi wa maeneo ya visiwa hivyo, ambao kwa muda mrefu hawana usafiri wa kuaminika wa anga wala majini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huduma ya bandari ni ya muhimu sana katika uchumi wa Taifa letu na kwa kuwa huduma hii inategemea pia kuwepo kwa miundombinu mingine kama barabara, reli na viwanja vya ndege, Kamati inashauri nguvu inayotumika kuwekeza katika barabara itumike vile vile katika reli na bandari. Ili kuvutia nchi jirani kutumia bandari zetu kikamilifu, Serikali haina budi kuboresha bandari za Mtwara, Tanga, Kigoma, Mwanza na Itungi, ikiwa ni pamoja na matengenezo ya magati na vivuko, vipewe kipaumbele hasa baada ya kukamilika kwa ripoti ya *Ports Master Plan Study,* inayofadhiliwa na Benki ya Dunia. Hatua hiyo pia itasaidia kuwaondolea kero wananchi wanaotumia usafiri wa bandari na maziwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kununua, kujenga na kukarabati vivuko vya magati kama vile kivuko cha Musoma Kinesi, Sengerema, Pangani, Ukerewe, Kigongo Busisi na maeneo mengine. Hii itawapunguzia adha wananchi na kuleta nafuu ya usafiri pamoja na mizigo yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa sana na ajali zinazotokea mara kwa mara, zinazosababishwa na vyombo vibovu vya majini na nchi kavu. Kamati inaishauri *SUMATRA*, kujiwekea utaratibu mzuri wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa vyombo hivyo na vile vitakavyobainika kuwa na hitilafu, visiruhusiwe kutoa huduma. Aidha, kwa vyombo vitakavyosababisha ajali kwa uzembe, adhabu kali zitolewe kwa wahusika ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa leseni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mikakati na Serikali kushughulikia suala la *ATCL* na kwa kuwa tumetaarifiwa kuwa, Mkataba wa *ATCL* na Shirika la Ndege la Afrika Kusini utavunjwa, Kamati inashauri, Serikali iharakishe kuunda Shirika jipya la Ndege la Tanzania na liwezeshwe kwa kutengewa fedha za kutosha ili litoe huduma ya usafiri huo ndani na nje nchi.

Kamati inashauri Serikali kuwekeza na kuimarisha Wakala wa Ndege wa Serikali Tanzania *(TGFA),* kwani una uwezo mkubwa wa kuingia katika soko la biashara ya usafiri wa anga. Aidha, tunaishauri Serikali kuboresha maslahi ya wafanyakazi ya *TGFA* ili wataalam wazalendo waliosomeshwa na Serikali kwa fedha nyingi, wasishawishike kukimbilia mashirika mengine ya ndege yanayolipa vizuri.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, miradi ya barabara inayojulikana kama *special project*s, yaani Dodoma – Manyoni – Singida, Nangurukuru – Mbwenkulu - Mingoyo – Lindi, yote ipo nyuma ya wakati na kwamba, imechelewa zaidi ya mwaka mmoja na nusu, jambo ambalo litasababisha gharama za ziada na mzigo mkubwa kwa Serikali. Kufuatia hali hiyo, Serikali ifuatilie kwa karibu, wakandarasi wahusika ili waweze kukamilisha ujenzi wa barabara hizo mapema iwezekanavyo. Aidha, Kamati inashauri barabara ya Usagara – Geita, ianze kujengwa kwa kiwango cha lami katika mwaka huu wa fedha, kwa utaratibu wa *design and build.*

Mheshimiwa Spika, kwa vile barabara nyingi zinahitajika kujengwa na Serikali haina fedha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutangaza Mpango wa *Build Operate and Transfer (BOT)* na ule wa *Build Own Operate and Transfer (BOOT),* kwa uwazi zaidi baada ya kukamilisha kutunga sera husika.

Kamati bado inaendelea kushauri marekebisho ya Sera ya Ujenzi yafanywe ili ujenzi wa barabara za Halmashauri uachiwe *TANROADS*, kwa kuwa Halmashauri nyingi hazina fedha na wala wataalam wa kutosha na uzoefu umeonyesha kuwa, *TANROADS* wana uwezo wa kujenga barabara kwa viwango vinavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inayapongeza mashirika, taasisi, wakala na bodi mbalimbali, ambazo zimekuwa mstari wa mbele katika kuchangia maendeleo ya Wakandarasi, Wahandisi, Wabunifu Majengo, Maboharia Wazalendo na wengineo, ambao wamekuwa wakikumbana na vikwazo katika utekelezaji wa majukumu yao kutokana na sheria zilizounda vyombo hivyo, kutokana na nguvu au kupitwa na wakati hivyo, kutokidhi mahitaji yao. Kamati inaishauri Serikali, kupitia upya Sheria za *ERB, NBMM, CRB, AQSRB, TBA, TAMESA* na nyinginezo, ili kuleta mabadiliko halisi katika sekta hizi.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya barabara haina budi kuzingatia uchumi wa kijiografia ili kuvutia wawekezaji, pamoja na soko la usafirishaji. Ujenzi wa barabara uende sambamba na reli na bandari ili kufungua njia za uchumi. Kwa mfano, barabara ya Tunduma – Sumbawanga, Sumbawanga – Kasanga, Mpanda – Kanyani, Mwandiga – Manyovu, Kigoma – Nyakanazi, Kigoma – Tabora, Tabora – Nzega, Tabora – Itigi – Manyoni, Maganzo – Maswa – Bariadi, Namkula – Lamadi, Mtwara – Masasi – Songea – Mbababay, Mbeya – Chunya – Makongorosi – Itigi – Mkiwa. Kamati inasisitiza kwamba, uendelezwaji wa miundombinu uzingatie fursa tuliyonayo ya kuzungukwa na nchi jirani ambazo ni *landlocked,* zinazotegemea bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na uamuzi wa Serikali wa kusitisha zoezi la kuuza nyumba ambazo ni mali ya Serikali, badala yake Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kujenga nyumba kwa ajili ya wafanyakazi wa Serikali kwa mkopo utakaolipwa kidogo kidogo. Nyumba hizo zisijengwe kama makambi na tunashauri yajengwe maghorofa ili kuwezesha matumizi ya ardhi, pamoja na usambazaji rahisi wa huduma za jamii hususan maji, umeme, masoko, shule na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwawezesha Wakandarasi Wajenzi Wazalendo, kupewa kazi kwa upendeleo maalum, kwani wanahitaji kazi za gharama zisizopungua dola milioni 45 ili waweze kupata vifaa, mtaji na ujenzi wa kibiashara katika sekta ya ujenzi. Mpango huu utatoa fursa na kuwajengea uwezo Makandarasi Wazalendo katika ushindani ambao hivi sasa haupo. Kama ilivyobainika kwamba, asilimia tatu ya wakandarasi wageni, ndio wanaofanya asilimia 80 ya kazi zote nchini. Mpango huu unakidhi malengo yaliyobainishwa katika Sera ya MKUKUTA, Sera ya Ujenzi *(Construction Industrial Policy)*, Sera ya Uwezeshaji na Dira ya Taifa ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, Kamati inawapongeza Chama cha Wakandarasi Wajenzi Wazalendo, kwa kubuni Mikakati na Mipango ya kutoa mafunzo kwa wataalam wazalendo, mpango ambao utaanza na makandarasi 15 na baadaye idadi hiyo kuongezwa hadi 50 katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Hii itapunguza kwa kiasi kikubwa, kutegemea wataalam kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia na kujadili kwa kina, mawasilisho ya Wizara ya Miundombinu na baada ya kupitia kifungu kwa kifungu, Kamati yangu imeridhika na malengo, mipango na bajeti ya mwaka 2006/2007 na hatimaye Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu, lijadili na kukubali kupitisha kiasi kilichoombwa cha Sh.463,881,945,000, ambazo kati ya hizo Sh.319,801,948 zikiwa ni za Tanzania na Sh.144,079,997,000 ni za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii na kuwashukuru pia Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Manaibu wake, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari na Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Katibu Mkuu wa Miundombinu Eng. John Kijazi, Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Omar A. Chambo, pamoja na Wataalam wote wa Wizara ya Miundombinu na wale wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara hii. Ushirikiano wao pia umeiwezesha Kamati kutembelea Miradi ya Wizara, kwa namna moja ama nyingine, umesaidia Kamati kuandaa taarifa hii kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati yangu, Mheshimiwa Joyce Massunga, kwa ushauri na busara zake zilizoweza kunisaidia kuiongoza Kamati. Naomba pia niwashukuru kwa namna ya pekee, wanakamati wenzangu, kwa mchango wao mkubwa wa kupitia na kuchambua Mpango wa Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii, kwa umakini mkubwa na kwa uadilifu hivyo, kufanya kazi yangu kama Makamu wa Mwenyekiti, kuwa rahisi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati ya Miundombinu, kwa Mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 103B(1), Toleo la mwaka 2004 kama ifuatavyo: Mimi Mheshimiwa Mohammed Missanga ni Mwenyekiti, Mheshimiwa Joyce M. Masunga, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini,

Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Ephraim N. Madeje na Mheshimiwa Anne K. Malecela.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Balozi Getrude I. Mongella, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Sigifrid S. Ng'itu, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, Mheshimiwa Mwaka Abdrahaman Ramadhan, Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na Mheshimiwa Godfrey W. Zambi.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii tena, kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S. Foka, Katibu wa Kamati ya Miundombinu, Ndugu Justina M. Shauri na Katibu Msaidizi wa Kamati Ndugu Zainab A. Issa, kwa bidii na utendaji wao mzuri katika kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake. Nawashukuru pia wafanyakazi wote wa Ofisi yako, kwa ushirikiano katika hatua zote za maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kuwasilisha na ninaunga hoja mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, nilikuwa nimeletewa hoja ya utaratibu hapa kwamba, ikiwa wale waliovaa baraghashia nimewatoa, vipi anaruhusiwa aliyevaa kilemba cha Singasinga. Taarifa ni ifuatayo kwamba, katika Bunge lililopita maombi mawili mahususi ambayo hayamo katika Kanuni zetu, yaliruhusiwa kwa misingi ya imani, moja ni hicho kilemba cha Singasinga na pili ni *Hijab*, kama alivyovaa na kupendeza Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia pale, Waziri wa Utumishi. Haya mawili yaliruhusiwa na katika Rasimu tutakayoandaa ya Kanuni, tutajaribu kuzingatia ili mambo haya mapya yanayojitokeza, yaweze kuingia katika Kanuni, kwa hiyo, kilemba cha Singasinga, kimekubaliwa kwa mujibu wa imani, kwa sababu haruhusiwi kabisa kukivua na pia *Hijab* imeruhusiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Msemaji Mkuu wa Upinzani, karibu.

**BAKARI SHAMIS FAKI – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(b)(c) na 8141, Toleo la 2004, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Miundombinu ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuvuta pumzi hadi siku ya leo na kustahili kusimama hapa.

Nawapa shukrani nyingi sana wapiga kura wa Jimbo langu la Ole, kwa kunirejesha tena hapa Bungeni. Lakini pia namshukuru Kiongozi wa Upinzani Bungeni, kwa kuniona ninastahili na ninafaa kumsaidia katika nafasi hii ya Msemaji Mkuu wa Kambi yetu ya Upinzani katika eneo zito la uendeshaji wa Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, naunganana na Watanzania wengi, kutoa mkono wa rambirambi kufuatia vifo vya Watanzania wengi katika ajali mbili mbaya sana za barabarani, zilizotokea ndani ya wiki moja ya mwezi wa Juni mwaka huu wa 2006 katika mikoa ya Kagera na Arusha. Ajali hizo ni changamoto kwa Serikali na labda kwetu sote kama wapiga kura. Usimamizi duni wa Sheria za Usalama Barabarani ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa magari usio makini na kutokana na baadhi ya askari kutuhumiwa kuomba rushwa na vyombo vingine vya Serikali ni kati ya sababu zinazotufanya sasa tulie kwa uchungu, kuomboleza vifo vya wenzetu na tuongeze Jeshi la Vizuka, Wajane na Watoto Yatima.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niitumie fursa hii, kuwapongeza wote waliohusika na ukamilishaji wa jengo hili zuri la Bunge letu Tukufu. Ni bahati mbaya kwamba, halitafikika kirahisi na wananchi wengi kutokana hasa na masharti ya kiusalama. Juhudi zaidi zifanyike kulitofautisha jengo hili na *Strongroom* ya Benki, kwa manufaa ya Watanzania bila kuathiri mahitaji ya kiusalama.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (*TPA),* imeendelea kulalamikiwa kwa utendaji duni na hasa kucheleweshwa kwa upakuaji na upakiaji wa mizigo. Lipo tatizo sugu la wizi bandarini, hasa wa vifaa mbalimbali vya magari yanayoingizwa nchini na watu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kulalamika kwa kuzidiwa kete kibiashara na bandari za Mombasa kule Kenya, Durban - Afrika Kusini, Maputo na Beira kule Msumbiji, Mamlaka ikaze msuli, kuboresha huduma katika Bandari zake. Kinawachopeleka baadhi ya wafanyabiashara Afrika Kusini na Mombasa nchini Kenya ni ufanisi na ubora wa kiujumla wa huduma katika bandari za huko.

Mheshimiwa Spika, sote ni mashahidi kuwa ni hivi karibuni tu, tumevisikia vyombo ya kuaminika vya habari, vikiripoti sana kuhusu mishahara mipya ya *TPA*, lakini hapa la kuzingatia siyo tu suala la mishahara, bali ni kiasi gani *TPA* wanazalisha. Ni vyema mishahara ibaki kama ilivyo na isipunguzwe kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ili kuepusha migogoro ndani ya *TPA.* Maana inaaminika kwamba, mishahara minono haiko pale *TPA* tu, bali ni katika mashirika mengi hapa nchini. Funika kombe mwanaharamu apite ni suala la kamba hukatikia pabovu tu, la kukazania hapa ni *TPA* kuzalisha zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, ni muda sasa nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa *TPA*, inakaimiwa. Tunashauri nafasi hiyo sasa ijazwe. Taratibu na kanuni zizingatiwe vizuri kutekeleza jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Kontena Bandarini Dar es Salaam. Pamoja na sababu zilizotolewa na Serikali kuhusiana na kuongezwa kwa muda kwa wawekezaji wa *TICS* kutoka miaka 10 hadi 25, kinyemela, bado tunajiuliza hivi Serikali inakimbilia wapi? Hivi Serikali inakufa; si ipo tu ya nini kufanya haraka yote hiyo?

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali kwa mujibu wa Sheria Namba Tatu ya mwaka 1988, kifungu kidogo cha 10, kutupatia nyaraka na maelezo juu ya mwenendo mzima wa kuongeza muda *TICS,* kinyume cha Sheria ya Ununuzi ya mwaka 2004. Aidha, tunataka kujua *TPA* inapata kiasi gani kutokana na ukodishwaji wa Kitengo hicho.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Ndege la Tanzania *(ATCL),* tulipolibinafsisha tulitarajia kwamba, ubinafsishaji huu ungeweza kutuletea unafuu. Kama tulivyoeleza awali, tulitarajia kupata ndege zaidi lakini matokeo yake Makaburu wakachukua ndege kutoka kwao na kukodishwa kwa Kampuni yetu na siyo yao ya *South African Airways (SAA)*. Njia za ndani zimekufa na Ndege ya *DASH 8* zilikodishwa kutoka Afrika ya Kusini wakati tungeweza kukodisha yetu ya *Foka 28*. Leo *ATC* haiendi Tabora, Dodoma, Shinyanga wala Kigoma. Mfumo mzima wa tiketi upo Afrika Kusini, *code* inayotumika ya *0183* ambayo ipo katika tiketi za *ATC* ni yao na si ile yetu ya *0197.*

Mheshimiwa Spika, wananchi wanataka huduma bora na ya uhakika kutoka *ATCL* na wanataka shirika hilo lichangie kukua kwa uchumi wa Taifa na siyo kutangaza hasara na matatizo kila kukicha. Ubia kati ya Tanzania na Shirika la Ndege la Afrika Kusini, haukuwa ubia halisi bali ulikuwa ni ushindani kati ya Shirika la Ndege la Afrika Kusini *(SAA)* na *ATCL* pengine na kuhuisha *Precision* ambayo sasa inaongoza kuliko Shirika la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Ndege la Afrika Kusini, halikutekeleza ipasavyo majukumu yake kama walivyokubaliana kwenye Mkataba na hivyo kupelekea Serikali ya Tanzania ku-*inject* pesa kiasi cha shilingi milioni 500 kuliendesha shirika.

Mheshimiwa Spika, tumefarijika kusikia kwamba, Shirika la Ndege la Afrika Kusini, wamekubali kujitoa katika ubia huu, lakini wanayo madai kadhaa katika kufikia hatua hiyo. Kwa hiyo, tunamtaka Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho, atueleze kinagaubaga, madai yao ili nasi tupate kuyaelewa. Aidha, atueleze kiasi cha shilingi bilioni 15, ambazo Mheshimiwa Waziri wa Fedha, aliiarifu Kamati ya Fedha na Uchumi kuwa, zitatolewa na Serikali kwa *ATCL;* ni za kazi gani, ndiyo mpango wa uendeshaji unavyoagiza au ni kama vile tunavyotoa ruzuku kwa *TANESCO*?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri, wakati anapojumuisha, atueleze yafuatayo kuhusiana na ile Ndege iliyokuwa Afrika Kusini kwa matengenezo:-

(a) Ndege hiyo imekaa muda gani kule Afrika Kusini?

(b) Ni gharama kiasi gani iliyotumika katika matengenezo hayo kwa ujumla wake?

(c) Fedha za matengenezo amezitoa nani na kama ni sisi kwenye fungu lipi la matumizi?

Mheshimiwa Spika, pia ni vizuri Mheshimiwa Waziri, atueleze utakuwaje mustakabali wa *ATCL* baada ya kuvunjika ubia uliopo sasa?

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *SUMATRA,* inaonekana kusuasua katika suala zima la udhibiti wa usafiri wan nchi kavu na majini. Ongezeko la ajali za kizembe majini na hasa Ziwa Victoria, zinatokana sana na udhibiti usio makini. Pamoja na changamoto kubwa ya kupunguza ajali za kizembe barabarani, *SUMATRA* inatakiwa pia isaidiane na Taasisi nyingine kwa lengo la kumaliza au angalau kupunguza tatizo kubwa la msongamano wa magari katika barabara za Jiji la Dar es Salaam na pia sasa tatizo linaanza kujitokeza kule Mjini Arusha.

Mheshimiwa Spika, utolewaji wa leseni za udreva kiholela ni lazima udhibitiwe, kwa sababu unachangia sana ongezeko la ajali barabarani. Umefika wakati sasa wa kuongeza kiwango cha kujali uhai wa Watanzania, kwa kufanya juhudi za makusudi za uchunguzi na ukaguzi wa kina hasa katika vyombo vya usafiri wa majini. Tusipochukua hatua sasa, tutajikuta tunaomboleza kila juma katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ni hivi karibuni tu, kule Ziwa Victoria, imezama meli ya *MV Nyamageni.* Watanzania wengi walikufa na meli hii ilikuwa inalalamikiwa sana kwamba, haina sifa ya kubeba abiria. Lakini kutokana na kutokuwa na umakini wa vyombo husika, meli hiyo ilikuwa inafanya kazi bila kujali.

Mheshimiwa Spika, inaaminika kwamba, Nyamageni ilikosa kifaa kinachojulikana kama *Emergency Position Indicating Radio Beacon (EPIRB),* kinachoonyesha ni wapi chombo husika kimezama kama imetokea ajali. Kama *SUMATRA* ingefanya ukaguzi wa kina na kuona kasoro hiyo, basi *MV Nyamageni* isingeruhusiwa kufanya shughuli zake na Watanzania wale wasingefariki duni. *SUMATRA* fanyeni kazi kwa umakini, tuokoe roho za Watanzania, uwezo mnao.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo *(TBA),* Serikali iweke wazi Sera yake ya sasa kuhusiana na uuzwaji wa nyumba za Serikali. Zoezi hili limekumbwa na dosari nyingi, hakuna uwazi katika mchakato mzima wa uuzwaji wa nyumba *(TBA)*. Bado Watanzania wanahitaji sana nyumba bora na zenye angalau unafuu wa bei ili wazinunue kwa kulipia kidogo kidogo kwa miaka 10, 15 au hata 20.

Pia wananchi wamengependa *TBA* ijenge nyumba zaidi ili wazipange kwa bei nafuu. Ni jambo la kushangaza kwa mfano, mfanyabiashara wa kawaida au mfanyakazi wa kawaida, anapoambiwa na *TBA* hapa Dodoma kwamba, kupanga nyumba moja kwenye nyumba za *TBA* kule Kisasa ni shilingi 150,000 kwa mwezi. Hatuwezi tukawa na maisha bora kwa kila Mtanzania, kama wanavyodai wenzetu wa Chama Tawala, kwa kutumia mabilioni ya fedha za Watanzania, ambazo ni kodi wanazotozwa kwa namna mbalimbali, kujenga nyumba ambazo Mtanzania wa kawaida wala hawezi kuisogelea kutokana na bei yake na kodi ya pango. *TBA* na Serikali kwa ujumla, wanachochea mchuano wa kitabaka kati ya angalau walio ahueni kifedha na walala hoi wa nchi hii. Kuishi katika nyumba bora ni haki ya kila binadamu na kama lengo la *TBA* ni kuanza na wafanyakazi, basi *TBA* ibuni utaratibu utakaowafanya wafanyakazi wengi na wa kawaida

wapate nyumba kwa masharti nafuu na siyo Maofisa wa Serikali na wafanyabiashara wakubwa tu. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, Mamlaka ya Nyumba iwe mratibu wa mahitaji ya nyumba za Jeshi, Polisi na Vikosi vingine ili kama mradi unafanywa kwa pamoja, gharama zitakuwa ndogo. Aidha, teknolojia ya *prefab* nayo iingizwe nchini ili tuweze kujenga nyumba kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya 2005/2006, Serikali ililimbia Bunge kwamba, ilikuwa inakusudia kuanza utekelezaji wa mradi mkubwa unaojumuisha ununuzi wa mabehewa 66 ya abiria, ununuzi wa mataruma ya reli, ukarabati wa mabehewa 600 ya mizigo na ukarabati wa vichwa 20 vya treni. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, ilieleze Bunge lako, mafanikio ya utekelezaji huo na kama umekwama sababu ni zipi, kwani kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri, anasema kilichokuwa kimebaki ni utekelezaji tu?

Mheshimiwa Spika, mbali na ahadi hiyo pia kulikuwa na mpango wa utekelezaji wa utandazaji wa nyaya za mawasiliano ya simu *(Optic Fibres),* kupitia chini ya ardhi kati ya Dodoma na Tabora; je, kazi hiyo imefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, kati ya rasilimali na vitega uchumi vinavyomilikiwa na *TRC* ni mkongo wa njia za mawasiliano *(Fibre Optic Backbone).* Kambi ya Upinzani, inaomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, mkongo huo unalisaidia vipi Shirika hilo katika kuendesha shughuli zake au mpaka sasa umekwisha liingizia Shirika kiasi gain na ni maeneo gani ya nchi ambayo yanafaidika na mkongo huo?

Mheshimiwa Spika, Serikali ni lazima ichukue tahadhari na umakini katika kukodisha Shirika la Reli, kwa kutanguliza maslahi ya Taifa na Watanzania kwa ujumla. Wafanyakazi ni lazima wapewe haki zao, kama Mikataba inavyoeleza na wapewe mafao yao bila usumbufu. Aidha, Mikataba na mwajiri mpya ni lazima iwe ya hiari baada ya mfanyakazi kulipwa mafao yake kama sheria inavyosema.

Umuhimu wa Shirika la *TRC* kwa maendeleo ya kiuchumi kwa nchi yetu, unajulikana na hatuna haja ya kurudia, ila cha msingi ni huyu mwekezaji kutambua umuhimu wa Shirika hilo kwa maendeleo ya uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mtu akisema anakodisha shirika muhimu kama *TRC,* ni lazima tumjue ndani na nje. Hili ni jambo la uchumi wa nchi na maisha ya watu; je, mwekezaji huyu anao uwezo wa kuendeleza reli hiyo na kuwekeza katika teknolojia mpya?

Bunge hili ni sauti ya wananchi wa Tanzania na linayo haki ya msingi ya kujua kila kipengele kilichopo katika Mkataba wa ukodishwaji wa *TRC,* kati ya Serikali na Mwekezaji kutoka India. Kitendo chochote cha Serikali, kujitahidi kufanya Mkataba huu kuwa ni siri kubwa hata mbele ya wawakilishi wa wananchi, ni ukandamizaji wa Demokrasia ulio wazi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ianze na utaratibu wa

kuwashirikisha Wabunge, kwa kupitia Kamati husika za Bunge katika Mikataba ambayo tayari Serikali ilikwisharidhia lakini inaonekana ina makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuwekeza sasa hivi katika reli ya Isaka/Kigali kwa kiasi cha pesa kilichotengwa si kipaumbele, wakati tumeshindwa kuimarisha na kuboresha njia za reli tulizonazo. Tunafahamu umuhimu wa reli hiyo, kwa uchumi wa nchi yetu na ushirikiano mzuri wa majirani zetu, lakini hakuna mizigo ya kutosha katika Vituo vya Isaka na Mbeya kwa bidhaa za Rwanda na Malawi, kwani mizigo mingi inasafirishwa na barabara kutokana na kutokuwa na uhakika wa Shirika hilo. Hivyo, Kambi ya Upinzani inashauri fedha hizo zielekezwe katika kuboresha miundombinu yetu ya ndani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusuasua kwa utendaji kazi kwa Shirika letu la Reli ambalo ndilo lililokuwa likitumiwa na Watanzania wengi wanaoishi Mikoa ya Kati, Magharibi na Kanda ya Ziwa, kwa sasa wananchi wengi wanatumia usafiri wa mabasi. Wanaosafiri safari ndefu za mikoani, wanakutana na manyanyaso makubwa toka kwa wenye mabasi. Hii inatokea pale mabasi yanapojaza abiria kupita kiasi, inawalazimu kuwateremsha abiria pindi mabasi hayo yanapokaribia kwenye vituo vya mizani.

Mheshimiwa Spika, licha ya usumbufu wanaoupata abiria, pia Serikali inakosa kile kilicho halali yake. Hivyo, tunaiomba Serikali na vyombo vinavyohusika, vifanye kazi yake kama inavyotakiwa na viwe makini pale abiria wanapotoa malalamiko yao kuhusiana na adha hizo.

Mheshimiwa Spika, limejitokeza tatizo kubwa la mabasi kukiuka kanuni za viwango vya Shirika la Viwango Tanzania *(TBS),* hasa katika ubora wa Bodi, kwa maana ya kuzingatia usalama wa abiria kama ajali itatokea. Idadi ya abiria kwa ukubwa fulani wa gari, nalo ni jambo la muhimu ambalo limekuwa likikiukwa na wamiliki wa magari hiyo. Ni kwa nini gari lililoidhinishwa na vyombo au mamlaka husika kubeba abira 62, libebe abiria 142 kama ilivyoripotiwa na vyombo vya habari na liendelee kufanya safari zake kama vile nchi haina Serikali?

Mheshimiwa Spika, miradi mingi ya ujenzi wa barabara haikamiliki kwa wakati na inaongeza mno gharama kwa wakandarasi na hata Serikali kutokana na wizi wa mafuta unaofanywa na wafanyakazi. Pamoja na juhudi za makampuni hayo ya ujenzi wa barabara kudhibiti wizi wa mafuta, upo umuhimu mkubwa kwa mkono wa dola kutumika kuwasaidia wakandarasi hao. Wezi hao ni maadui wa maendeleo ya Taifa kama walivyo wezi wa mafuta wa transfoma za *TANESCO.* Ni hakika Jeshi la Polisi, linao uwezo wa kuwadhibiti kwa manufaa ya Watanzania. Suala la barabara sasa limekuwa sugu sana hapa nchini kila Mkoa, kila Wilaya na kila Jimbo, kilio kikubwa ni ukosefu wa barabara ama zinazounganisha Mkoa na Mkoa au Wilaya na Wilaya na tatizo hili limejitokeza hasa katika Mikoa ya Kusini, Magharibi na ile ya Ziwa. Barabara nyingi zimejengwa chini ya viwango. Hili limeipelekea Serikali kupoteza fedha nyingi mno, kwani imejikuta kila baada ya miaka miwili, inatenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizo. Mfano wa barabara hizo ni Mbeya – Chunya – Makongolosi, Mbalizi – Mkwajuni, Kyela – Ipinda, Mlowo – Kamsamba – Mbozi na kadhalika. Barabara zote hizo na nyingine nyingi, zimekuwa zikitengenezwa chini ya kiwango kiasi kwamba, wakati wa mvua aidha, hazipitiki kabisa au zinapitika kwa shida.

Mheshimiwa Spika, tunashauri barabara hizi zijengwe kwa kokoto, ambapo kwa Mbeya kokoto zipo za kutosha pale *Kongoro Query.*

Mheshimiwa Spika, imefika wakati sasa Serikali ipange vizuri kwani kupanga ni kuchagua, kwa hiyo, kupunguza madai ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu miundombinu katika majimbo yao, kwa ukuaji wa miingiliano ya kibiashara baina ya Wilaya na Wilaya kwa maendeleo ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, iandae mpango utakaoonyesha jinsi tatizo hili la *networking* za barabara litakavyomalizika. Ujenzi wa barabara nyingi nchini, bado unaoongozwa na falsafa ya kiukoloni mamboleo, ambapo barabara hujengwa kwa nia ya kufanikisha malengo ya ubepari wa Kimataifa na hasa kuhamasisha uzalishaji na usafirishaji wa mazao ghafi ya kilimo na pia madini.

Mtandao wa barabara unaopigiwa debe na kushabikiwa na wafadhili ni uleule wa wakoloni wa kuangalia kwanza ni wapi na kunazalisha nini na uchumi wa kiukoloni mamboleo utafaidi vipi. Kinachofikiriwa kwanza ni kupatikana kwa faida kibao, yaani *super profit,* kwa manufaa ya awamu mpya na ya kisasa ya ubepari iitwayo utandawazi na maslahi ya kijamii husukumizwa pembeni kimakusudi.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la wazi la ubabaishaji katika taaluma nzima ya ubunifu wa majengo hapa nchini, kuporomoka ovyo kwa majengo na nyufa nyingi hata katika majengo ya Serikali yenye umri mdogo tu, ni dalili tosha za ubabaishaji huo. Kama si kwamba, taaluma hiyo imevamiwa na wataalam feki, basi lipo tatizo la rushwa ambapo watu wababaishaji hufumbiwa macho na Bodi inayohusika. Ni lazima Bodi ya Wabunifu Majengo izaliwe upya, kama Bodi yenyewe haiwezi kujipanga upya, basi ipangwe upya na Serikali. Maisha ya Watanzania yasichezewe kamari na wazembe wachache ndani ya bodi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna ubishi kwamba, juhudi za makusudi za kuwawezesha makandarasi wazalendo zinahitajika sana. Hakuna nchi inayoweza kupata maendeleo kiuchumi na kijamii kwa kutumia wageni badala ya wananchi wake. Wakati kimsingi naunga mkono juhudi za kampeni za Chama cha Makandarasi wa Ujenzi Tanzania*,* kuhusu umuhimu wa kuwaendeleza makandarasi wazalendo, naamini bado lipo tatizo sugu miongoni mwa wakandarasi wazalendo wa kufanya kazi kimzaha na kwa kulipua badala ya kufanya kazi kiushindani na kwa kuzingatia ubora wa hali ya juu, uhakika, uaminifu na uharaka. Sina nia ya kusema kuwa hakuna makandarasi wa kigeni wababaishaji na hata wabangaizaji, lakini inakera mno pale mwananchi anapokuwa yeye ndiye mvunja nchi namba moja. Uzalendo usiwe ndiyo kisingizio cha kufanya kazi kiholela. Uholela huo hutumika kama mwanya ambao huwapa sababu watoa maamuzi kuwapa makandarasi wenye sifa za Kimataifa na kuwaengua makandarasi wazalendo.

Mheshimiwa Spika, ukiondoa kile kinachoitwa miji mikubwa au mikoa mizito, hali ya viwanja vya ndege katika maeneo mengi ya Tanzania ni mbaya sana au ni sawa na hakuna kitu kabisa. Maendeleo ya kimiundombinu ikiwa ni pamoja na viwanja vya

ndege, yaelekezwe kwa Watanzania wote. Mtazamo wa kikoloni na hata kikoloni mamboleo wa eti kuteua maeneo yanayodaiwa kuwa na faida za kiuchumi, haustahili kuendekezwa wala kudekezwa, Watanzania wote wanataka maendeleo ya kisasa na ni lazima vigezo vya kugawa rasilimali ya Kitaifa viangaliwe upya.

Maendeleo siyo Mbeya, Kilimanjaro, Arusha na Dar es Salaam tu, ila ni pamoja na Tandahimba, Pemba, Simanjiro, Namanyere, Sumbawanga, Singida, Mafia na kadhalika. Matatizo haya ya kuchagua baadhi ya mikoa kuendelezwa viwanja vyake, ndiyo imepelekea hata ndege ya mabilioni ya shilingi ya Mheshimiwa Rais, kutokuwa na uwezo wa kutua katika mikoa yote. Hii inaleta hisia tofauti miongomi mwa Watanzania, ambao walilazimishwa kujibana ili kununua ndege hiyo. Kila mkoa una haki ya kuwa na kiwanja kizuri cha ndege.

Mheshimiwa Spika, kusudio la ujenzi wa Bandari ya Mwambani Tanga, ni jema hasa katika suala zima la kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii Mkoani Tanga. Pamoja na kusudio hilo jema, tunayo matatizo makubwa ya ubora wa teknolojia, kimenejimenti na kiuwezo, siyo tu katika Bandari ya Tanga, Mtwara, Mwanza, Kigoma, Bukoba na hata Dar es Salaam. Napenda kuishauri Serikali, iendeshe kwanza zoezi la uzalishaji na uboreshi wa bandari hizo, ambazo kimsingi zimo katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, imewahi kusikika kwa siku za nyuma kwamba, Serikali ilikuwa na mpango wa kuanzisha usafiri wa boti kati ya *City Centre* na maeneo kama Tegeta na Boko, pia kumewahi kufikiriwa kuanzishwa usafiri maalum wa treni ya mjini kutoka stesheni katikati ya Jiji la Dar es Salaam kwenda Buguruni, Tabata na Ubungo kwa upande mmoja na maeneo ya Vingunguti, Kiwalani, Ukonga, Segerea na Pugu kwa upande mwingine. Usafiri huo wa treni za mjini na boti ilionekana na wakazi wengi wa Jiji la Dar es Salaam kuwa ni ukombozi mkubwa kwa matatizo makubwa yaliyopo Jijini.

Tunaishauri Serikali, iangalie tena uwezekano wa boti na treni kutumika kupunguza kero sugu ya usafiri Jijini Dar es Salaam. Ifike mahali mipango iwe ni vitendo. Tuvuke majukumu ya udhibiti. Ni lazima sasa tuwe wabunifu, vinginevyo muda si mrefu usafiri wa Jijini Dar es Salaam, utashindikana kabisa. Dar es Salaam inahitaji barabara za chini ya ardhi, kupunguza kabisa msongamano na kulifanya Jiji letu kuwa la kisasa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa habari za kutia moyo za Serikali kununua kivuko kipya na cha kisasa katika kivuko cha Magogoni, bado ipo kero ya usalama wa wananchi kuwa majaribuni kutokana na kuharibika kwa mara kwa mara kwa vivuko vilivyopo, yaani *MV Kigamboni* na *MV Alina*. Sina uhakika kama kivuko kinachoitwa *Mv Usiwe Kupe,* bado kipo kazini au kimestaafishwa. Uninuzi wa kivuko kipya uende sambamba na ukarabati mkubwa wa vivuko vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, wakati wananchi wa Misungwi na Sengerema, wanasubiri kupatiwa kivuko kipya badala ya kile kilichopo sasa, ipo haja ya kivuko cha Kigongo

Busisi kufanyiwa matengenezo ya haraka sana. Ile tabia ya kuzimika moto mara kwa mara huenda ikaligharimu Taifa hili kwa kupoteza uhai wa raia walio wengi. *(Makofi)*

Ni vema sana wakati wa kusafiri katika vivuko kutenganisha bidhaa za mafuta, hasa petroli, abiria na vyakula. Ili kuepusha kutokea majanga. Pia Serikali iwakemee sana waendesha vivuko hivyo, waondokane na uzembe. Mfano kama ule uliotokea katika kivuko cha Pangani, wahusika waliposahau kuweka mafuta katika engine za kivuko hicho na ikabidi wanyonye mafuta kutoka kwenye basi la Tawfiq, ambalo lilikuwepo humo na kuweka kwenye *engine* za kivuko hicho, kama ilivyoripotiwa na vyombo vya habari. Kama isingetokea ndani ya kivuko hicho kuwepo kwa hilo basi, matazamio ni kutokea patashika shika, nguo tatua, ndani ya kivuko hicho. Tujihadhari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mtandao wa Barabara ya Kikoloni - Mambole. Ujenzi wa barabara nyingi nchini bado unaongozwa na falsafa ya kiukoloni-mamboleo, ambapo barabara hujengwa kwa nia ya kufanikisha malengo ya ubepari wa Kimataifa na hasa kuhamasisha uzalishaji na usafirishaji wa mazao ghafi ya kilimo na pia madini. Mtandao wa barabara unaopigiwa debe na kushabikiwa na wafadhili ni ule ule wa wakoloni wa kuangalia kwanza ni wapi, kunazalishwa nini na uchumi wa kiukoloni-mamboleo utafaidi vipi. Kinachofikiriwa kwanza ni upatikanaji wa faida kibao *(super profit),* kwa manufaa ya awamu mpya na ya kisasa ya ubeberu iitwayo "utandawazi" na maslahi ya kijamii husukumizwa pembezoni *(marginalization),* makusudi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta liko hoi bin taaban, linajiendesha kwa hasara kwa sababu lilianzishwa bila kupatiwa mtaji na wakati huohuo limebebeshwa mzigo mzito wa madeni, pamoja na jukumu la kuwalipa mafao wastaafu waliokuwa wa *East African Post*.

Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Mahesabu ya Serikali ya tarehe 25 Juni, 2005 inaonyesha kuwa, Shirika hilo linadaiwa kiasi cha shilingi bilioni 16.5 na dola za Kimarekani milioni 1.5, kati ya hizo shirika linaitaka Serikali ilipe kwa niaba yake, shilingi bilioni 13.9 na dola milioni 1.06 na deni lililobakia lifutwe.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uweli kwamba wafanyakazi wa mashirika mengi ya umma, ambayo yameuzwa, watumishi wamepata shida sana kupata mafao yao kutoka kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii, kwa mujibu wa sheria.

Hivyo basi, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba, madeni inayodaiwa na Shirika hilo, yalipwe na wafanyakazi wawe na uhakika wa kulipwa stahili zao. Shirika linahitaji kunusuriwa, maana limekuwa *specified* kwa muda, sasa haliwezi kufanya biashara maana haliwezi kukopesheka. Ipo haja ya Serikali kulitupia jicho la rehema Shirika hili, vinginevyo litakata roho muda si mrefu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali yake dhaifu, Shirika linashauriwa lifanye jitihada kubwa katika usafirishaji wa vifurushi Mikoani na Wilayani, kwani hili

limezorota kwa kiasi fulani. Pia wafanye utafiti ni kwa sababu gani wateja wanakimbilia *DHL* kusafirisha mizigo yao. Shirika pia lijizatiti vizuri sana ili waweze kukabiliana na ushindani unaowakabili, ambao wao Shirika la Posta, wameuita *unfair competition*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, *ATHCO* imegundua malipo yapatayo kiasi cha shilingi 1,274,612,847, ambayo hayakuhamishwa katika chombo chochote, ipo haja ya kuendelea kufanya utafiti zaidi kwa mali ambayo bado haijagunduliwa.

Mheshimiwa Spika, nyumba zinazokadiriwa kufikia nne, ambazo ziko Dar es Salaam, *Toure Drive,* ambazo zilihamishiwa na kumilikiwa na Serikali, zingeliliingizia shirika *(ATHCO)*, hela nyingi kama zingelimilikiwa na kuuzwa na shirika hilo. Kuna tuhuma kwamba, nyumba hizo zilipelekwa Serikalini kutoka *ATHCO* lili wakubwa wapate kuzinunua kwa bei poa.

Mheshimiwa Spika, kuna wasiwasi kwamba, wapo watu wajanja, ambao wanachukua fursa hii ya muda mfupi wa *ATHCO,* ili waweze kufungua kesi za madai na kujipatia mali kwa urahisi kabisa. Yako madeni kadhaa yanacheza na muda, mfano, deni la kiasi cha shilingi milioni 400, kule Moron - Komoro.

Mheshimiwa Spika, inatuhumiwa kwamba, kuna watu wanavuruga kumbukumbu za mali za iliyokuwa *ATC* ili *ATHCO* ikimaliza muda wake wapate kuhodhi mali hizo. Kwa hiyo, Serikali inashauriwa kuwa macho na hilo na kufanya utaratibu wa kuzitafuta na kuziweka vizuri kumbukumbu zote za mali za iliyokuwa *ATC* kwenda *ATHCO.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *ATHCO* haiwezi kuyalipa madeni yake, Serikali ni lazima ifanye juhudi ya kuipatia fedha ili iweze kulipa madeni yake. *ATHCO* ni mtoto wa Serikali kinyume na *ATCL,* ambaye ni shirika binafsi na bado Serikali inatoa hela nyingi kuliendesha.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa ni Mamlaka muhimu sana katika kutoa huduma kwa wananchi, hasa katika kilimo, usafiri wa anga na majini na katika ujenzi na kadhalika. Mamlaka kwa kushirikiana na Serikali, inashauriwa ipeleke utabiri wa hali ya mvua na ukame kwenye Halmashauri ili wakulima wajue wafanye nini kwa wakati gani. Kwa kuwa Mamlaka haina fedha za kukidhi mahitaji yake, ni vyema Serikali iipatie mamlaka fedha ili itimize malengo yake, ambayo pamoja na mengine, ni kutoa huduma muhimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sana Serikali iwapatie *TMA,* rada ambayo inakadiriwa kufikia kiasi cha shilingi bilioni 1.5. Kwa kupatiwa kifaa hiki, Mamlaka itaweza kufanya kazi zake kwa uhakika na kwa ufanisi mkubwa, unaoendana na wakati huu wa Teknolojia ya Karne ya 21.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya simu za mkononi isichukuliwe kama ni jambo la anasa, bali ni hatua muhimu katika kuleta maendeleo ya nchi. Kulikuwepo na

malalamiko mengi juu ya wananchi wa kipato cha chini, kutomudu ughali, sio tu wa bei za simu zenyewe bali hata muda wa maongezi. Tumefadhaishwa sana leo hii kusikia kwenye bajeti kwamba, ushuru wa huduma za mawasiliano umeongezwa kutoka asilimia tano hadi asilimia saba. Hii maana yake ni kuongeza kiwango cha umaskini kwa Watanzania hasa wale wenye kipato cha chini. *(Makofi)*

Serikali katika kuongeza ushuru, imesema ni karibu kiwango cha asilimia kumi kinachotozwa katika nchi za Afrika Mashariki. Lakini Serikali haijaeleza, je, uchumi wa Tanzania unakaribiana na wa Uganda na Kenya; je, *exchange rates* za nchi hizi za Afrika Mashariki zinakaribiana na ja ongezeko la thamani kati ya nchi hizo na sisi zinalingana?

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote, bado tunaitaka Serikali izingatie sana suala hili la kuongeza ushuru katika huduma za simu za mkononi, kwani litawaumiza sana wananchi walio wengi nchini. Kwa hiyo basi, kama haitowezekana kupunguza hadi angalau kufikia asilimia tatu au nne, basi ibakie ile ile asilimia tano. Maana kidonda kitaendelea kuuma lakini si kama kukiwekea msumari wa moto.

Mheshimiwa Spika, zipo taarifa za miundombinu muhimu ya Kitaifa ikiwa ni pamoja na madaraja muhimu kuhujumiwa mara kwa mara. Serikali iandae ulinzi shirikishi wa rasilimali za Kitaifa katika sekta ya miundombinu. Askari wa Jeshi la Polisi, wawezeshwe na washirikishwe ili waongeze zoezi la ulinzi wa kimkakati wa madaraja, reli, taa za barabarani na kukomeshwa kwa uzidishaji wa mizigo inayozidi uzito stahili kwa barabara zetu kuu.

Mheshimiwa Spika, kila mwaka wa bajeti, Serikali imekuwa ikiahidi juu ya miradi ya *BOT*, lakini sasa ni miaka kumi bado hatujaona hata utaratibu rasmi wa mwekezaji aliye tayari kuwekeza, kuelezwa juu ya utaratibu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikaweka bayana utaratibu wenyewe, maana haujaeleweka na walio wengi nchini. Pia iwekwe bayana ni maeneo na miradi gani ambayo Serikali iko tayari kuwaruhusu wawekezaji kuwekeza kwa utaratibu wa *BOT*.

Mheshimiwa Spika, barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na kadhalika, ni miundombinu muhimu kwa ufanisi wa uchumi wa kisasa katika Taifa lolote. Uwekezaji zaidi na Menejimenti bora ya miundombinu ni kati ya mambo yanayoweza kulipeleka mbele Taifa letu kiuchumi. Kwa hiyo, Serikali ijitahidi sana katika kuimarisha miundombinu muhimu kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Msemaji Mkuu wa Upinzani kwenye Sekta ya Miundombinu, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na kuwaita wachangiaji, kuna mambo mawili ya ufafanuzi wa utaratibu, ambayo lazima niyaseme kwa sababu ninapoulizwa kuhusu utaratibu hata kama ninaandikiwa, ni muhimu nifafanue ili anayehusika au wanaohusika, wasione kwamba, labda tunaenda kinyume.

Baada ya yote haya, tunaendelea kuhusu mavazi. Kuna Mheshimiwa Mbunge, hapa ameandika kuhusu vazi alilovaa Naibu Waziri wa Maendeleo Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian. Kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wabunge wasiomfahamu, Mheshimiwa Dr. Batilda Buriani ni mwanamke wa Kiislam. Kwa tafsiri ile ile ya *Hijab* na Meza haijapewa *Hijab* muweje kuziona hapa, hazilingani. Kwa hiyo, kwa mwanamke wa Kiislam, kufunika nywele zake kwa namna yoyote ile, itatambuliwa na Spika kwamba, ni jambo halali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Ijumaa wiki iliyopita, wakati tunaendelea na Kamati ya Matumizi, nilitoa matangazo kuhusu mpira uliokuwa unaendelea Ujerumani. Kuna Mbunge ameni-*challenge* kwamba, napata wapi mimi madaraka ya kuingilia na kusema mambo kama hayo. Kanuni ya 54 inasema hivi: "Spika, aweza kulihutubia Bunge wakati wowote na kwa ajili hiyo, aweza kumkatiza Mbunge yeyote hata anayezungumza." Nashukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa ninao wachangiaji 39, anayetangulia ni Mheshimiwa George Malima Lubeleje, halafu atafuatiwa na Meshimiwa Lucas Selelii. Wakati huo huo ajiandae Mheshimiwa Eustace Katagira na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, kwa mpangilio huo. Kwa hiyo, tutaanza na Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri. Niwapongeze Waheshimiwa Manaibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii na wataalam wote. Najua wanafanya kazi nzuri, lakini katika mazingira magumu ya ufinyu wa bajeti, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru wananchi wa Jimbo la Mpwapwa, kwa kunirudisha tena Bungeni na mimi ninawaahidi kwamba, nitakuwa nao wakati wote katika kuleta maendeleo katika Jimbo langu la Mpwapwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kuhusu barabara za Kitaifa *(Trunk Roads).* Hivi sasa kuna miradi mikubwa ya barabara, kuna barabara ya kutoka Dodoma kwenda Manyoni, ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami, wananchi mpaka sasa hawaelewi kwa nini mradi ule unachelewa. Halafu kuna barabara ya kutoka Manyoni kwenda Singida, miradi hiyo imecheleweshwa sana. Mheshimiwa Waziri, atupe maelezo katika Bunge hili, kwa nini miradi hiyo inachelewa? Tatizo inawezekan ni mkandarasi, lakini mkandarasi anapoteuliwa, lazima awe na uwezo. Kama Mkandarasi hana uwezo, kwa nini anateuliwa kutengeneza barabara hizo?

Kwa hiyo, hili nataka nipate maelezo. Lazima tuwe na *time frame* ni lini kazi hiyo itakamilika. Kwa sababu ipo miradi mingi katika nchi hii, Mikoa ya Kusini wanalalamika, Mikoa ya Kanda ya Kati, Tabora, Mwanza kwa watani zangu kule, wote

wanalalamika. Kwa hiyo, naomba miradi hii inapoanza kutekelezwa, ikamilike mapema ili wananchi waweze kupata huduma. Barabara ndiyo maendeleo na barabara ndiyo uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie barabara za Mji wa Dodoma. Mheshimiwa Waziri, naomba leo mchana hebu upite tu ukague hizo barabara zetu. Hivi sasa *greda* linapita linatengeneza barabara na wanaweka changarawe, ambayo ni vumbi. Tunachohitaji wananchi wa Mji wa Dodoma ni barabara za lami na wala siyo barabara za changarawe. Dodoma ni Makao Makuu ya Nchi hii, Dodoma ina heshima zake na Dodoma tunapata wageni wa Kimataifa. Ninawaomba sana, Mheshimiwa Waziri na Manaibu Mawaziri, hebu wajaribu kuzunguka waangalie hizo barabara. Haiwezekani barabara ya Manispaa, *greda* linapita katikati ya Mji, linatimua vumbi maana yake nini? Najua mipango ipo, lakini hiyo mipango itatekelezwa lini? Sasa suala la kutupiana mpira, *CDA* itatengeneza, sijui Manispaa, naomba migogoro hii ya Manispaa na *CDA* muiangalie, tunataka barabara zitengenezwe.

Mheshimiwa Spika, nije barabara za Mikoa. Napenda nimpongeze sana Meneja wetu wa *TANROAD* wa Mkoa wa Dodoma na wasaidizi wake, wanafanya kazi nzuri san, lakini kama nilivyosema, mazingira ni magumu sana. Nashukuru wameshatengeneza barabara ya kutoka Mbande kwenda Kongwa - Mpwapwa – Mlali, lakini kiwango cha matengenezo ni kidogo sana. Kwa sababu fedha zinazotengwa ni kidogo. Kwa hiyo, tunachoomba ni kwamba, waongezewe fedha. Kwa sababu kile kiwango cha matengenezo ya barabara hiyo ni changarawe, ni kutengeneza na *greda* tu, lakini tunahitaji matengenezo makubwa. Hiyo barabara ilikuwa na mpango wa kuwekwa kwenye msamaha wa madeni na kwamba, hiyo barabara ingetengenezwa, lakini hiyo barabara imetengenezwa kuanzia Mbande mwisho Kongwa. Hata kile kipande cha Mbande – Kongwa, mkandarasi hakuitengeneza vizuri hiyo barabara. Hivi sasa lile eneo limeharibika sana, magari yanapopita inakuwa ni shida kubwa, hasa magari madogo. Kwa hiyo, naomba barabara hii ya kutoka Mbande – Kongwa – Mpwapwa – Lupeta kwenda Matomondo mpaka Mlali – Pandambili, itengewe fedha za kutosha kwa ajili ya matengenezo makubwa siyo matengenezo ya kutumia *greda,* inaleta makorongo.

Kazi yetu sisi Wabunge ni kuishauri Serikali siyo kuiagiza, lakini wakati fulani kama Serikali haisikilizi maombi ya Wabunge tunaiagiza Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara za Wilaya, tatizo ni kwamba, fedha zinazotengwa kwenye Mfuko wa Barabara ni kidogo sana, asilimia 30 kwa asilimia 70. Kwa sababu Mfuko wa Barabara, Wizara inabaki na asilimia 70 na Halmashauri za Wilaya asilimia 30. Fedha hizo hazitoshi na tumeshazungumza na tumeiomba Serikali kwamba, *formular* ingebadilishwa angalau iwe asilimia 50 kwa 50, ingesaidia sana. Huko Vijijini ndipo watu wengi na ndiko tunategemea kupata mazao, usafirishaji wa mazao na abiria. Lakini hizi barabara za Wilaya kama zitaendelea kupata asilimia 30, nina hakika hatutengenezi barabara kwa kiwango kinachotakiwa. Tunaishauri Serikali iongeze hiyo asilimia iwe asilimia 40 au 50 ili tuweze kupata fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie barabara ya kutoka Gulwe – Berege - Mima kwenda mpaka Fufu na Sebuka. Barabara kweli ni ya Wilaya, lakini Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, inatengewa kwa mwaka shilingi milioni 20 au milioni 30, haziwezi kutengeneza barabara, ni kutengeneza barabara kwa *greda* tu, lakini haziwezi kutengeneza madaraja. Ni lazima Halmashauri zipewe fedha za kutosha ili ziweze kutengeneza barabara hizo. Tuna barabara nyingi katika Wilaya ya Mpwapwa, ambazo zinapitika kwa shida sana.

Barabara za Tarafa ya Rudi, barabara za Tarafa ya Kibakwe, unakwenda mpaka Malolo, barabara zinapitika kwa shida sana. Hivi sasa tunaishukuru Serikali, inajenga Daraja la Kitara, Kitara ni kati ya Kibakwe na Rudi. Hili daraja lilishavunjika miaka mingi iliyopita, Serikali imetenga fedha, fedha zilizotengwa ni kidogo. Tunataka daraja lile likamilike ili wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa waweze kusafirisha mazao yao na vilevile abiria wanapata shida ya usafiri, wanatembea kwa miguu kwenda katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye makampuni ya simu za mkononi. Mpwapwa tayari kuna minara imejengwa kwa ajili ya simu za mkononi za *Celtel,* lakini bado tunaiomba Serikali, kwa sababu mawasiliano ni muhimu sana katika maendeleo yetu, *TTCL* wameshindwa kusambaza simu vijijini. Sasa nadhani ikijengwa minara mingi vijijini, itasaidia mawasiliano kwa wananchi wetu. Wameshajenga mnara pale Mpwawa, kati ya Lukole na Msanze, lakini tunahitaji Kata ya Matomondo wajenge mnara, halafu Mima na Chunyu wajenge mnara. Hii itasaidia mawasiliano katika Wilaya nzima mpaka Mkanana kule milimani, kule Pwanga hivi sasa wanakamilisha mnara. Mawasiliano yatasaidia sana katika Wilaya yetu ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na wataalam wake, lakini Wizara hii ni muhimu, lazima ipewe fedha za kutosha. Wizara haiwezi kutengeneza barabara, fedha zinazotengwa ni kidogo sana, haiwezekani hata kidogo. Bila barabara katika nchi hii, hakuna maendeleo. Dunia nzima huwezi kupata maendeleo kama huna mawasiliano ya barabara, haiwezekani hata siku moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru tena na nikupongeze wewe binafsi, kwa jinsi unavyoendesha vikao vyetu. Nimpongeze Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wetu, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Job Ndugai. Niwapongeze Wenyeviti wenzangu wa Kamati, jinsi wanavyowasilisha taarifa zao hapa. Nimpongeze Mheshimiwa Mohamed Missanga, jinsi alivyowasilisha taarifa ya Kamati yake. Lengo letu ni kushirikiana na Serikali na kwa yale ambayo yanashindikana, niko tayari kuishauri Serikali, ndiyo kazi yetu sisi Wabunge kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tunachoomba ni kwamba, ushauri wa Wabunge ni vizuri uwe unazingatiwa na Serikali. Sisi hapa tunatumwa na wapiga kura, uchaguzi umeshapita, sasa kilichobaki ni kufanya kazi za maendeleo. Serikali hii ya Awamu ya Nne, imeanza vizuri sana. Nampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, anafanya kazi nzuri sana, pamoja na Baraza la Mawaziri, wameanza vizuri na wanafanya kazi nzuri. Ninampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi hii ili niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. Baada ya kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, kwa kwa kweli imenichanganya, nimechanganyikiwa na nadhani wakati atakapokuwa anahitimisha hoja yake, nitafurahi sana kama atatoa ufafanuzi wa kutosha hasa katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, napenda tu kutahadharisha kwamba, mimi natoka Kanda ya Magharibi na katika hilo, sioni aibu wala sisiti kutetea Kanda ya Magharibi, hasa kwa upande huu wa miundombinu. Kwa sababu nimeona katika kitabu chake na nimemsikiliza wakati anawasilisha taarifa, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, nilikuwa nasoma vitabu ambavyo vipo hapo nashindwa kuelewa. Hivi azma ya Serikali ni nini hasa katika Kanda ya Magharibi na maeneo ya Ziwa Victoria?

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza juu ya kuondoa umaskini, tunapozungumza kuleta maendeleo, tunapozungumza kukuza uchumi, kama hatuzungumzii barabara nzuri, reli nzuri, viwanja vya ndege vizuri, bado hatujafanya chochote. Katika kusoma majalada na kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nitaeleza kwa nini nimechanganyikiwa hasa katika maeneo ya Kanda ya Magharibi na eneo la Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, barabara ni kiungo muhimu sana kwa usafiri wa aina yoyote utakaoutumia, ukisafiri kwa ndege, lazima utashuka kwenye ndege utaanza kutumia barabara, ukisafiri baharini, utashuka utaanza kutumia barabara na ukisafiri kwenye barabara kuu, lazima utaingia kwenye barabara za mitaa au barabara za vijijini. Kwa hiyo, barabara ni kitu cha kwanza kabisa katika nyenzo ya kukuza uchumi. Kwa hiyo, katika mawazo yangu ambayo nilikuwa natarajia kuyapata na mwanzoni pale nilipokuwa namsikiliza Mheshimiwa Waziri, nilitegemea kabisa barabara ambazo atakuwa anazitaja, zitakuwa zimejielekeza na kujikita zaidi katika kuchochea na kuibua hali ya uchumi ambayo tunatarajia kufikia hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, nilijua kabisa ataeleza kwa makini, namna ambavyo Serikali ya Awamu ya Nne, imejiandaa kuhakikisha barabara ya kutoka Itigi – Tabora – Kigoma inajengwa kwa kiwango cha lami. Nilitegemea kwa uhakika kabisa, atajielekeza namna gani barabara ya kutoka Nzega – Tabora – Ipole mpaka Mbeya itajengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kinyume cha matarajio, ndiyo maana nasema mimi nimechanganyika. Kinyume cha matarajio, nimesoma hata katika vitabu hivi ambavyo vinaonyesha fedha, barabara zote muhimu za Kanda ya Magharibi zote hazimo. Ukizungumzia barabara ya kwenda Mpanda, ukizungumzia barabara ya kwenda Kigoma,

ukizungumzia barabara ya kwenda Mbeya na ukizungumzia barabara ya kwenda potepote Magharibi hazimo.

Mheshimiwa Spika, barabara zilizopo kwa kweli hapa uzalendo umenishinda, chukua barabara ya kutoka Manyovu kwenda Mwandinga, kule kwa ndugu zetu wa Kigoma, imepangiwa kwenye vitabu vya fedha shilingi bilioni mbili. Ukichukua barabara ya kutoka Ipole kwenda Mpanda, imepangiwa shilingi milioni 600, ukichukua barabara ya kutoka Nzega kwenda Tabora, imepangiwa shilingi milioni 500, ukichukua barabara ya kutoka Sumbawanga kwenda Nyakanazi shilingi milioni 500. Kuna barabara moja, juzi jamaa zangu wale wa Mwanza walilalamika sana mpaka wakawa wanaandika kwenye magazeti, tumewapangia fedha, hazimo humu kwenye kitabu cha hotuba, hakuna na hata kwenye kitabu cha fedha, ile barabara ya Usagara kama sijasokea sana, hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini iko barabara ya kutoka Marangu - Tarekea imepangiwa shilingi bilioni 17. Jamani hivi nchi hii hii moja, barabara moja tu, tena barabara ile ni kama vile kutoka Urambo unakwenda Kaliua, inapangiwa shilingi bilioni 17. Barabara nyingine shilingi milioni 500, nyingine shilingi milioni 300 na nyingine *zero;* maana yake nini? Hapo ndipo nimenichanganyiwa, kweli uzalendo umeshinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeiomba Wizara hebu tutende haki, tunaelewa kabisa vipaumbele mnavyo vingi, tunaelewa kabisa sungura ni huyo huyo mdogo, hilo tunalijua, lakini tutende haki twende angalau kikanda. Unapozungumzia Kanda utataja Magharibi, unapozungumzia Kanda utataja Kanda ya Ziwa, unapozungumzia Kanda utataja Kanda ya Kusini ya wakulima wa korosho, ndiyo kanda hizo. Lakini unapozungumzia kutoka Tarekea kwenda Marangu, hivi jamani hiyo ndiyo haki?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hapo hatutendi haki, lazima tuseme ili hata vizazi vijavyo vije viseme kwamba, sisi tulisema, lakini hapo hatujatenda haki. Ndiyo maana nimesema hilo la kwanza nimechanganyikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa Magharibi huu tukiuibua, mimi siku zote nimekuwa nikisema, sisi Watanzania tutaendelea kulia lia, tutaendelea kuomba omba, tutaendelea kunung'unika, tutaendelea kulaumu Kenya kwa sababu bado hatujaamua kuibua Kanda nyingine mpya za uchumi. Tujenge barabara za kibiashara, tujenge barabara zenye faida na tujenge barabara za kuibua biashara mpya. Hapo Magharibi nchi yetu inapakana na nchi nyingi ambazo hazina bandari, Mungu atupe nini. Ametupa nchi tatu, ukiweka hata Uganda inakuwa ya nne, hazina bandari. Lakini tunazidi kulalamika, kuwalalamikia Kenya wanatuzidi kete, kwa sababu wao wamewekeza kwenye kuibua uchumi. Lakini sisi pale ambapo tunatakiwa tuweke uchumi hatuweki, barabara zile tungeweza kuibua uchumi kwa kutumia nchi ya Kongo *DRC,* tungeweza kuibua uchumi kwa kutumia nchi ya Rwanda, tungeweza kuibua uchumi kwa kutumia nchi ya Burundi na ikiwezekana na Uganda na ingewezakana Mwanza, ingekuwa ni *harbour* ya Kanda ya Magharibi na hususan na Kigoma hasa kwenye Bandari kama ya Manyovu. Lakini hatuyaoni hayo jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nilikuwa na hamu ya kunywa chai, lakini nimeshindwa kabisa, kwa jinsi ambavyo hatujatendewa haki Kanda ya Magharibi na Kanda ya Ziwa Victoria. Kwa hiyo, hapa nitaomba Mheshimiwa Waziri, mimi ni Mbunge mzoefu, tutapambana kwenye vifungu na naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mniunge mkono. Mpaka atuambie vizuri ni kwa namna gani Kanda ya Magharibi, anaitendea haki hasa katika hili la kwanza la barabara na Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, sikuweza kuona bayana ni namna gani Mkataba ambao unaendelea sasa hivi wa Shirika la Reli na Serikali, unapozungumzia Reli kwa Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi, hapo ndipo mkombozi wao. Lakini naogopa na inaashiria kwamba, hii inaweza kuja kutokezea kama ilivyokuja kutokezea Mkataba wa Serikali na Shirika la Ndege.

Mheshimiwa Spika, tulikuwepo humu humu, Waheshimiwa Wabunge tulishauri, tulisema kwamba, Mkataba mnaoingia na Shirika la Ndege la Afrika Kusini hauna maslahi kwa Taifa, tulisema hapa hapa Bungeni. Leo kwa kweli bado tutaendelea kusema na kwa Shirika la Reli, Waziri hajaeleza ni kwa namna gani Shirika la Reli na Serikali, wamekubaliana kuboresha huduma. Kwa sababu reli ndiyo imekuwa mkombozi kwa muda mrefu sana Kanda ya Magharibi na Kanda ya Ziwa, inasafirisha mizigo na abiria wanasafiri kwa kutumia hiyo reli. Sasa inasemekana Shirika la Reli limepata mwekezaji kutoka India wa kuja kukodisha treni. Reli inabaki mali ya Tanzania. Sina uhakika kwa sababu hakufafanua vizuri ni kwa namna gani itabaki mali ya Tanzania na tunafanyaje. Hivyo ilivyo reli kwa sasa ni reli ambayo imeshafikia kikomo, ina miaka 100 iliyopita. Lakini la pili, inabeba ratili 50 tu, wakati wenzetu wanakwenda kwenye ratili 100 na wanakwenda kwenye ratili 90. Sasa bado tuna ratili 50, hebu tuingie mahali ambapo tutazungumzia biashara. Hebu tufike mahali ambapo tutazungumzia maslahi ya Taifa, hebu tufike mahali ambapo tutalenga mbele.

Mheshimiwa Spika, nilitarajia katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri, angesema kwamba, kwa Shirika la Reli tumeingia ubia na watu wa India sawa, lakini ningetarajia kusema wazi kabisa; je na Serikali yenyewe imo? Kinachokuja kutuhangaisha katika Mikataba mingi Serikali inajitoa, huwezi ukajitoa kwenye mambo ya huduma, huwezi ukaachia asilimia mia moja kwa mia moja kwenye mambo ya huduma. Ndiyo hayo mambo yanakuja kutuhangaisha hata kwenye migodi, tumejitoa kwa kila kitu, tumewaachia wanachukua wanavyotaka. Treni kama tutawaachia wafanye wanavyotaka, watakuja kutusumbua siku nyingine watasema hatuendi Mwanza na hatuendi Kigoma. Unapoacha kwenda Mwanza na Kigoma, unaweka athiri kubwa sana ya kisiasa hata ya kiuchumi kwa Kanda ya Magharibi na kwa Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili la pili, nalo limenichanganya, naomba maelezo mazuri ya kwamba, je, huyu mwekezaji anachukua asilimia ngapi na Serikali inabaki na asilimia ngapi? Lakini, la pili, upo mkakati gani wa kuitengeneza reli iweze kufikia kiwango cha kisasa, baadae tuanze kufikia treni za umeme, kwani Kanda ya Magharibi kuna ubaya gani mkituletea treni za umeme tutashindwa kupanda?

Tuanze mkakati wa kutengeneza treni za umeme. Unasafiri kutoka Tabora kwa dakika 30, hata watani zangu hawa wagogo, wanaopenda kwenda kufanya kazi Dar es Salaam, kwa muda wa nusu saa watakuwa wamefika Dar es Salaam, halafu baada ya kazi wanarudi Dodoma. Ndiyo unazungumza maendeleo, lakini hajasema chochote kama ana mpango wa maendeleo katika treni na kuweka maendeleo katika reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, kabla kengele haijanigongea ni *Air Tanzania* na kwa kweli hata kengele ikigonga, sijaunga mkono hoja, nitamke wazi moja kwa moja. Shirika la Ndege ni lazima kama unataka kuimarisha Sekta ya Utalii, Shirika la Ndege na Utalii ni ndugu, hatuwezi kupanua utalii kama hatuna Shirika la Ndege, hatuwezi kuzungumzia tunainua utalii kama Shirika letu la Ndege ni hohehahe. *Air Tanzania* tumeiuza, matokeo yake sisi Tanzania sasa hivi tunabaki tuko katika kilio.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ningependekeza na ningedhani Waziri angetuambia bayana, kwa muda gani muafaka Serikali imeweka ili tuwe na *National Career?* Bwana Mipango aseme kabisa kwamba, ni lini Serikali imeweka tuwe na *National Career?* Ni lini ile Kodi yetu ya *Air Tanzania* inarudi ili tuanze kuimarisha Shirika la Ndege na ndipo tutaimarisha utalii? Tutaendelea kulalamika, kuwalalamikia Wakenya kwa sababu sasa hivi huwezi ukajilinganisha na *Kenya Airways*. Angalia hata kwenye vyombo vya Kimataifa vya nje *Kenya Airways* ana-*appea*r kwenye *CNN,* ana-*appear* mpaka kwenye *BBC.*

Sasa sisi tumeng'ang'ania kulalamika tu wakati bahati mbaya sana Serengeti na Ngorongoro, Kilimanjaro, vyote viko katika maeneo ambayo hata Kenya anaweza akayafikia bila ya kufika Tanzania. Hawezi kuja mtaalii yeyote kama hana uhakika wa usafiri. Kwa hiyo, katika hili, ningetaka Waziri aseme ni lini tunalifufua Shirika letu la Ndege, tuwe na *National Career*, *Air Tanzania* yenye maslahi kwa Taifa letu. *Air Tanzania* yenye maslahi ya kibiashara hasa katika sekta ya kiuchumi na hasa ukizingatia utalii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa kweli bado nimechanganyikiwa, naomba tukutane kwenye vifungu na naomba Waheshimiwa Wabunge, waniunge mkono.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. EUSTACE D. KATAGIRA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja hii.

Awali ya yote, napenda kuishukuru Serikali hususan Wizara ya Afya, kulitokea mlipuko wa Malaria kule Mkoani Kagera hususan Wilaya ya Karagwe, lakini habari nilizonazo ni kwamba, Serikali imechukua hatua za haraka na Mheshimiwa Waziri, amefika mwenyewe Hospitali ya Nyakahanga pale Wilayani Karagwe. Walikwenda mpaka katika *Health Centre* ya Nkwenda, ambayo ipo katika jimbo langu na amejionea mwenyewe na hatua zinachukuliwa za kusaidia janga hili la mlipuko wa Malaria. Kwa hiyo naishukuru sana Serikali, kweli hii ni kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kushauri kwamba, *cyrcle* ya Malaria katika maeneo yale inajulikana, kila mara baada ya mvua nyingi huwa inajitokeza kitu cha namna hii. Malaria inakuwa kali na kweli inakuja kwa wingi na kila mara inakuwa ni vizuri maandalizi yafanywe ili mlipuko ukitokea, uweze kushughulikiwa kwa haraka haraka.

Mheshimiwa Spika, pia tumefarijika kuona kwamba, Serikali imeshaweka matangazo ya tenda ya kukarabati barabara za Mkoa wa Kagera, hususan pia barabara za Wilaya ya Karagwe. Barabara ya kutoka Kyaka kwenda Bugene mpaka Benako katika mradi huu wa ukarabati lakini pia barabara ya kutoka Bugene kwenda Kaisho mpaka Murongo. Nashukuru hatua hiyo, lakini ningependa nitoe maelekezo kidogo au msaada kidogo kwamba, katika ukarabati wa barabara ya kutoka Bugene kwenda Kaisho mpaka Murongo, kuna sehemu mbili ambazo ni korofi sana. Kwa hiyo, wakati wa kukubaliana na mkandarasi aelekezwe kabisa kwamba, katika barabara ya Bugene kwenda Kaisho Murongo ile sehemu ya kati ya Nkwenda na Lukulaijo ni sehemu ambapo barabara inavuka dimbwi kubwa na kila mara barabara huwa inafunikwa na maji.

Kwa hiyo, aelekezwe afanye kazi nzuri pale katika sehemu ile korofi, aweze kunyanyua barabara kidogo na itasaidia wakati wa mvua barabara iweze kuendelea kupitika. Lakini pia katika sehemu ya Mlima wa Rwabunuka katika barabara hiyo ni muhimu katika ukarabati huu, mkandarasi aelekezwe aweze kuweka changarawe za kutosha, ili changarawe zisiishe baadaye ikawa ni utelezi na ule ni mlima mbaya. Lakini pia maji ya mvua yameshaanza kula sehemu ya barabara hiyo, kwenye Mlima huo mkali, ili afanye marekebisho ili barabara isiendelee kuliwa na maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, nitoe kilio cha Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, kuhusiana na barabara za Wilaya hiyo. Kuna barabara moja inatoka Kayanga inapita Rwambaizi, inapitia Kigarama, Businde mpaka Murongo, ikielekea nchi jirani ya Uganda. Barabara hii ina kilomita 124. Barabara hii ni ndefu mno kwa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe kuendelea kuikarabati na kuitunza. Tunapendekeza na wananchi wanaomba hii barabara ichukuliwe iwe barabara ya Mkoa ili *resources* za Halmashauri ya Wilaya Karagwe, ziweze kutumika kusaidia katika barabara nyingine ambazo ni fupi na zinaunganisha vijiji.

Lakini pia barabara hii ni muhimu sana kwa sababu, inaiunganisha Tanzania na nchi jirani ya Uganda. Kwa hiyo, inasaidia sana biashara, *movemen*t ya wananchi kutoka Uganda kuja Tanzania, kutoka Tanzania kwenda Uganda na ni muhimu ikatunzwa vizuri. Kama ilivyo kwa urefu huu, kuna wakati Halmashauri imechukua miaka minne bila ya kuikarabati hata kidogo na barabara imekuwa haipitiki. Hii ni barabara ambayo inasaidia pia wananchi waende Hospitali ya Wilaya kutibiwa. Kwa hiyo, ni muhimu barabara hii kweli iwe ni *reclassified* na iingie katika uangalizi wa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, zipo pia barabara nyingine za namna ile. Tuna barabara ya Kigarama, Mabira mpaka sehemu ya Kyerwa, inaitwa Rwenkorongo. Hii barabara ina urefu wa kilomita 51.8 na hii barabara kama nilivyotaja kwanza, barabara hii ni mzigo

kwa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe. Ni muhimu barabara pia iunganishwe na barabara niliyoitaja kutoka Kayanga kwenda Murongo, ili mzigo huu ubebwe na mkoa ili ziweze kutengenezwa kila mara ili Halmashauri ya Wilaya iweze kuwa na nguvu sasa ya kuweza kuhudumia barabara nyingine za kusaidia wakulima na wakazi wa vijijini. Lakini pia niunganishe barabara ya tatu, barabara ya Mabira mpaka Nkwenda. Hii ni barabara ndefu ya kilomita 32. Lakini si urefu tu, barabara hizi zina matatizo makubwa kwa sababu mandhari ya Karagwe hususan jimbo la Kyerwa, si mandhari ambayo ni nyoofu, ni mandhari yenye milima na mito. Kwa hiyo, unakuta utengenezaji wa barabara hata kama sio ndefu sana, kweli ile ya kwanza niliyoitaja ya kilomita 124, ni barabara ndefu sana.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hii ya kilomita 32 ni barabara inayopanda milima, inateremka kwenye vijito, inakuwa ni kazi kubwa, mzigo mkubwa kwa Halmashauri. Mwisho wa yote, unakuta barabara moja inakula fedha nyingi na barabara za kuunganisha vijiji na vijiji, Kata na Kata, inakuwa fedha hazipo za kuweza kuzihudumia hizo barabara ambazo zingehudumiwa vizuri na Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe. Tunaomba sana kwamba, hizi barabara ziwe *reclassified,* ziondoe mzigo kwenye Mfuko wa Halmashauri ndipo pia barabara zile fupi fupi za kilomita 7, 12, au 21, zinazounganisha vijiji zitaweza kupata huduma nzuri na zikatengenezwa zikawa zinapitika wakati wote. Tufahamu maeneo ninayoyataja ya barabara hizi ni maeneo ya uzalishaji mkubwa wa kahawa, maharage na mahindi, ambayo inasaidia si Karagwe peke yake vinakuja mpaka Bukoba, Mwanza hata mpaka Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu Tanzania, kwa miaka karibu 10 iliyopita, tulipiga kelele ikaleta huduma katika jimbo la Kyerwa hususan, sehemu ya Kaishonalsingiro. Lakini baada ya kutoa huduma hiyo kwa wananchi wachache, Shirika hatujaliona tena kusambaza huduma hizo. Tunaomba Shirika hilo sasa lijihimu, lijitahidi kusambaza hizi huduma kwa wananchi wengi zaidi ili nao wafaidike na *services* za Shirika hilo. Lakini hapo hapo, naomba nitoe shukrani za pekee kwa Mashirika ya Simu za Mkononi, ambayo sasa yameshaanza mkakati wa kuleta huduma katika Wilaya ya Karagwe hususan jimbo la Kyerwa. Shirika la *VODACOM* limeshakuja, Shirika la *CELTEL* limeshakuja na Shirika la *TIGO.* Hawa wameonyesha nia, wameshaanza mikakati ya kuweka huduma katika maeneo ya Nkwenda, Kamuli, Kaisho na Isingilo. Isipokuwa tungeomba sasa, kuna eneo moja liko mpakani na Uganda, eneo la Murongo, tungeomba Mashirika haya yaliangalie pia eneo hili ili na eneo hilo lije liwe katika mkumbo wao wa kutoa huduma katika maeneo haya.

Naomba niongelee barabara ya Kyaka kwenda Kayanga. Barabara hii imeongelewa sana na ni barabara inayotoka katika mpaka karibu na Uganda kuja mpaka mji wa Wilaya ya Karagwe. Tungeomba pamoja na kuwa imetangazwa katika matengenezo yatakayo tengenezwa ya ukarabati wa barabara za Wilaya ya Karagwe, naomba pia niongeze na mwenzangu kama alivyoongea Mbunge wa jimbo la Wilaya ya Karagwe kwamba, wananchi wanaomba hii barabara itengenezwe kwa kiwango cha lami, ili iweze kuunganisha mkoa pale Kyaka pamoja na mji wa Wilaya ya Karagwe.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kidogo Uwanja wa Ndege wa Bukoba. Wabunge wengi wa Kagera wameliongelea, tunaomba kabisa na tunaisii Serikali itusaidie huo Uwanja utengenezwe vizuri ili *runaway* yake iwekwe lami na ndege ziweze kutua na kuondoka wakati wote, iwe ni mvua na jua, ili isiwe kwamba ukifika Mwanza unaanza tena kufikiria kama Bukoba mvua inanyesha au mvua hainyeshi. Imekuwa inabidi wakati mwingine, watu watoke hapa badala ya kwenda Mwanza na kwenda Bukoba wapande ndege ya kutoka hapa kwenda Entebbe, watoke Entebbe na gari ili tuweze kwenda katika nchi yetu Tanzania kule Bukoba na Karagwe. Kwa hiyo, tunaomba pamoja na yote pamoja na ukosefu wa fedha lakini angalau *runway* peke yake itengenezwe ili ndege ziondoke na kutua, mvua inyeshe au jua liwake.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na nasema naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia asubuhi hii. Awali ya yote, niipongeze hotuba ya Waziri wa Miundombinu, ambayo kwa kiasi Fulani, inaleta matumaini kwa maendeleo ya wananchi wetu katika majimbo yetu.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Nianze na kivuko cha Pangani. Wizara ya Miundombinu, nafahamu wana uhakika kwamba, kivuko cha Pangani kina hali mbaya sana. Nishukuru ziara ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Mama Maua Daftari, kuja Pangani na kushuhudia yeye mwenyewe hali halisi ya kivuko kile na amekiri kwamba, kivuko cha Pangani kina hali mbaya. Kuna baadhi ya maelekezo alitoa kwa watendaji pale wa kivuko cha Pangani, ambayo yatekelezwe. Sasa sielewi ni tatizo la ufinyu wa fedha, lakini yalikuwa ni maelekezo muhimu kwa ajili ya kuokoa maisha ya wananchi wa Pangani, wasipate majanga kutokana na hali halisi ya kivuko kile. Kivuko kile hakifai hata kwa kutengenezwa upya *(is beyond repair)*.

Vile vile naishukuru Serikali kwa taarifa nilizokuwa nazo ni kwamba, tenda imetangazwa, mzabuni amepatikana wa kununua kivuko kipya na wananchi wa jimbo la Pangani, wanalielewa hilo, isipokuwa muda sasa unapita kutokana na hali halisi ya kivuko cha Pangani kilivyo, hatuna uhakika Mungu apishie mbali ni wakati gani janga linaweza likatokea. Sasa naiomba Serikali labda ituarifu hivi mnategemea kivuko hiki ni lini kitafika Pangani ili tuwe na matumaini ya kwamba, tunajivutavuta huku tukisubiri kivuko kipya cha Pangani. Vile vile namshukuru Mheshimiwa Rais, alipokuja Mkoa wa Tanga kutoa shukrani kwa wananchi wa Mkoa wa Tanga. Alisema wazi kwamba, kama Serikali na yeye kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ilikuwa ni moja ya ahadi katika Ilani ya Uchaguzi kwamba, Serikali kazi yake imekwisha, isipokuwa sasa anamwachia Mbunge wa Pangani, afuatilie kivuko cha Pangani. Nataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Pangani wanasubiri kivuko kipya kitafika lini? Ni vyema ukaawaarifu ili tuwe na uhakika muda uliobaki tunauona ni mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, sambamba na eneo la kivuko cha Pangani, kuna ule ukuta wa bahari ambao unazuia maji yasiingie katika Mji wa Pangani, ni ukuta uliojengwa wakati

wa Mjerumani. Naweza nikasema una zaidi ya miaka 120 au 130, umejengwa kwa teknolojia ya zamani sana. Umejengwa kwa mawe ya matumbawe na chokaa kwa wakati ule na udongo ndio ilikuwa sementi ya wakati ule. Mpaka leo ukiuona ukuta ule, unahimili katika baadhi ya maeneo lakini hivi sasa umekwishachoka. Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, inategemea Mfuko wake wa fedha za barabara, unamega kidogo ili kufanya *repair* ya ule ukuta. Kwa kweli ule ukuta hivi sasa linaweza likawa ni janga lingine kwa watu wa Mji wa Pangani. Maji yakijaa *high tied,* yanapanda mita moja *above sea level* na Pangani yenyewe iko kwenye *sea level*. Sasa unaweza ukafikiria ukuta ule ukibomoka, yale maji yataingia katika ule Mji wa Pangani na yale majumba yote yatakuwa ndani ya maji ya chumvi, angalau kwa kina cha mita moja. Ni gharama au ni hasara kubwa kwa vifaa mbalimbali katika majumba yaliyokuwepo pale Mji wa Pangani.

Kamati ya Miundombinu ilifika Pangani, imeona hali halisi ya ukuta ule. Mimi niliwaeleza na wao wakaliona, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwepo. Nimeomba kwamba, zitengwe fedha ili kunusuru ule ukuta kwa maana ya kujengwa upya. *Estimates* za haraka haraka zilizowekwa pale, zinahitajika karibu shilingi 600 milioni kujenga ule ukuta wa bahari, ambao uko katika pande zote mbili za Mji wa Pangani. Kwa maana Mji wa Pangani uko katika ukingo wa Mto, yaani mwishoni unaingia baharini na ndio tuseme mwisho wa Mto wa Pangani. Sasa kiungo kile cha kivuko na ukuta wa bahari upande huu wa Pangani kuna Kata nne upande wa pili kuna Kata tisa, jumla Kata 13. Uchumi mkubwa uko katika upande wa pili, ambao ndio unaounganisha barabara ya kutoka Pangani kupitia Saadani Bagamoyo hadi Dar es Salaam. Kutoka Pangani mpaka Dar es Salaam ni kilomita 150. Sasa kwa *aspect* ya kiuchumi ile barabara ni muhimu sana, kiusalama ni muhimu sana sasa sijui Serikali ina mpango gain? Pamoja na kwamba, taarifa tuliyopewa kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, naipongeza kwamba iko mikakati ya kuhakikisha kwamba, hii barabara inafika mahali inakuwa katika kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu vile vile kwamba, sasa hivi kuna Hifadhi ya Taifa ya Saadani, tunazungumzia utalii. Utalii kwa maana tunazungumzia ukuaji wa uchumi, barabara hiyo mimi Pangani niite ni MKUKUTA namba moja, kwa wananchi wa Pangani. Pamoja na juhudi za Serikali za kuleta fedha kwa ajili ya kuwasaidia wananchi waondokane na umaskini, lakini barabara yenyewe tu ikijengwa ni MKUKUTA tosha. Naiomba sana Serikali, pamoja na juhudi inazofanya, lakini vile vile itazame *priorities* za kiuchumi katika nchi hii, tunahitaji fedha kwa ajili ya kukidhi bajeti ya nchi hii. Yako maeneo mengi sana ambayo yako tayari, yameiva, kinachotakiwa ni kwamba, tupeleke juhudi na kupeleka mafungu ya fedha ili tuongeze zaidi Pato la Taifa katika uchumi wetu.

Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 23 alisema, kukamilisha ujenzi wa daraja jipya Mpiji, ambalo litawezesha njia mbadala ya Dar es Salaam - Tanga. Mimi ninavyofikiri, Daraja la Mpiji limeiunganisha Dar es Salaam na Bagamoyo. Lakini daraja litakalounganisha Dar es Salaam - Tanga aidha, kwa kupitia Msata au kwa kupitia Saadani, ni Daraja la Makurunge, ambalo liko kwenye Mto Ruvu. Mto Ruvu kuna lile Daraja la Ruvu tunalolifahamu kutoka Mlandizi, lakini ukienda

*downstream* ndiyo utalikuta Daraja la Makurunge, ambalo kuna *Bailey bridge* pale ya Jeshi, lakini limeruhusiwa kupita tani tano. Ndiyo maana wakati ule lilipoharibika lile Daraja la Lugoba, magari yalishindwa kupita barabara ya kupitia Msata kwenda Bagamoyo Dar es Salaam kutokana na daraja lile.

Daraja la Makurunge na daraja lingine lililopo *downstream* Wami, haya ndiyo madaraja mawili muhimu ya kuweza kuunganisha kwa dharura zote kiusalama hata kwa wananchi. Sasa waanze kutumia hiyo barabara, tukipata madaraja haya mawili, tutakuwa tumepiga hatua nzuri na hatua ya awali kuhakikisha kwamba, hii barabara sasa inaanza kupata matumaini ya kupitika wakati wowote. *TANROADS* wanafanya kazi nzuri katika eneo la Bweni mpaka Mkwaja. Sasa kutoka Mkwaja kwenda Saadani na kutoka Saadani kwenda Wami na kutoka Wami kwenda kwenye Daraja la Makurunge, kama nilivyosema awali, pana kilomita 150 ukifika mpaka Tanga ni kilomita 200. Mheshimiwa Waziri, wewe ni mdau wa hii barabara ukitaka kwenda Rombo. Hata Mheshimiwa Mary Nagu, pia ni mdau wa barabara hii ukitaka kwenda Hanang ni karibu sana.

Mheshimiwa Spika, sasa umuhimu wa hii barabara unafahamika vizuri sana. Mimi naiomba tena Serikali, iharakishe pamoja na watalaamu, hebu wakae wafikirie kwa sababu mlitupanga katika utaratibu wa *Build Operaton and Transfer (BOT)*. Inawezekana ikacheleweshа ujenzi wa barabara hii. Naona kuwe na utaratibu mwingine, ambao utaweza kuharakisha hii barabara.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka kusisitiza daraja ambalo linaunganisha Pangani na Tanga, Daraja la Choba. Serikali imetenga pale karibu shilingi 100 milioni na imekwishateua mkandarasi na mkandarasi amekwishaanza kazi. Lakini inaonekana mkandarasi yule kidogo katika hatua za utekelezaji, aidha, *foreman* aliyemweka pale anazembea ile kazi imeshapita muda mrefu, mpaka sasa hivi lile daraja hata kuinua zile kingo mbili za ukuta upande mmoja na wa pili ili kuweza kufunika lile daraja, bado hajakamilisha. Nafahamu kwamba, Mkataba uko vizuri tu kwamba, mkandarasi halipwi mpaka ile hatua aliyofikia imekamilika. Lakini tulichobaini ni kwamba, yule *foreman* aliyekabidhiwa kujenga lile daraja au kusimamia lile daraja, anauza sementi na nondo, japokuwa haitokuwa ni hasara kwa Serikali, lakini hasara ni ya yule mkandarasi na hatimaye tatizo tutakalolipata ni ucheleweshaji wa kukamilika kwa daraja lile. Nimekwisha zungumza na Meneja *TANROADS*, nimemweleza hizi taarifa wananchi wenyewe katika vijiji vile, wamenifuata wamenieleza kwamba, sementi inauzwa, nondo zinauzwa, kwa hiyo, kwa kweli inaleta tabu kidogo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nataka kumwomba Mheshimiwa Waziri, Kivuko cha Pangani wakati mmoja kilisogea pembeni, wakati basi linataka kuingia kwenye kivuko. Kosa sio la mwenye basi, kosa lilikuwa ni wale *operators* wa kivuko, hatimaye basi likaingia Mtoni likaharibu unga wa ngano, mchele na sementi ya abiria, ambao walipakia shehena zao. Hiyo ilikuwa ni Serikali ya Awamu ya Tatu, Waziri alikuwa ni Mheshimiwa John Magufuli na nilimweleza ile habari, Serikali kwa maana Wizara, ilionyesha nia ya kuweza kuwafidia hasara waliyopata abiria wale, pamoja na yule mwenye basi kwa sababu kosa lilikuwa sio la kwao.

Mheshimiwa Spika, nataka kumwambia tena Mheshimiwa Waziri, hoja ile nitaileta tena kwako, naomba uitazame upya na hatimaye tuweze kuwafidia wale wananchi, kwa sababu bado naulizwa hatma ya bidhaa zao zilizoharibika katika basi lileb wakati kosa sio la mwenye gari, isipokuwa ni *operators* wa kivuko.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nasema naunga mkono hoja mia kwa mia na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Miundombinu ambayo imeletwa leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kuchangia, kama ilivyo utamadani wetu, ni vyema nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze Watendaji wote waliochaguliwa ndani ya Chama, hususan Mheshimiwa Makamba ambaye ndiye Katibu aliyebeba jahazi hili lote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, nichukue nafasi hii, kwa kuwa sikupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu, nimpongeze kwa hotuba yake nzuri na kazi nzuri anayoifanya kwa kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Mawaziri na Manaibu Waziri wote kwa kazi nzuri waliyoifanya ambayo wametupa matumaini makubwa kwa sisi Wabunge na wananchi wa Tanzania nzima kwa ujumla. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Basil Mramba kwa kazi nzuri anayoifanya. Sina wasiwasi naye, haya yote tunayoyazungumza atayatekeleza.

Pia, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye nina uhakika kwa uzoefu wa Wizara hii atafanya kazi nzuri kwa ushirikiano mzuri na Mheshimiwa Waziri. Nimpongeze Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga pia kwa ushirikiano mzuri na kazi nzuri. Sina wasiwasi nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kukupongeza wewe mwenyewe binafsi kwa kuchaguliwa kukaa kwenye nafasi hiyo. Nilipokuwa nachangia hotuba ya Mheshimiwa Rais ulikuwa haupo. Kwa hiyo, naomba nikufikishie mimi mwenyewe moja kwa moja kwamba nakupongeza.

Pia, umetutoa wasiwasi watu wa Tabora baada ya kuona kwamba hicho Kiti ni kizito, lakini kwa sasa hivi nina imani wale wote waliokupigia kura wameshaona mafanikio yako, uaminifu wako na utendaji kazi wako mzuri na pia wananchi wa Urambo hususan Jimbo la Urambo Mashariki ambao walikupigia kura wewe, wana imani hawakuipoteza na utaweza kuwatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, sasa niingie kwenye hoja ambayo ni changamoto kwa siku hii ya leo. Naungana na Mheshimiwa Selelii, lakini nasikitika sana kuona kwamba Mheshimiwa Basil Mramba hakuiona vizuri hiyo barabara itokayo Dodoma – Itigi – Tabora kwa sababu ilishachangiwa sana katika Bajeti ya 2005/2006. Lakini nimeshangaa leo kutokuiona katika utaratibu wa mchakato mzima wa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nadhani leo watu wa Tabora tuthibitishiwe: Je, hii barabara bado ni ya Mkoa au ni ya Taifa? Kama ni ya Taifa na kama ni ya Mkoa majibu yake yapatikane leo. Kwa sababu hii barabara ina umuhimu wake, inaunganisha mpaka Mkoa wa Kigoma. Tunapozungumzia Tabora, ni pamoja na Kigoma. Sasa kama Waziri pamoja na *Cabinet* nzima hawakuliona hili, naomba lipewe umuhimu wake. Kwa kuiingiza kama ahadi ya Mheshimiwa Rais, sio kweli. Hii ilikuwa ni ahadi ya Wizara wakati wa Awamu ya Tatu. Sasa kama watamtwisha mzigo Rais, Mheshimiwa Kikwete, wanafanya makosa makubwa sana. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu akae upya, aliangalie hili suala la barabara hii inayounganisha Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wa Tabora, watu wa Kigoma tunateseka sana kwa kukosa barabara za uhakika. Wenzetu wanaolia, ni kweli kila mtu ana matatizo yake, kwa sababu kila mtu anapolia anashika kichwa chake kutatua matatizo yake. Huwezi ukalia ukashika kichwa cha mwingine.

Kwa hiyo, kwa upande wangu namuunga mkono Mheshimiwa Selelii kwamba hebu tupate uhakika wa hii barabara inayotoka Dodoma – Itigi – Tabora hadi Kigoma, hatima yake ni nini? Kama ipo katika upembuzi yakinifu, hivi utafanywa kwa miaka mingapi? Wanaofanya huo upembuzi yakinifu ni wataalam kutoka wapi? Kwa sababu kuna Watanzania ambao wamesomea hiyo kazi. Sasa kama ni Watanzania wanaweza kucheleweshaupembuzi yakinifu kwa muda wa miaka 20, basi ujue hatundewi haki wananchi wa Tabora na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, ninazosababu kuu za kuomba Serikali itoe kipaumbele kwa barabara hii. Kipaumbele chake ni hivi, Tabora na Kigoma tuna mazao mengi sana lakini uwezo wa kuyaleta Dar es Salaam hatuna. Basi tusaidiwe hii barabara hata tuweze kuuziana wenyewe kwa wenyewe kutoka Mkoa wa Kigoma wakaleta Tabora na sisi tukatoa Tabora tukapeleka kule kwa sababu mazao yanayolimwa Tabora siyo ambayo yanalimwa Mkoa wa Kigoma.

Pili, sisi sasa hivi tunateseka! Pia, baadhi ya bidhaa ni ya ghali mno! Hata hivyo, niwapongeze wafanyabiashara wa kule, wanafanya kazi katika mazingira magumu. Biashara hata kama ya ujenzi, mathalan *Cement*, nondo na kadhalika bei yake ni kubwa. Ukiangalia gharama za kusafirisha, pia wao kukodi ni taabu! Wenye magari wanalalamika na bado wanaleta kwa shida sana.

Mheshimiwa Spika, pia tuna tatizo la tumbaku. Wananunuzi wa tumbaku wanalalamika kutokana na gharama za uendeshaji. Kwa hiyo, bei ya tumbaku hususan kwako, tumbaku inalimwa sana kwako, lakini bei yake inakuwa chini kutokana na gharama za usafirishaji. Tumbaku inatoka Tabora kwenda Morogoro, barabara zake ni mbaya kiasi ambacho kama inatengenezwa, ni masaa matatu, manne mtu ameingia

Tabora au Kigoma. Hivi Serikali inapata kigugumizi gani? Hebu tusaidiwe kwa hili! Hivi hawaoni kwamba kuna faida ndani yake! Hawaoni kama kuna umuhimu wa kufanya kitu cha namna hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote, namwomba Mheshimiwa Mramba hebu atuangalie aombe *Cabinet* yake waandae upya, angalau hii barabara iweze kuingia humu. Kwa mfano suala la barabara za Mkoa tu wa Tabora, suala la Mkoa wa Tabora katika jedwali la Mheshimiwa Waziri Mkuu, umepewa Shilingi milioni 800 kwa Mkoa mzima. Sasa siwezi kuzungumzia Dar es Salaam ambayo imepewa Shilingi bilioni nane, siwezi kuzungumzia kwa sababu kila mtu na nafasi yake aliyopewa. Lakini hivi kulikuwa na ugumu gani wa kuziongeza hizo pesa angalau kuweza kufungua barabara baina ya Wilaya na Wilaya ili tuweze kufanikisha maendeleo ya Mji wa Tabora? Kwa sababu Mkoa wa Tabora uko nyuma na Mkoa wa Kigoma ndiyo sisemi! Nani atawajali kule tena, maana wako magharibi kabisa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninapozungumza, ni lazima nione na umuhimu wa kutengeneza miundombinu ndani ya Kigoma. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kuwe na ufunguzi wa barabara ya kutoka Tabora kwenda Mbeya. Ni muhimu sana. Mimi huwa nasafiri kwenda Mbeya, ni masaa kumi umeshaingia Mbeya kutoka Tabora. Kwa hiyo, tunapata viazi, badala ya sasa hivi viazi wanatuuzia kilo Sh. 500/= tungepata kwa 200/= na wananchi wanaolima zao la viazi Mbeya wangepata soko. Kwa hiyo, ni soko ambalo sisi tunataka, kama Watanzania, tumezoea masoko ya kwenda nje. Lakini masoko ya kuzunguka wenyewe kwa wenyewe Tanzania bado utamaduni huo hatuna. Korosho zingeweza kufika Tabora na wananchi wa Tabora wakajua, maana ya korosho hakuna. Kwa hiyo, ninafikiri pamoja na mipango mizuri tunayoipanga, utekelezaji wake uwe unaangalia na jiografia ilivyo.

Miaka ya nyuma angalau kulikuwa na tabaka la Vyuo, angalau Wakoloni walikuwa wanaona. Waliona ili kuitangaza Tabora ni lazima tuweke vitu kama hivi. Kwa hiyo, Tabora ilikuwa inaeleweka hata kwenye Jiografia ya wanafunzi shuleni. Lakini kwa sasa hivi, Mheshimiwa Mramba hebu liangalie hilo upya, ulione unalipangaje angalau Tabora na Kigoma ziweze kusikika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye suala ambalo mimi siilaumu Serikali, lakini hivi *Cabinet* nzima chini ya Waziri, mawazo yake Waziri hakuyapeleka kwenye *Cabinet* kuhusu Uwanja wa Ndege wa Tabora kwamba ni sehemu ya usalama wa Taifa?

Mheshimiwa Spika, hivi kama tukipeleka Viwanja vya Ndege sehemu nyingine kukatokea la kutokea, maana viwanja vinavyokwenda labda Mwanza, Kigoma kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali na nini, lakini tatizo kubwa lililopo nasikia Mwanza hamna. Tatizo lililopo Tabora, kuna mambo mengi ambayo yalifanyika na sababu za msingi za kuweka Kiwanja cha Ndege cha Tabora. Miaka ya nyuma kulikuwa na *Contractor* ambaye anaitwa *Muldan Rose*. Yule alianza kukitengeneza kile kiwanja kwa ajili ya usalama. Hivi itakapotokea vita, mtakimbilia wapi? Usalama wake utakuwa wapi?

Mimi ninaomba, kwa sababu kiwanja hiki kilikuwepo tangu mwanzo kwenye mipango ya nchi hii na kiliondolewa baada ya vita ya Kagera, ninaomba Mheshimiwa Waziri, hebu liangalie hili suala la Kiwanja cha Ndege cha Tabora kirejeshwe tena. Kwa sababu kilikuwepo kwenye *program* zote na usanifu ulishafanywa na kila kitu kipo, hebu pekueni kwenye kumbukumbu zenu ili mwone kiwanja hiki mnakifikiriaje?

Mheshimiwa Spika, suala la reli kwa kweli ni tatizo. Kwanza nimponge Mheshimiwa Naibu Waziri Mama Maua Daftari. Tulikutana naye kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, tuliyomwagiza aliyatekeleza yote kuhusu wasafiri. Kwa hilo, nampongeza sana. Ni kitu hatujakizoea! Hatujakizoea tu, lakini kuna mambo ambayo alipewa afanye na kweli nimefuatilia nimeona. Ahsante sana mama yangu nakupongeza sana kwa kazi nzuri uliyoifanya na kweli umeitikia agizo la Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Lakini pamoja na hayo, wananchi walikuwa wanaridhika sana kusafiri moja kwa moja kutoka Dar es Salaam kwenda Tabora, Mwanza Kigoma hadi Mpanda. Lakini kwa utaratibu huu, hatujui itachukua muda gani. Kama ni reli imeharibika, kama ni reli imechoka, Serikali ina mpango gani wa kuboresha au kukamilisha kabla ya ubinafsishaji? Atakapokuja mwekezaji, inawezekana huduma za abiria zitakwama, hatapata faida!

Kwa hiyo, ninaomba Serikali iangalie upya ni jinsi gani watatatua hili tatizo ili akina mama na akina baba wanaohangaika kuhamishwa kwenye mabasi hapa waweze kukamilisha angalau usafiri uwe rahisi.

Mheshimiwa Spika, lingine, kuna wafanyabiashara wadogo wadogo hawawezi kusafirisha mizigo yao kwa kutumia haya mabasi kutoka Dar es Salaam walete hapa, wapakie, wapeleke. Sijui kuna utaratibu gani wa kuwasaidia hao watu! Ni vyema ieleweke kwamba kuna mabehewa ya walalahoi ambayo wakifika, wanapakia mizigo yao kwa bei nafuu. Lakini pia lazima mfanye mipango ya kukubaliana na wenye magari makubwa ili wale wanaopakia biashara zao ndogo ndogo, basi wapunguziwe ile gharama. Mimi naomba tusaidiwe kwa sababu tunateseka sana katika suala la usafiri.

Mheshimiwa Spika, suala la *TAZARA*, naomba nalo liangaliwe upya kabla hatujapa Mwekezaji. Kwa sababu wale wachina walitufadhili, wametukopesha, tumeiendesha *TAZARA* na sasa hivi wameongeza fedha za kutukopesha kuendesha *TAZARA*. Leo mnapomwingiza mtu mwingine watatuelewaje? Kwa hiyo, ni vyema kama kutakuwa na uwezekano wawekeze wenyewe ili angalau kuweze kuwa na urahisi. Maana tukianza kusuguana tena kupishanapishana kwamba tunatafuta mwekezaji mwingine nje ya Wachina, hawatatuelewa. Waliijenga kwa madhumuni na kwa maana maalum ya ukanda wa Kusini. Mimi nadhani ni vyema Mheshimiwa Mramba unapojaribu kutoa maoni yako kuhusu ubinafsishaji, mimi ningekuomba uliangalie upya, ni vyema wakakabidhiwa Wachina wenyewe ili wawekeze wenyewe, ndiyo wenye kuiendesha. Tusiwategemee watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, nimeongea, nadhani sina wasiwasi yatakuwa yamechukuliwa na wenzangu. Nirudie kwa kumpongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama

kwa kuendesha Kiti vizuri na kuteuliwa kwake pamoja na Mheshimiwa Job Ndugai. Nilikuwa nimesahau, naomba mniwie radhi, ni miongoni mwa watu niliopanga kuwapongeza na kuwapa pongezi zao nyingi kwa kazi ambazo wamezifanya pamoja na mama yangu Anne Makinda ambaye ni mzoefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, pamoja na kwamba nimezungumza kwa lugha ambayo inaeleweka, wameielewa na ya jazba, yote haya ni kutokana na kutafuta jinsi ya kuupanga MKUKUTA ili twende nao sambamba na sera za Chama cha Mapinduzi. Naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Nimeshakupongeza, bahati mbaya hukuwepo, lakini naomba nirudie kukupongeza na hasa kwa *speed* yako unayoitumia hapa Bungeni, inaonekana. *Speed* yangu ya kuongea sio kali sana, kwa hiyo nitajikita katika maeneo machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wao wote kwa hotuba waliyotuletea hapa. Kengele ya mwisho inaweza kupigwa kabla sijaunga mkono, kwa hiyo, natanguliza kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni barabara. Naomba niongelee kwanza Barabara za Kwimba. Ninapoongea juu ya Kwimba, naongelea barabara tatu tu. Naongelea juu ya Barabara ya Mabuki – Malampaka, Barabara ya Mwamahya kwenda Itongoitale, Barabara ya kutoka Mabuki - Malampaka kwenda Malya na kutoka Malya mpaka Sumve, halafu, kwenda Mwanza. Nimeangalia barabara kutoka Mabuki kwenda Malampaka sijaiona. Isipoonekana barabara hii ina maana mtu wa Ngudu Makao Makuu unamfunga. Hawezi kusafiri. Nimeona kutoka Ngudu kwenda Jojiro. Sasa baada ya kufika Jojiro, anakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, kutoka Jojiro kwenda Malampaka hakuna fedha na kutoka Jojiro kwenda Mabuki hakuna fedha. Nilikuwa nafahamu barabara hii ya Mabuki - Malampaka iko katika mpango wa Benki ya Dunia, lakini bado sijaziona vizuri. Naomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kufunga hotuba yake, atuhakikishie watu wa Kwimba, wa Kata ya Nyamilama na watu wa Maswa kama barabara hiyo ipo au haipo na kama inafungwa au la. Maana inawezekana Mheshimiwa Waziri ana mpango wa kuleta ndege kutoka Maswa kwenda Mwanza. Nilikuwa naangalia fedha zilizotengwa kwa barabara kutoka Magu, kupitia Ngudu kwenda Jojiro, ni kilomita 64. Fedha zilizotengwa ni Shilingi milioni 57. Siku nyingi sijaingia darasani, wanasema kilomita moja ni chini ya Shilingi milioni moja: Je, ni kweli? Yupo mkandarasi anayeweza kufanya kazi hiyo au zinajengwa kwa utaratibu gani? Hapo nilikuwa naomba kusaidiwa kama kweli Wizara ina nia ya kuyafungua Makao Makuu ya Wilaya ya Kwimba. Mara nyingi nasema kwamba inawezekana Kwimba haijulikani iko wapi au watu wanakutana nayo tu kwenye vitabu.

Kwimba imegawanyika ikatoa Magu, ikatoa Misungwi, lakini haikui kwa sababu haijafunguliwa. Wakati wa mvua, mtu wa Ngudu hawezi kusafiri kwa sababu kutoka

Jojiro kwenda Mabuki hakupitiki, kutoka Ngudu kwenda Malya hakupitiki na ndiyo maana wafanyabiashara wengi kutoka Ngudu wanahama kwenda Mwanza, Shinyanga, Magu, Makao Mkuu ya Wilaya ya Kwimba hayakui kwa sababu haijafunguliwa. Naomba sana, Mheshimiwa Waziri wakati ana-*wind up* atuambie barabara hizi mbili Mabuki - Malampaka ipo au haipo!

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee juu ya barabara ya kutoka Mwamahya kwenda Itongoitale. Barabara hii ni muhimu sana kwa watu wa Tarafa ya Mwamshimba, ndiyo inayosafirisha mazao kutoka katika eneo hilo. Imetengewa pesa lakini naona haitoshi. Kuna daraja la Buyogo kwenye mto Mwame ambapo upande wa pili wa Misungwi, ndiyo iliyoua watu wengi sana. Nisingependa kusikia kwamba kwenye daraja hili la Buyogo watu wanaangamia katika utaratibu huo uliotokea kwenye Wilaya Misungwi. Sina hakika kama fedha hii inatosha hata kukarabati barabara ile pamoja na daraja la Buyogo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana angalau kwa mara ya kwanza Wizara inataja kwamba imebadilisha mtambo wa simu. Wilaya ya Kwimba kama nilivyosema mwanzo, Makao Makuu yake yako. Mitambo ya simu Ngudu, ni ya zamani sana, kwani bado simu zake ni za kukoroga, vidole mpaka vinauma. *(Makofi/Kicheko)*

Labda safari hii ndiyo tumekumbukwa, sina uhakika. Maneno haya huwa yanajitokeza mara kwa mara. Nimemsumbua sana Mheshimiwa Maua Daftari. Naomba sana. Kuweka mashine siyo hoja, tunachohitaji kujua ni mashine hizi zitaanza kufanya kazi lini? Kwa sababu sisi kuziangalia zile mashine haitoshi, tunaka kuzitumika.

Nashukuru watu wa *Mobile Phones*, nashukuru watu wa *TIGO* wapo, *VODACOM* wanakuja. Lakini hebu jiulize, nashindwa kusema ahsante kwa sababu moja tu, hakuna umeme Mjini. Hivi unaweza kuendesha simu za mkononi bila umeme? Uta-*charge* kwa njia gani? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sina hakika kama kuna mawasiliano mazuri sana kati ya Makampuni ya Simu za Mkononi na watu wa *TANESCO* kwa sababu hawa wanatakiwa kwenda pamoja. Mimi nashukuru kwamba angalau zipo, watu wanasafiri kwenda ku-*charge* Mwanza kilomita 80, unaporudi anatumia kidogo *charge* imekwisha. Lakini angalau anayo mkononi, tunashukuru. Tunaomba na watu wa *VODACOM* waje, wameahidi kuja. Tungependa wafike.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la reli. Mimi nashangaa sana. Mtu anakuja kwangu kama Mbunge anasema Mheshimiwa naomba nauli ya kwenda Dar es Salaam. Nampatia nauli ya kutosha kutoka Mwanza mpaka Dar es Salaam, halafu analazimishwa kuteremka Dodoma kwa gharama ya nani? Anatoka Dar es Salaam anakuja kutua Dodoma kwanza, kwa gharama ya nani? Hapa Dodoma ombaomba ni wengi sana, sio Mheshimiwa Chibulunje. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninachoomba Shirika hili lifanye utaratibu, mtu atoke Dar es Salaam kwa mabasi maalum, akifika hapa anakuja kuunganishwa kwenye treni,

lakini kwa nauli ile ile ya treni. Ikitokea treni au mabasi hayo yameharibika njiani, treni ikaondoka, basi hao wasiathirike, iwe gharama ya watu wa reli. Hamuwatendei haki wasafiri wanaotoka Dar es Salaam kwenda Mwanza kwenda Kigoma na Tabora na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuleta utaratibu huu, mimi naamini ilitakiwa utafiti ungelifanyika na ifanyike, maamuzi mazuri yafanywe ili watu hawa wasipewe adhabu ambayo hawana mpango nayo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, nashukuru sana mimi nimeshaunga mkono ila naomba nisaidiwe kupewa maelezo hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bujiku kwa mchango wako. Kwa sababu muda uliobaki hautuwezeshi kumwita mchangiaji yoyote, ninayo matangazo yafuatayo: Kwanza Mheshimiwa Omar Kwaangw' anaomba Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii wakutane leo saa 10.00 jioni, Chumba Namba 219 jengo la Utawala kwa kikao kifupi.

Pia, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)*, Mheshimiwa Halima Kimbau, ameniomba nitangaze kuwa saa 7.15 Wajumbe wote wa *LAAC* wakutane kwa kikao kifupi cha kujadili safari yao ya kwenda Dar es Salaam kesho tarehe 4 Julai, 2006.

Mkutano huo utafanyika saa 7.15 katika Ukumbi Namba 227 ghorofa ya nne jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo na kwa kuzingatia kwamba zimebaki dakika mbili na nusu tu, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.57 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni, Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Msemaji wa kwanza kwa jioni hii, nimeombwa na Waheshimiwa kutoka Mkoa wa Mtwara yaani Waheshimiwa Hawa A. Ghasia, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Dunstan D. Mkapa, kwamba, kuna wageni wao kutoka Mkoani. Sina hakika wako upande gani, ni watumishi na viongozi kutoka Mkoa wa Mtwara, nadhani Wilaya mbali mbali kama Vile Masasi, Nanyumbu na kadhalika.

Ningeomba pale walipo wasimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwatambua. Sijui, ndio hao wanaingia sasa, labda! Ahsanteni sana! Karibuni kutoka Mtwara, tunafurahi sana kuwa nasi hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza. Nitakuwa natangaza mabadiliko kidogo katika orodha kwa sababu nimegundua kwamba baadhi ya wale Waheshimiwa waliokwishachangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, wamejitokeza mbele. Ipo nafasi ya takriban wote kuweza kusema.

Lakini sasa, nitakuwa nachukua wale ambao hawajaongea kabisa ili waweze kupata nafasi. Tunaanza na Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Nyaulawa, wakati huo huo Mheshimiwa Mudhihir ajiandae.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kunipa nafasi ya kuwa mzungumzaji wa kwanza jioni ya leo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, nimepata taarifa kwamba, pale Kijijini kwangu Itepula ninakotokea, kuna Mzee wangu mmoja mtu mzima sana na pia ambaye alikuwa rafiki wa baba yangu sana huyu Mzee Benson Mwamengo, amefariki dunia jana trehe 02 Julai, 2006. Naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu pamoja na Manaibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara na wataalam wote Wizarani kwa kuandaa hotuba ambayo nina hakika ni nzuri. Nasema ni nzuri kwa sababu mengi yanayozungumzwa kwenye hotuba ya Waziri, bado inajibu yale ambayo Serikali inayazungumza kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati yangu ya Miundombinu. Napenda pia niseme kabisa kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu. Nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu kwa Taarifa yake nzuri aliyoitoa hapa Bungeni asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, aidha, nimshukuru pia Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Ndugu yangu Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, kwa taarifa yake pia ambayo mimi nasema ni nzuri, kwa sababu ina ushauri na uelekezi kwa Serikali kuweza kufanya yale ambayo inaipasa Serikali ifanye. Kuna wenzangu wengine asubuhi wamezungumza kwamba, tutapamba na Serikali. Kwa mtazamo wangu na maoni yangu mimi, sidhani kama tunakuja kupambana na Serikali. Lakini, nadhani tunakuja tuzungumze na Serikali, tuishauri pale ambapo tunadhani inaweza kurekebisha, basi irekebishe. Lakini inawezekana Serikali isitekeleze yote kwa sababu ya uhaba wa fedha, basi nina hakika na sisi Wabunge tutakuwa tunaelewa tukitumaini kwamba Serikali haiwezi ikatekeleza yote katika mwaka mmoja wa fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, mimi napenda nizungumze kwa ufupi sana. Kwanza, nizungumzie Kiwanja cha Ndege cha Songwe. Tunapojenga

Viwanja vya Ndege nchini, maana yake tunafungua milango kwa ajili ya shughuli zetu za uchumi katika nchi hii. Nami nafurahi kwamba Mkoa wa Mbeya ni moja ya maeneo ambayo Serikali iliyaona kwamba yanafaa na ilipendekezwa liwe moja ya maeneo yanayofaa chini ya mpango wa *Special Economic Zone (SEZ),* yaani maeneo maalum ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kujenga Kiwanja cha Ndege Mbeya, maana yake tutakuwa tunafungua kiuchumi Nyanda za Juu Kusini na tumeshasikia kwamba watu wanaotoka nchi za Zambia, Congo, Malawi, Zimbabwe na kadhalika bado wanafikiri kwamba Tanzania ni nchi nzuri kiuchumi, tatizo ni kwamba Dar es Salaam ni mbali. Kama tungeweza kujenga Kiwanja cha Ndege Mbeya, tukajenga *Malawi Cargo Centre* tukapaimarisha vizuri sehemu nyingine ni *Dry Port* kama tunavyozungumza kwa kule Mbeya, tukaimarisha na tukajenga barabara zote za Mkoa wa Mbeya pamoja na Nyanda za Juu Kusini kwa ujumla, nadhani tutakuwa tunafungua nchi hii kiuchumi kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bado naona suala la Kiwanja cha Ndege Mbeya ni la muhimu na mimi namshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba liko kwenye Bajeti, nadhani limetengewa Shilingi bilioni nne. Nina matumaini kwamba Kiwanja kitakamilika mwaka 2008 kama ambavyo inaonyesha kwenye vitabu na kwa maana hiyo, wananchi wa Mbeya na Nyanda za Juu Kusini wataweza kufaidika na huduma zitakazotokana na Kiwanja cha Ndege kujengwa kule Mbeya.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze kwa ufupi sana kuhusu barabara za kule Jimboni kwangu Wilayani Mbozi. Kule Mbozi kuna barabara takriban nne, tano ambazo zinashughulikiwa na *TANROADS*. Barabara ya kwanza ambayo ni muhimu sana unapozungumza uchumi wa Wilaya ya Mbozi ni barabara inayotoka sehemu inayoitwa Mlowo kwenda Kamsamba. Barabara hii ina urefu wa takriban kilomita 140 na inaunganisha Mbozi na Jimbo la Kwela kwa Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya sehemu ya Kiliamatundu, Sumbawanga Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Barabara hii ni muhimu sana. Pamoja na kwamba inahudumiwa na *TANROADS*, matengenezo yake huwa siyo madhubuti sana. Barabara hii mara nyingi wakati wa Masika huwa inakatika sana na hivyo kulazimisha watu kukwama na kulala njiani mara kwa mara. Kwa hiyo, naomba Serikali itilie maanani, iisukume *TANROADS* wafanye matengenezo madhubuti na siyo matengenezo ambayo yanailazimisha Serikali kila mwaka kupeleka pesa nyingi sana kwenye barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, kuna barabara nyingine ambazo ni barabara ya kutoka Ruanda kwenda Iyula, Idiwili hadi Nyimbili, kuna barabara tunaiita *Mbozi Circle*, kuna barabara ambayo inatoka Zelezeta inapita Isansa, Magamba, Ipoloto kwenda Itaka, kuna barabara inayotoka Igamba kwenda Msangano. Zote hizi ni muhimu sana katika uchumi wa Wilaya ya Mbozi.

Mheshimiwa Spika, nimesema mara kadhaa nilipopata nafasi kusimama kwenye Bunge lako Tukufu kwamba Mbozi ni Wilaya ya kilimo, hata kama tukiwasaidia wakulima vizuri, lakini tusipoimarisha miundombinu hususan ya barabara, tutakuwa bado hatujawasaidia wakulima sana. Kwa hiyo, angalau hizi barabara ambazo zinaunganisha Wilaya kwa sehemu kubwa, kama zikipata matengenezo ya kutosha kwa mwaka, nadhani tunaweza tukawa tumetatua tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, najua nchi hii ina tatizo la barabara sehemu katika mbali mbali. Lakini kama tulivyosema, kila mtu hulia pale inapostahili na Mawaziri wajue kwamba kuna tatizo. Katika hili, ningeomba kabisa nimwombe Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Mramba apate nafasi ya kuja kutembelea Wilaya yangu au Jimbo langu la Mbozi Mashariki. Kwa sababu yeye najua alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, inawezekana anazifahamu hizi barabara zote ninazozizungumza, ingekuwa sio vibaya akamtuma hata Naibu wake anayeshugulikia barabara Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga tuje tumtembeze ili tutakapokuwa tunazungumza matatizo ya barabara awe anazielewa. Nashukuru kwamba maeneo mengine amefika na bila shaka hatasita kuja kuzitembelea barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, hii barabara ya Mlowo – Kamsamba, sehemu yenyewe ya Kamsamba ambayo ni Jimbo la Mbozi Magharibi, kuna Daraja kwenye Mto Momba ambako wananchi hulazimika kuvuka kwa kamba wakati wanakwenda kwenye Tarafa ya Kipeta kule Sumbawanga au kutoka huko kuingia Mbozi. Ni hatari, watu kuvuka mto mkubwa kama huo kwenye kamba na wakati mwingine watu hutumbukia kwenye Mto ambao una mamba wengi sana.

Kwa hiyo, tunapofikiria kuunganisha maeneo muhimu kiuchumi, basi Serikali ifikirie kujenga daraja kwenye Mto Momba Kata ya Kamsamba kuunganisha Kata ya Kiliamatundu kwenye Jimbo la Kwela. Natumaini Mheshimiwa atakapokuwa anajibu hoja, basi atatuambia kwamba pengine Serikali ina mipango gani.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala la *TAZARA* na *TRC*. Suala la *TAZARA* na *TRC* kama wenzangu wengine walivyozungumza, bado ni suala muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Sasa kitu ambacho nazungumza, kwa mfano cha pamoja kati ya *TRC* na *TAZARA* ni *Fuel Levy*. Tunajua mafuta yote hutozwa kodi, lakini *Fuel Levy* inayotozwa katika Mashirika haya mawili, hayanufaiki kabisa na fedha hizi. Najua mwaka 2005 Serikali imetoa Shilingi milioni 100. Serikali imetoa milioni 100 kwa *TAZARA* na kwa *TRC*. Lakini nikiangalia na *Fuel Levy* ambayo Mashirika haya mawili yanalazimika kulipa na wakati huo huo kuyapa Shilingi milioni 100, sio kuyatendea haki hata kidogo!

Mheshimiwa Spika, tunazungumza kuimarisha *TRC*, tunazungumza kuimarisha *TAZARA*, mimi nadhani ingekuwa busara kama Serikali ingefikiria angalau asilimia 50 ya fedha za *Fuel Levy* ambazo Mashirika yale yanalipa, basi ziwe zinarudishwa kwa Mashirika hayo ili yaweze kutumia kiasi hicho kurekebisha miundombinu yake na nadhani wanaweza pia wakaendelea kulipa kodi hiyo kwa moyo mkunjufu kabisa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine kwa *TAZARA*, ninaomba Mheshimiwa Waziri alisemee. *TAZARA* yenye takriban wafanyakazi 3,433 kwa Reli nzima, ina matatizo makubwa sana kwenye *Terminal Benefits* za wafanyakazi wake.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi *TAZARA* inadaiwa takriban bilioni moja na *NSSF*. Inawezekana ni zaidi, lakini siyo chini ya bilioni moja. Hiyo nina hakika sana. Naomba Serikali na hasa Wizara ilizungumze hili suala kwa sababu Watanzania wengi wanapata shida sana. Tulipotembelea *TAZARA*, niliwaambia kwamba wananchi wa nchi hii wanateseka. Wametumikia nchi sawa sawa, wametumikia nchi vizuri, lakini wanapostaafu wanapata shida kweli!

Mheshimiwa Spika, mtu anakaa Mwanza, anastaafu *TAZARA*, anasafirishiwa mizigo yake, halafu pensheni yake anaambiwa atafuatilia. Lakini, inamchukua huyu mtu pengine miaka miwili, mitatu kulipwa pensheni yake. Ametembea Dar es Salaam mara ngapi? Bado anapokwenda Dar es Salaam halipwi pesa zozote za kujikimu kwa siku zile ambazo anafuatilia. Sasa, huku ni kuwatesa Watanzania ambao kwa kweli wametumikia nchi yao vizuri, lakini inapokuja kuwalipa, inakuwa ni taabu sana.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali iingilie kati. Najua inawezekana *TAZARA* uwezo wao wa kulipa ni mdogo, lakini Serikali iingilie kati ili iweze kutatua tatizo hili na wananchi wetu wasipate taabu. Kuna Karakana ya *TAZARA* Mbeya. Karakana ya *TAZARA* Mbeya haitumiki sawasawa kwa maana ya kwamba *motive power* waliyonayo *TAZARA* sasa hivi ni ndogo sana. Kwa hiyo, kuna *manpower* kubwa ambayo inakaa tu wakati mwingine bila kufanya kazi ya kutosha, lakini wanalipwa mshahara na marupurupu yote. Huku si kuiangamiza TAZARA zaidi!

Mheshimiwa Spika, suala lingine, mimi nimefanya kazi *TAZARA*. Kulikuwa na utaratibu kwenye vyombo vikubwa au kwenye Ofisi kubwa, kwa mfano Makao Makuu ya *TAZARA* na kwenye Karakana, kwamba kuwe na watu ambao angalau idadi yao inawiana, *one to one*. Lakini, kwa taarifa nilizonazo, Karakana ya Mbeya imejaa Ma-*Engineer* wa Kizambia. Tunapozungumza hivi, siyo kwamba tunazungumzia utaifa, lakini tuangalie yale ambayo tulikubaliana tangu mwanzo kwenye vitabu vya kuongoza, vinasema namna gani. Kwa hiyo, *TAZARA* kumejaa Wahandisi wa ki-Zambia hasa kule Mbeya. Nashauri Wizara ishauri TAZARA irekebishe hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala la kuanzisha *TAZARA* na *TAZARA Act*. *TAZARA Act* inazungumza tu kwamba Mkurugenzi Mkuu wa *TAZARA* lazima atoke Zambia. Sasa, hii huwa siielewi, hasa leo wakati tuna soko huru kwa ajira, soko huru kwa shughuli nyingi hata za kiuchumi. Lakini, bado *Act* ya *TAZARA* inasimama vile vile kwamba Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ile lazima atoke Zambia.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwamba, izungumze na Serikali ya Zambia ilete Muswada hapa Bungeni ili Sheria hiyo iweze kuangaliwa upya na ikiwezekana hata Watanzania wenye sifa pia waweze kugombea nafasi hiyo ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Reli ya Uhuru *TAZARA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie suala la *TMA* kwa kifupi sana. Naomba nisisitize kama baadhi ya wenzangu walivyozungumza kwamba, Mamlaka ya Hali ya Hewa, kwa nchi nyingine bado ni Taasisi ambayo ni muhimu sana. Kwa nchi nyingine, watu hawaendi makazini kama hawajui hali ya hewa leo ikoje. Lakini, kwetu inawezekana ikawa vigumu kwa sababu hata vifaa kwa ajili ya utabiri wa hali ya hewa, walivyonavyo siyo vya kisasa sana. Tunashukuru jitihada za Serikali za kuisaidia Mamlaka hii. Lakini, bado haijafanya vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, leo, *TMA* haiwezi ku-*forecast weather* kwa ajili ya miezi sita ijayo au mwaka mzima ujao. Lakini, wanaweza kukupa hali ya hewa pengine siku tatu, nne au wiki moja ijayo. Sasa, hii haiwezi ikatufanya sisi tukawa tayari kwa ajili ya kujua hali ya hewa ya mwaka kesho itakuwa namna gani ili tuweze kupanga mipango yetu. Pengine kama Mamlaka ya Hali ya Hewa ingekuwa na vifaa hivyo, ingeweza hata kuishauri Serikali, tungeweza hata kuchukua tahadhari na haya majanga ya kuhangaika sana na njaa mwaka huu, pengine yasingekuwepo kuhangaika sana kwa sababu tayari tungekuwa na taarifa za awali. Kwa hiyo, ninaomba Serikali iangalie namna ya kuisaidia Mamlaka ya Hali ya Hewa ili ipate kununua vifaa vya kutabiri hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, pia, naomba Mamlaka ya Hali ya Hewa ijenge Kituo cha Hali ya Hewa Mbozi. Najua wana Kituo kidogo sana, nadhani wanapima mvua tu. Lakini Mbozi ni Wilaya ya kilimo, Mbozi kuna mvua nyingi zinanyesha. Lakini, nadhani ingekuwa muhimu wananchi wakajua hali ya hewa inakwenda namna gani ili waweze pia kupanga mipango yao ya kilimo vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la Chuo chetu cha Usafirishaji na hili nazungumzia suala la kutoa leseni. Mimi nilipotembelea kile Chuo, nilishangaa sana na nadhani hata sehemu nyingine nilipokwenda kutafuta leseni yangu kwa ajili ya kuendesha gari, nilikwenda Polisi kwa ajili ya kutafuta leseni, lakini wenye utaalam wa magari ni Chuo chetu cha Usafirishaji. Nadhani hali hii iangaliwe upya na vizuri zaidi.

Wataalam wa magari ni Chuo cha Usafirishaji, leseni zinatolewa na Polisi sio sahihi. Bahati mbaya sana Polisi wanaopaswa kum-*test* mtu ili aweze kupewa leseni wengi wao hawana utaalam wa kutosha. Mimi nadhani huko kwenda kinyume, naomba Serikali iliangalie hili vizuri ili kazi hii iachiwe Chuo chetu cha Usafirishaji ambacho kwa kweli ndicho kimepewa jukumu la kusimamia Sekta ya magari na mafunzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Chuo chetu cha Dar es Salaam *Maritime Institute*, Chuo hiki, tulikitembelea kama Kamati. Kiko kwenye hali mbaya sana ya majengo. Hakina zana nzuri za kufanyia kazi. Tunaomba Serikali iangalie pia Chuo hiki ili kiweze kufundisha Mabaharia badala ya kuwatuma wengi nchi za nje, basi wengi waweze kufundishwa hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala la Makampuni ya Simu kwamba yajitahidi sana kupeleka simu Vijijini. Mimi Jimboni kwangu wananchi wangu wako tayari kabisa kutumia simu za mkono hasa wananchi ambao wako mbali na kule

Mjini ambako tayari hizi huduma zipo kama Wananchi wa Kata za Itaka, Nambinzo, Halungu, Isansa, Nyimbili na maeneo mengine. Kwa hiyo, ninaomba Serikali hasa Wizara ya Miundombinu iyaelekeze haya Makampuni yajenge minara ya simu huko ili wananchi waweze kufaidika na huduma hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba Serikali iisaidia UDA. UDA, inakufa! Kama kweli tunasema kwamba tunataka kuleta ushindani, *then* UDA haiwezi kushindana hata kidogo! Nimepata taarifa kwamba UDA sasa hivi inadaiwa na Serikali Shilingi milioni 600. Lakini hizi Shilingi milioni 600 zinadaiwa namna gani? Kwa maana ya kwamba kuna kipindi Serikali ilileta magari mabovu aina ya TATA. Yale magari hayakudumu zaidi ya mwaka mmoja, yote yakawa *grounded*, lakini deni wakaambiwa UDA ndiyo walipe. Nadhani tutakuwa hatukuifanyia haki UDA kama tukiendelea kusema walipe hizi Shilingi milioni 600. Kwa maana hiyo, naiomba sana iisaidie UDA kuifutia deni hilo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba barabara ya Sanga Sanga - Mzumbe *University*, ina kilomita 3.5, Serikali iharakishe kuitengeneza. Nadhani Chuo kinakua na kuna shughuli nyingi kule. Nasema hivyo kwa sababu mimi ni Mjumbe wa *Board* ambaye naliwakilisha Bunge lako Tukufu na Wajumbe wenzangu kwenye walinituma *Board* nije niliwasilishe hili Bungeni ili Serikali iweze kulishughukia kwa kuagiza *TANROADS* imsisitizie Mkandarasi anayejenga, amalize kazi hiyo kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kwa sababu kengele karibu inagonga, naomba tena nichukue nafasi hii nimshukru sana Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya hotuba yake. Nadhani ni hotuba elekezi. Mimi naamini Serikali haiwezi kufanya mambo yote kwa wakati mmoja, lakini, basi iweke vipaumbele kati ya Mikoa na Mikoa ili wananchi wote wa nchi hii wafaidike na *resources* zilizopo katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa Richard Nyaulawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mudhihir na Mheshimiwa Kabwe Zitto ajiandae. Sasa namwita Mheshimiwa Richard Nyaulawa.

Mheshimiwa Spika, inaonekana Mheshimiwa Richard Nyaulawa hayupo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mudhihir kama uko tayari, endelea.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa maoni yangu na mchango wangu kwa Wizara hii muhimu ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nachangia hotuba ya Waziri Mkuu nilizungumzia habari ya barabara ya Kibiti – Lindi na nikawa nafikiria pengine kesho wakati wa majumuisho nipate majawabu. Lakini nalazimika kuchangia tena leo kwa sababu jana Waziri wa Miundombinu alituita Wabunge wa Mikoa ya Lindi, Mtwara, Dodoma Singida na Dar es Salaam. Ndiyo nikagundua kwamba kuna ulazima tena leo kwa sababu alisema

jana “Nimewaiteni hapa kutokana na michango mliyokuwa mnachangia kwa Waziri Mkuu. Inaonekana hamwelewi hali halisi ya matengenezo ya barabara”

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wabunge tunaotoka maeneo yale, nafikiri tunaelewa vizuri hali halisi ya barabara kuliko hata wataalam na Mheshimiwa Waziri mwenyewe. Maneno hayo ya jana ndiyo yaliyonisababisha leo niombe kuchangia tena katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge wa Lindi, Mtwara na Ruvuma, tunapozungumzia habari ya barabara, tunazungumza kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005, Ukurasa wa 52, Ibara 44 (b), inayotaja Nangurukuru - Mbwemkuru - Mingoyo, Mkuranga - Kibiti, Ndundu - Somanga na Ukurasa wa 54 inayozungumzia habari ya Mtwara - Masasi, Songea - *Mbamba Bay*. Kwa hiyo, hatuzungumzi kwa kutaka kumbana mtu, tunazungumza kwa kutaka Ilani yetu itekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi napata taabu sana kutambua kikwazo ni nini hadi barabara hizi za Kibiti - Lindi, Masasi - *Mbamba Bay* kuwa zinakwamakwama. Tatizo ni nini? Maana Ilani imesema wakandarasi wamepatikana. Sasa kwa nini kazi haiendi? Wamekuja Viongozi wa Kitaifa pale, Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Alipotaka kuelezwa na Waziri mhusika na yule wa mwanzo alikuwa Naibu Waziri, kisingizio kikubwa kilipelekwa kwamba Kampuni ya Kharafi haifanyi kazi vizuri. Wanajivutavuta mno hawa Kharafi, hawashikiki. Lakini, mimi baada ya maelezo yale ikabidi nifanye kazi ya ziada. Kama tatizo ni Kharafi hashikiki, ilikuwaje huyu wa kutoka Nangurukulu kwenda Mbwemkuru naye hajamaliza? Naye hashikiki! Kuna tatizo gani? Suala la Dodoma - Shelui, naye hashikiki! Au kuna tatizo ndani ya Wizara! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu huyu Kharafi anayejenga kutoka Mingoyo kuja Mbwemkuru aliingia Mkataba wa kujenga madaraja ya *Beam type* 9, 8 yamekamilika; madaraja ya kawaida 18, 16 yamekamilika; Kalvati kubwa 15, 9 zimekamilika; Kalvati ndogo 197,158 zimekamilika; *Linen drains* hizi kwa kilomita 27, kilomita 21 tayari; *Layer works*, kilomita 92, kilomita 50 tayari na *Sub-base process* kilomita 92, kilomita 50 tayari. Kama haya yamewezekana, hili tatizo lingine la kokoto, chanzo chake hasa ni nini? Nauliza hivi kwa sababu katika Mradi ule kuna Afisa wa Wizara ya Ujenzi, lakini kuna *Consultant,* tena tumemtoa nje kabisa, Canada.

Wakati hawa Kharafi wanapasua kokoto Mlima wa Mamba na hawa wataalam wapo, kwa nini hawakuwazuia mapema? Wakatoka pale tena wakaenda kupasua mwamba wa Kikwetu, Mtaalam yupo, *Consultant* yupo, wakaacha zimepasuliwa kokoto sijui kilomita ngapi. Halafu baadaye unasema hii hapana. Kuna ajenda gani? Mimi nafikiri kuna haja ya kuambiwa. Maana haitoshi tu kuwaambia Viongozi wetu, Waziri Mkuu, Rais; “Huyu Kharafi mkaidi! Kharafi mkaidi! Kwa nini hawa wasimamizi wote wapo na hali hii inatokea? Tunashindwa kuizuia! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunachotaka, maana habari hii ya ahadi ahadi, imekuwa tangu baada ya Uhuru. Ilifikia mahali Mheshimiwa Maalim Nabahan Sinani katika Bunge hili alianza mchango wa Sh. 300/= ili watu wa Lindi na Mtwara tuchangie kupitia

Korosho zetu kujenga barabara. Marehemu Sokoine akasema hapana, ni jukumu la Serikali. Sasa, aliyekoswa koswa na nyoka, hata akikanyaga unyasi, hushtuka! Tunaona tunarejeshwa kule kule.

Mheshimiwa Spika, nami ninaposema nina wasi wasi na Wizara, mimi nazungumzia Wataalam ambao ndiyo wako *permanently*. Hawa viongozi wamekuja jana tu, wale akina Mheshimiwa Basil Mramba na wao ndiyo wanapewa hizo taarifa kuja kutupa sisi. Tunataka tarehe, bwana! Hivi Ndundu mpaka Somanga, ujenzi unaanza lini na utakamilika lini? Nangurukuru mpaka Mbwemkuru, ujenzi unaendelea, utamalizika lini? Mbwemkuru - Lindi- Mingoyo, utamalizika lini? Kazi ya usanifu, upembuzi yakinifu kutoka Mtwara - Mnazi Mmoja - Masasi - Tunduru - Songea - Mbinga - *Mbamba Bay*, utaanza lini kipande kwa kipande na utakamilika lini? Hii ndiyo taarifa tunayoitaka hapa. Sisi wenyewe tuisikie na wananchi kule wa Mikoa husika nao waisikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunakuwa na wasiwasi hivi na siyo wasiwasi wa bure. Ukiangalia hiki kitabu cha Nne - Mipango ya Maendeleo, Ukurasa wa 135, mimi sina ugomvi na wananchi wa Kilimanjaro na wao wana haki ya kupata barabara kama sisi wengine. Ndiyo! Lakini, mimi nahoji vigezo vilivyotumika vya kipande cha Marangu - Tarakea - Rongai - Rombo, kutengewa Sh. 17,112,500,000/=, lakini, kipande cha Ndundu - Somanga chenye kilomita 60 kutengewa Shilingi bilioni 7.6 tu na kipande cha Mkuranga - Kibiti kutengewa Shilingi bilioni 5.1 tu.

Mheshimiwa Spika, hata ukijumlisha vipande hivi viwili, bado tunapata jumla ya Shilingi bilioni 12 tu. Hatujafikia hata ile Shilingi bilioni 17 ya kipande kimoja. Narudia, sina ugomvi na watu wa Kilimanjaro kutengenezewa barabara, lakini kama tunasema Sungura huyu mdogo tunagawana kidogo kidogo, hivi ndiyo kidogo kidogo namna hii! "Ukila na kipofu, usimshike mkono, atagundua kwamba unampunja." *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi nalisema hili kwa nia njema kabisa, kwa sababu ndugu zangu historia ya barabara kwa sisi wa Lindi ni ngumu sana. Waswahili wanasema: "Bubu akizidiwa, hutamani kusema." Lakini, Wazee wanasema: "Mwenye hekima, mwenye busara akizidiwa hutamani ububu." Sisi wa Lindi, Mtwara na Ruvuma kwa hili la barabara, hatuutaki ububu, hatuitaki busara hiyo ya kuwa kimya, tunataka tuseme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, historia ya matatizo ya barabara Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma, imeanzia na uchumi wa kikoloni. Wakoloni kwa makusudi kabisa waliamua Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ndiyo watoke wafanyakazi wa Mashamba ya Mkonge na mashamba ya Karanga hapo Kongwa. Sisi tulikuwa Manamba, ndiyo maana leo ukienda Kilosa, unakuta Wayao, ukienda Muheza, Korogwe, tupo Wamakonde kule walikwenda kukata Mkonge, ndiyo ilikuwa kazi yetu, Manamba! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya uhuru, tulifikiria suala la Manamba litakwisha, lakini ndiyo likaja suala la Ukombozi wa Kusini mwa Afrika. Sisi tukatolewa mhanga,

eneo lile likawa kama *Buffer Zone*, hakuna maendeleo mpaka wenzetu wakomboke. Wameshakomboka!

Mheshimiwa Spika, sasa hivi watu wanatamani kubadilisha neno Manamba kwa sababu linakera, wameleta jina lingine, Machinga! Wafanyabiashara ndogo ndogo wanaitwa Wamachinga. Ukiwakamata kumi tu, uwahoji wanaotoka Lindi, Mtwara na Ruvuma, hawafiki watatu. Sasa, Wachaga, Wahaya, wote wanafanya biashara ndogo ndogo, wamachinga tu, yaani katika kutuweka katika hali ile ile. Inaumiza sana! *(Kicheko/Makofi)*

Tulifikia mahali tulikuwa tunazungumzia habari ya Mama Ntilie hapa, Mheshimiwa Mary Nagu wakati ule akiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii akaja juu, siyo Mama Ntilie! Ni Mama Lishe! Serikali ilitamka na sasa hivi ni Mama Lishe tu. Ndiyo! Lakini la Wamachinga hili, watu wanaona sawasawa tu. Inaumiza sana! Kwa sababu wafanyabishara ndogo ndogo wanajulikana kama Wamachinga, mimi Mbunge mzima ninawakilisha hapa Jimbo la Mchinga wanakotoka Wamachinga, naitwa Machinga, maana yake sijui. Tumekosa nini, sijui! Inauma sana! Inauma kweli kweli! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa, hata kitu kinachotakiwa kuwekwa Lindi na Mtwara, basi kinaangaliwa hiki, hapana! Hiki, ondoeni! Hizi barabara mimi siamini kama zitakwisha. Tutafikia mwaka 2010 bado tuna mambo kama haya, mambo yenyewe ya kupeleka Shilingi bilioni tano huku, Shilingi bilioni 17 sehemu nyingine! Kweli tutafika mwaka 2010, hatujamaliza!

Mheshimiwa Spika, mimi sishangai hata lile eneo lililotengwa la Chuo cha *VETA* pale Mitwero, sishangai ile *fence* itafikia mahali itatafunwa na chumvi. Hapajaanza kujengwa! Siyo kitu cha kwanza hicho! Tulikuwa na reli kule, ikang'olewa. Hata reli ambayo ilishawekwa na Mkoloni, basi iling'olewa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo Lindi. Kwa hiyo, sisi tunaposimama hapa kuzungumza suala hili, mtu asisimame akajibu kwa wepesi tu. Tunajua mnapiga kelele mnazungumza, hamwelewi hali halisi. Sisi hali halisi tunaielewa vizuri zaidi kuliko mtu yeyote! Miaka 45 baada ya uhuru, ikinyesha tu Lindi hakufikiki, tuliambiwa: "Mtapanda *taxi* kutoka Mtwara mpaka Mwanza." Kwa trekta basi kutoka Lindi! Hufiki Kibiti! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, siku moja kaka yangu Mheshimiwa Mkuchika alinipigia simu saa nane usiku, kaka nimekwama. Nikamwambia bwana ingekuwa tunaulizana sisi watu wenye vigugumizi nisingekujibu maana ungesema na mimi nakuigiza. Nami nimekwama niko Mihambwe. *(Kicheko/Makofi)*

Nashukuru alipata bahati akampigia Dr. Mahanga usiku huo, bwana, mimi nimekwama, kuna wakandarasi barabarani wanatengeneza barabara, abiria wanakwama mpaka kufikia magari 200. Si mkandarasi, si Wizara ya Ujenzi, wanaona uchungu wa kuja kuwakomboa watu hawa, hivi sisi tujisikieje? Sijasema hivi toka nimeingia Bungeni,

hiki kipindi cha tatu, lakini leo nimelazimika kuzungumza kwa sababu tumechoka kweli kweli. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenye njaa anakwenda miayo tu, ukimwona mtu anakwenda mbwewe, kashiba. Tabia ya mbwewe ya mtu aliyeshiba ina harufu. Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma hatuna Mbunge wa Chama cha Upinzani. Sisi, pamoja na shida yote hiyo, ni wavumilivu, lakini wale wanaopelekewa Shilingi bilioni 17 huko ndiko kwenye Wapinzani, wanaokwenda mbwewe. *(Makofi/Kicheko)*

Tunataka tuambiweje? Kwamba ili upate huduma, basi lazima uwe Mpinzani! Sisi tuna imani na Chama hiki, kimetutoa mbali, tuna historia nacho. Mzee Kingunge atakuwa shahidi yangu, nyumba ya kwanza kufunguliwa Ofisi ya *TANU* Mkoani Lindi, moja ilikuwa Mchinga ya Mohamed Mudhihir na ya pili, Lindi ya Mzee Mnonji. Nyumba aliyokuwa anakaa Bwana Kabongo Lindi ni ya Bwana Mohamed Mudhihir, leo siwezi kutoka CCM kwa sababu ya mtu fulani tu, Ujenzi. Kama kuna mtalaam hapa wa Ujenzi hawezi kwenda na mdundo wa Serikali ya Awamu ya Nne, akae pembeni atuachie ngoma yetu. Waziri Mkuu, amewagundua watu namna hiyo kwenye Halmashauri na sasa amewaajiri kwa Mkataba. Naomba Waziri Mkuu, Mkataba sasa kama huu uelekezwe kwenye Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sisi watu wa Lindi na Mtwara tunastahili barabara kwa kiwango kile kile wanachostahili Watanzania wenzetu, hatuna tofauti. Kama Mama Ntilie ilikuwa mbaya, akaitwa Mama Lishe, hili la Manamba kubadilishwa kuitwa Wamachinga, linaumiza sana. Iteni *spade spade,* wale ni wafanyabiashara ndogo ndogo. Lakini watu wana-*enjoy* tu, tunafanyiwa dhihaka nyingine mpaka wengine wanafikia kusema watu wa Lindi na Mtwara wanaogopa ng'ombe. Mbona ninyi mnaogopa pweza sisi hatusemi? Maana yake dhihaka nyingine mbaya sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza na kwa kweli nakuwa katika wakati mgumu sana kuzungumza baada ya mzungumzaji aliyepita, kwa sababu wiki mbili zilizopita nilikuwa Mtwara na niliona tatizo ambalo wananchi wa Kusini wanalo. Lakini nafarijika kwamba matatizo ambayo wananchi wa Kusini wanayo hawako peke yao, wananchi wa Magharibi wana matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wabunge, wamezungumzia matatizo ya barabara na hasa barabara ya Itigi – Tabora, Tabora – Urambo, Urambo – Kigoma na baadaye Mwandiga - Manyovu. Hili la Itigi – Tabora tayari Mheshimiwa Mwanne Mchemba amelizungumzia, nisingependa kulizungumzia sana.

Lakini napenda kufahamu kutoka Wizara ya Miundombinu kwamba Bajeti ya sasa inaendana na maelekezo ya Bajeti ya miaka miwili mingine inayofuata. Barabara ya Itigi – Tabora, sio tu haionekani katika Bajeti ya mwaka huu, bali hata mwakani na hata

mwaka unaofuata. Kwa hiyo, hii inatia shaka kuhusiana na dhamira nzima ya jinsi gani ya kuhakikisha Mikoa hii ya Magharibi inafunguka ili wananchi wake waweze kufanya shughuli za uzalishaji, waweze kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mwandiga – Manyovu imetengewa jumla ya Shilingi bilioni mbili mwaka huu, mwaka 2005 barabara hii ilitengewa Shilingi milioni 800, bahati mbaya mpaka sasa fedha hizo hazijatumika na mwaka wa fedha umekwisha. Tatizo nadhani ni la *procurement*. Hili inabidi Wizara iliangalie sana. Nahisi kabisa *TANROAD* Makao Makuu kuna tatizo.

Mimi sitaki nionekane ni mbaguzi wa watu wa nchi nyingine. Lakini nahisi tatizo kubwa zaidi ni kuwa na Mkurugenzi wa *TANROAD* ambaye sio Mtanzania ambaye haijui Tanzania, ambaye hana uchungu na maendeleo ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Marehemu Shaaban Robert aliwahi kusema "Titi la mama tamu." Mghana siamini kabisa anao uwezo wa kuwa na uchungu wa kuendeleza barabara za nchi yetu kama ambavyo angepewa Mtanzania. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hili liangaliwe ili kuweza kuhakikisha kwamba mambo haya yanakwisha, ndiyo maana leo fedha zinatengwa katika Mikoa, hakuna kilichofanyika.

Bahati nzuri barabara hii ya Mwandiga - Manyovu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari alikwenda kule, ameiona na alikwama. Kule ndiko maeneo ambayo tunalima kahawa ya kutosha. Waziri Mkuu, alishangaa nilivyomwambia kwamba Kigoma tuna kahawa wakati wa Kikao cha Wadau wa kahawa pale Dar es Salaam. Mwaka huu wakulima wa kahawa wanapata matatizo ya kusafirisha kahawa yao kwa sababu ile barabara haipitiki. Sasa fedha zimetengwa kwa ajili *otter seal*.

Naomba niishauri Wizara kwamba, fedha zilizotengwa mwaka 2005 Shilingi milioni 800 zitumike kwa ajili ya kufanya *details design* kwa sababu ile barabara haina *detailed design*. Sehemu ya fedha zitakazobaki zijenge yale maeneo ambayo hayapitiki ili wananchi waendeleze shughuli za uzalishaji mali wakati tunatafuta fedha kwa ajili ya kujenga barabara ile kwa kiwango cha lami kuanzia Mwandiga mpaka Mwanyovu.

Mheshimiwa Spika, nimeona Bajeti ya mwaka 2007/2008 *estimation* ya ku-*allocate* Shilingi bilioni sita, sio haba na naamini kabisa kwamba fedha hizo zinatengwa Mwandiga – Manyovu. Sio kwa sababu kule kuna Upinzani, lakini ni kwa sababu watu wa Kigoma nao wanapaswa kuingizwa katika mchakato wa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapokuwa Mbunge, wakati mwingine inabidi usiangalie unakotoka peke yake. Unapokuwa Mbunge vile vile lazima uangalie Taifa kwa ujumla. Naamini kabisa kwamba sungura wetu ni mdogo, ni lazima agawiwe vizuri na kuwe na *affirmative action* ya kusaidia yale maeneo ambayo bado yana matatizo.

Mheshimiwa Spika, lakini katika hili, naomba niwe mzalendo kidogo. Kabla ya uzalendo, Waziri katika ukurasa wa 14 amezungumza kwamba Serikali imepata fedha kutoka *MCC (Millennium Challenge Cooperation)* kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege Kigoma. Naomba tu ufafanuzi kwa sababu mimi naamini Serikali yetu bado haijapata fedha za *MCC*. Hata katika Hotuba ya Mipango na Hotuba ya Wizara ya Fedha, *allocation* ya hii fedha haikuonekana.

Kwa hiyo, tunapopanga kwamba tutajenga Uwanja wa Ndege wa Kigoma kwa fedha za *MCC* wakati hata mpango wenyewe wa *MCC* kama nchi haujakamilika kwa sababu mpango huu kabla ya kupelekwa kwa wafadhili, ni lazima uje Bungeni, Wabunge wauone, waone ni jinsi gani ambavyo fedha hizi za Wafadhili tunazozipata zinaweza zikagawanywa nchi nzima. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri anipe ufafanuzi wa hili, isije kuwa wameandika hapa ili kuwafurahisha watu wa Kigoma kwamba uwanja wao wa ndege nao utajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwe mzalendo sasa. Mwaka 2002 tulibinafsisha *ATC* ikawa *ATCL*. Waziri, ametuambia kwamba mwaka 2005 jumla ya Shilingi bilioni sita zilitolewa kama ruzuku, ukurasa wa 15 wa Hotuba ya Waziri. Mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya ya *ATC,* Waziri amesema bilioni 13, lakini ninavyofahamu, kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, fedha zilizotengwa ni Shilingi bilioni 15. Kwa hiyo, itabidi Waziri ajaribu kuangalia na Waziri wa Fedha ili waweze kurekebisha hilo eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Desemba mwaka 2002 tulipobinafsisha *ATC* tulikuwa na malengo ya kuhakikisha kwamba *ATC* inaimarika. Msemaji wa Upinzani amezungumza. Nimeangalia Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi ya mwaka 2005 akionyesha kwamba ubinafishaji wake ulikuwa na mafanikio makubwa. Changamoto pekee ambayo Waziri aliainisha, ninayo hotuba, ni kwamba *ATC* inapata changamoto ya ushindani. *(Makofi)*

Mwaka mmoja baadaye tunavunja Mkataba na *South African Airways*. Nataka nipate ufafanuzi kutoka Serikalini. Mwaka jana matatizo ya *South African Airways* na *ATCL* yalikuwa hayafahamiki? Kama yalikuwa yanafahamika, kwa nini Bunge halikuelezwa ukweli? Au ndiyo haya mambo ya kusema kwamba vipengele vya Mikataba havitakiwi kuambiwa Wabunge ambao ni Wawakilishi wa Wananchi?

Mheshimiwa Spika, vipengele hivyo vya Mikataba vinaandikwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mikataba yote ya Serikali inaandikwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Inaweza ikapata ma-*consultant* kutoka nje, inaweza ikawa *out source* lakini sehemu kubwa ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iweke usiri kwenye Mikataba ya maana kama hii? Matokeo yake mwaka 2005 miezi 12 tu tunasema Shirika linakwenda vizuri, mwaka huu Waziri wa Wizara hiyo hiyo anakuja na maelezo

kwamba tunavunja Mkataba na *South African Airways* kwa sababu hauna manufaa kwa wananchi. Naomba Serikali itoe maelezo ya kina kuhusiana na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tunabinafsisha *ATC,* tuliunda *Air Tanzania Holding Company*, kwa ajili ya kuangalia mali zote za *Air Tanzania*. Waziri wa Miundombinu katika hotuba yake amezungumzia suala la *Air Tanzania* kuhakikisha kwamba inarejesha au inakamilisha uhamisho wa mali za *Air Tanzania* katika nchi kadhaa na moja ya hizo nchi ni Afrika Kusini. Naomba Waziri anieleze, nyumba ya *Air Tanzania* Afrika Kusini, sasa hivi inamilikiwa na nani? Kwa nini tunahitaji kuhamisha umiliki? Ndio maana wakati mwingine tunaposema tuwe makini katika masuala ya nchi yetu, inabidi tuwe makini kweli kweli! Tuwe tayari kuhakikisha kwamba tunalinda maslahi ya nchi hii! Tuwe tayari kuhakikisha kwamba mali za wananchi zinalindwa kwa sababu *ATC* imeanzishwa kwa hali ngumu sana. *(Makofi)*

Mtakumbuka *ATC* imeanzishwa wakati wa vita. Tumetoka kupigana, Jumuiya ya Afrika Mashariki imevunjika, hatuna mali, Wakenya wamechukua kila kitu! Mwalimu akasema ni lazima tuanzishe *National carrier.* Tumeanzisha, tumebinafsisha kwa malengo mazuri. Mali zinapotea na siyo *South Africa* peke yake, mali zinapotea *Comoro*, mali zimepotea *Oman* na pia mali zimepotea Harare. Leo hii miaka sita na tulizungumza hapo nyuma kwamba kuna mali za nchi zimepotea Afrika Kusini, tukaambiwa tuthibitishe, nashukuru kwamba Serikali imethibitisha yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anieleze, mali zetu za *ATC* zilizoko katika nchi hizi, sasa hivi zinamilikiwa na nani? Mali za Zimbabwe, Afrika Kusini na za Comoro tuelezwe ili tuweze kupata uhakika, tujue hizi mali tunazipata namna gani au bado wanazo wajanja wachache?

Mheshimiwa Spika, hilo ndiyo suala la kitaifa, ambalo nilitaka nilizungumzie. Tupate maelezo ya kina tuweze kujua ni jinsi gani ambavyo nchi yetu inakwenda ili tusirejee makosa ya zamani. Lengo letu sisi ni kuhakikisha kwamba makosa hayafanyiki tena huko tunakokwenda tuhakikishe kwamba tunaweka nchi yetu katika hali bora zaidi. Marehemu Nkuruma alisema *forward ever backward never.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapoibua haya, tunataka kuhakikisha kwamba hayafanyiki makosa mapya ili kuweza kuboresha maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, kulikuwa kuna suala hapa lilitokea hivi majuzi. Nafahamu kabisa kwamba sasa hivi kuna *monopoly* ya *Precision Air* katika biashara ya anga. Mimi sina tatizo hata kidogo na *Precision Air.* Anayemiliki *Precision* ni Mtanzania au niseme ni Watanzania, wanaajiri Watanzania, ni sehemu ya kuongeza wajasiriamali wa Tanzania. Lakini sidhani kama ni sahihi kuzuia Watanzania wengine kuingia katika biashara hiyo, kwa sababu unapokuwa na *monopoly* inakuwa ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, leo hii nakwenda Kigoma, nikikosa ndege ya *Precision* hakuna ndege nyingine. Sasa nilikuwa naomba nipate maelezo kutoka Wizarani, nini

hasa kilichotokea katika ndege ya *Karibu Airways*? Ni kwa nini Karibu hawakupewa Mkataba wa kuendesha ndege hizi? Naomba nielimishwe kwa sababu sina maelezo ya kina kuhusu tatizo hili.

Kuna tatizo kwamba mmiliki alikuja akaondoka, hakulipa hata hela za gesti na kadhalika, lakini haya ni mambo ambayo Taifa linapaswa kuelezwa, kwa sababu kipindi hiki ambacho hatuna *national carrier* ni vyema hawa *private sector* ambao wanashiriki katika mambo ya ndege kuhakikisha kwamba hakuna mtu mmoja ambaye anamiliki *route* zote kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naamini kabisa kwamba Waziri Mramba, ni mpya, ndiyo ameingia pamoja na wenzake, angalau Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, alikuwepo kidogo. Wakati mwingine tutoe muda kwa Mawaziri ambao wanaingia kwa ajili ya kuweza kujitafuta. Uchaguzi wenyewe ulichelewa sana, watu wameanza kazi mwezi Januari.

Lakini tulikuwa tunaomba Waziri ajaribu kuyachukua maoni mbalimbali ambayo Wabunge wanayatoa kwa ajili ya kuweza kuyafanyia kazi ili kuhakikisha kwamba rasilimali za nchi zinagawiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize, kwa sababu najua hili liko mioyoni mwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Barabara za kuunganisha Mkoa wa Kigoma, Tabora na Mkoa Rukwa na barabara nyingine za Kitaifa ni muhimu sana na ninaomba zipewe kipaumbele cha juu na naomba masuala ambayo Waheshimiwa Wabunge wameya-*raise* waweze kuyatolea maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi leo niweze kuchangia yale ambayo yamejaa ndani ya moyo wangu kwa kipindi kirefu baada ya kupata uhuru wetu, miaka 45 iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niwapongeze wale wote waliosoma hotuba zao, Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Waziri Mkuu, hongereni sana. Tunawatakieni kila la kheri na leo hatimaye Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ameisoma hotuba yake na naamini yale wanayoyasema wenzangu yatafanyiwa kazi na Serikali na kurekebisha baadhi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba na mimi niwapongeze viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Rais na wale waliopata nyadhifa mbalimbali kwa ajili ya kukiongoza Chama chetu na ndiyo nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni kipindi changu cha pili katika nafasi hii ya Ubunge. Miaka iliyopita alikuwepo Mbunge aliyeitwa Kanali Ayubu Kimbau, alikaa kwa kipindi cha miaka 25, alisema mpaka kinywa kikawa kinatoa moto kuzungumzia masuala ya gati na Uwanja wa Ndege wa Mafia. Kilio chetu jamani watu wa Mafia ni usafiri wa kuingia

na kutoka, sisi tuko Kisiwani. Tunafahamu matatizo yapo na ni mengi katika nchi yetu, lakini hebu basi safari hii baada ya kipindi cha nyuma kuongea na kuahidiwa kwamba kabla ya miaka hii mitano kwisha kipindi kilichopita gati letu la Mafia lingemalizika na Uwanja wetu wa Ndege ungemalizika. Lakini mpaka safari hii bado hakuna lolote kwa upande wa uwanja wa ndege.*(Makofi)*

Sasa tunashukuru katika kitabu hiki cha Mheshimiwa Mramba, ukurasa wa 14 usafiri wa anga *paragraph* ya 20 mstari wa tatu kutoka chini unasema: "Wizara pia ina mpango wa kupata msaada kutoka Shirika la Kimarekani *MCC* kwa ajili ya kuendeleza Viwanja vya Ndege vya Mafia na Kigoma." *(Makofi)*

Lakini ukienda ukurasa wa 19, malengo ya sekta kwa mwaka 2006/2007 ukianzia ukurasa 19, 20, 21 mpaka 24 neno Mafia hakuna. Sasa tufuatishe ukurasa wa 14 au tuufuatishe ukurasa wa 19 mpaka 24? Ukiangalia katika Kitabu cha Nne, mwaka huu Uwanja wa Ndege wa Mafia umepangiwa Shilingi bilioni mbili. Lakini ni kawaida Uwanja wa Ndege wa Mafia, kupangiwa na Uwanja wa Ndege wa Arusha. Lakini naomba niseme, mwaka 2002 Mafia hatukupata kitu, mwaka 2003/2004 hatukupata kitu, mwaka 2004/2005 tulipangiwa Shilingi milioni 100 Mafia na Arusha, Mafia hazikuja, lakini Waziri akaahidi kwamba kulikuwa na milioni 700 zimetengwa kwa ajili ya Uwanja wa Ndege wa Mafia. Lakini bado hata hizo Shilingi milioni 700 hazikuja. Sasa mwaka huu tumepangiwa hizi Shilingi bilioni mbili. Sijui niombe, sijui nishauri au sijui nifanye nini.

**MBUNGE FULANI:** Lia! *(Kicheko)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Siyo kulia. Mimi nilipangia kabisa huenda kesho kama hawakutamkwa Mafia, mimi kuanzia kesho nagoma kula. Nagoma kula kabisa! Lakini hili nalisema kwa uchungu, naomba sana hizi Shilingi bilioni mbili hebu sasa tuanze kama huu mpango wa *MCC* mtaongea nao, tunaomba basi hii Shilingi bilioni mbili ya safari hii Arusha pumzika kwanza, ili Mafia tuanze kazi, maana kuna kiama cha upembuzi yakinifu sijui kitachukua kiasi gani na kitachukua muda gani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mramba alipokuwa Waziri wa Fedha katika kipindi kilichopita, kwa huruma yake alitusaidia Mafia kwa kuwaelekeza kwamba tunaomba tuongee na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, pamoja na fedha na kweli tulipata bahati akaidhinisha fedha kutoka mamlaka ya Bandari, Shilingi bilioni 1.96 zitoke, lakini nashukuru fedha zilitoka na zimefanyiwa kazi. Shilingi milioni 900, upembuzi yakinifu ambao umemalizika jana na bado Shilingi milioni 600 kwa ajili ya kulipa gharama za wale watakaohamishwa 500, lakini bado milioni kama 400.

Sasa tunaomba hebu tupekuepekue, Mheshimiwa Waziri wa Fedha atusaidie watu wa Mafia, tuko Kisiwani. Leo sina uwezo, lakini ningekuwa na uwezo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Mawaziri husika, Waziri wa Fedha na Waziri wa Miundombinu, naomba twende mkatembelee Mafia mwone jinsi tunavyoathirika, jinsi tunavyoumia na kuadhirika siyo kuathirika, maana leo kuteremka kwenye chombo kama

uko wewe na mwanao au mke au na wakwe zako lazima mjitose baharini. Sasa ama upandishe nguo uwe uchi au ufunike ujitose na nguo zako. Tuwaonee huruma jamani miaka mingi 45 toka Uhuru tukae tuangalie! Tuoneeni huruma*! (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sina la kusema, lakini nilisema nitachangia Wizara hii kwa kuwa ndiyo kilio chetu kikuu. Leo tunajigamba Tanzania kwamba tunakusanya kodi Shilingi bilioni 180 kwa mwezi au zaidi. Hivyo basi, juu ya mahesabu yenu, hamuwezi kutenga siku tatu katika mwaka mzima tukapata Shilingi bilioni 18 mkamaliza matatizo ya Mafia? Halafu miaka mitano yote pengine ndiyo maisha, katika miaka ya maisha yanayokwenda, siku tatu Shilingi bilioni 18, tutamaliza Uwanja wa Ndege na gati.

Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nikwambie kwamba, matatizo haya wanayolalamika Wabunge mengi yanachangiwa na Watendaji. Lakini kwa kuwa wenzenu ni sisi na sisi ndiyo ninyi wanasiasa wenzetu, hiyo inabidi tukuelezeni. Lakini Watendaji ndiyo wanaotuvuruga. Hivi kweli agizo la Mheshimiwa Waziri Magufuli alipokuwa ujenzi, Wizara haina mpango wa kutoa Shilingi milioni 200 au 300 kwa ajili ya kununulia vifaa vya ujenzi katika barabara za Mafia? Kuna nini?

Lakini nasema, Watendaji wa Wizara hizi ndiyo wanaosababisha watu wafikie kugawana mpaka sasa kutamka *zone,* huyu Kaskazini, huyu Mashariki, huyu nini, lakini chanzo ni Watendaji wetu. Wengine wana roho mbaya na ndiyo wanaotukanisha Serikali yake Mheshimiwa Waziri Mkuu, waangalieni! Ninyi mnatoa kauli wao wanafanya wanavyotaka wao. Hawa ni maadui wa nchi hii! Waangalieni, wapembueni tena. Haya yote yasingetokea, lakini kwa sababu pengine wanajipendekeza kwa Waziri, hata mimi ningekuwa Waziri, kama unaniambia Mafia tunakutengea bilioni 100 nitakataa! Siwezi kukataa! Lakini wao wanajipendekeza kwa sababu ya kwao wanataka wajinufaishe ama waonekane bora kupitia kwa Mawaziri wao. Wanajipendekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba kwa huruma zote, safari hii tuoneeni huruma watu wa Mafia, tumechoka! Watu wanaadhirika, watu wanapoteza maisha, bahati mbaya hakuna Waandishi wa Habari. Laiti kama kungekuwa kuna Waandishi wa Habari, kila siku mngekuwa mnasikia vifo vya watu wanavyopata baharini. Watu wanatosa mizigo yao! Tuseme nini tena? Tunaiheshimu Serikali yetu, tunakiheshimu Chama chetu. Leo Upinzani umepata nguvu kwa sababu ya hili hili tu. Kwani Watendaji wetu hawajui? Katibu Mkuu aliyepita wa Wizara ya Ujenzi ndiye huyu wa Miundombinu, haelewi matatizo ya Mafia?

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ufuatane na Waziri wa Fedha na Waziri wa Miundombinu twende Mafia kabla ya Kikao hiki kumalizika. Baada ya Bajeti hii, Mungu atajalia itapita, twende mkaangalie athari tunayopata watu wa Mafia. Tuoneeni huruma. Upande wa Mafia natumaini mmeshanielewa. Gati, Uwanja wa Ndege na magreda, tunayataka. Nisipopata majibu mazuri, kesho sili!

Mheshimiwa Spika, nimerudi jana kutoka Kisumu. Tulikuwa tunazungumza masuala ya upungufu wa maji ya *Lake Victoria*. Taarifa tutaiandika, lakini Sekta ya

*Marine* upande wa Ziwa *Victoria*, wakati wowote itasimama kama hatukuchukua hatua kali na za dharura kwa ajili ya Afrika Mashariki. Ukikosa *Lake Victoria,* sidhani kama kutakuwa na Afrika Mashariki. Ndiyo kitu kinachotuunganisha.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iwasaidie wasafiri wa Ziwa Victoria, kwa sababu tuna visiwa kule, watakuja kuathirika jamaa zangu wa Ukerewe na visiwa vingine vidogo vidogo. Matokeo yake, sijui mtafanya nini kulijenga daraja kutoka Mwanza mpaka Ukerewe, itakuwa ni ndoto za Alinacha na sio leo hata ikiwezekana.

Kwa hiyo, naomba Wizara ya Afrika Mashariki, Mheshimiwa Chenge, wenzako walikuwepo pale, uliuliziwa tukakutetea. Lakini hali ingekuwa nzuri kama ungekuwepo. Tunaomba sana hili suala la *Lake Victoria* msilifumbie macho, ni hatari. Taarifa kamili tutazifikisha kwa Mheshimiwa Spika na mtazipata. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hii hoja. Lakini na mimi naomba sana Mafia safari hii ikumbukwe. Shilingi bilioni mbili ziwe za kuanzia na kama kuna sehemu sehemu, basi hata kama hiyo wanayosema katika 17 tutoe mbili, tukiongezea kule ikiwa nne, basi itafanyika vizuri ili tuweze na sisi kuwa miongoni mwa Watanzania waliokuwa huru na kuweza kupata usafiri mzuri na wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narejea tena kuunga mkono hii hoja na nashukuru na nawatakia kila la kheri. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Mwinchoum, Mbunge wa Kigamboni atafuatiwa na Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, Mheshimiwa George Simbachawene tumekubaliana aongee kesho asubuhi. Kwa hiyo, baada ya hawa wawili ajiandae Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia kidogo kwenye Bajeti hii ya Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake na Watendaji wake. *(Makofi)*

Pili, tuna tatizo kidogo katika Jimbo la Kigamboni. Moja, kuna barabara inayotoka Kongowe kwenda *Ferry*. Barabara hii imejengwa muda mrefu uliopita. Lakini ina matatizo ya aina mbili, moja kuna eneo moja linaitwa Midizini pale Kigamboni. Kabla ya ujenzi wa barabara, kulikuwa na njia ya kupitisha maji machafu kwenda baharini. Kwa bahati mbaya katika ujenzi hili halikufanyika.

Kwa hiyo, wananchi wa Midizini na Kigamboni kipindi cha mvua hawalali, nyumba zote zinajaa maji. Ninaomba zichukuliwe hatua za dharura ili kuwanusuru wananchi wa Midizini kuondokana na tatizo hili. Hilo moja.

Lakini la pili, barabara yetu bado ni nzuri, *Ferry* -Kongowe. Lakini linalojitokeza sasa hivi ni kwamba kwa bahati mbaya pia wajenzi hawakufikiria kujenga njia panda. Kwa hiyo, zinakatika kwenye njia panda. Kwenye eneo hili kuna magari makubwa yanapita yakiwa yamebeba mawe, michanga, hatimaye barabara inakatika na inatishia kuharibu barabara yenyewe.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara kwa kupitia kwako, iliangalie tatizo hili ama sivyo, baada ya muda mfupi wananchi wa Tarafa ya Kigamboni tutakuwa hatuna barabara ya uhakika yaani *Ferry*-Kongowe. Njia panda tunaomba zijengwe ili kuitunza barabara hii ya *Ferry*-Kongowe, angalau ndani iingie mita 200 au mita 100 za lami.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kuendelezwa barabara ya Ferry - Pemba - Mnazi. Kwa bahati mbaya sasa hivi nyumba zilizopo barabarani zimeshapigwa *X*. Waliohamia katika barabara hii walitolewa kwenye Vijiji vyao mbali huko kuhamia barabarani wakati wa Operesheni ya Vijiji. Wametoka Kitonga wamekuja Kibugumo, wametoka Mji Mwema *Bondeni-Beach* wameletwa barabarani juu. Sasa haya sio makosa yao. Gezaulole pale kuna Kijiji kilikuwa kinaitwa Mbwa Maji, wameletwa huku barabarani kikaitwa Geza Ulole.

Sasa tunapoendeleza barabara hii watu wataalam wanasema hamna fidia. Hili ni tatizo! Wamekuja pale kwa utashi wa Serikali, hawakuja kwa utashi wao. Kwa hiyo, ninaomba kwa kuendeleza barabara hii na suala la fidia lifikiriwe. *(Makofi)*

Katika kuendeleza barabara ya Feri - Pemba - Mnazi, kuna mpango wa kuongeza kidogo, kutoka Kibugumo kwenda Gezaulole. Kwa bahati mbaya mjenzi aliyejenga barabara hii kutoka Mji Mwema hadi Kibugumo, sasa hivi barabara ina mashimo. Barabara imevimba, hata nafikiri muda ule wa kukabidhiwa rasmi haujafika. Barabara ni mbaya!

Kwa hiyo, wananchi wa Tarafa ya Kigamboni wanasema, mjenzi huyu, kwa nyongeza ya pili, hawamtaki. Kwa hiyo, ninawaambia watu wa Wizara ya Miundombinu watakaoomba ujenzi wa barabara kutoka Kibugumo kwenda Gezaulole, aliyejenga awali hatumtaki na pia arekebishe barabara iliyojengwa ambayo kwa sasa hivi ina mashimo hata muda wa miaka miwili, mitatu haujafika.

Mheshimiwa Spika, suala la Pantoni. Pantoni sisi Wana-Kigamboni ndiyo njia yetu. Tunashukuru Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kununua Pantoni. Lakini namwomba Mheshimiwa Waziri kupitia kwako, yasitokee yale ya *MV Alina*. Fedha zimetengwa za kutosha, boti iliyoharibika *MV Kigamboni* ilikuwa nzuri, wakatuletea *MV Alina* ambayo tunaambiwa ilikuwa inapakia ng'ombe. Ninaomba fedha zilizotolewa ni za uhakika, watuletee pantoni nzuri itakayofaa ambayo itapita pantoni iliyoko sasa hivi *MV Kigamboni*. Isiwe ya *MV Alina* ambayo baadaye ikamponza kaka yangu Mustafa Nyang'anyi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni daraja la Kigamboni. Ninaelewa Serikali iko kwenye juhudi ya kujenga daraja hili. Mjenzi ni *NSSF*. Sasa kuna utata hapa, Wizara inasema bado *NSSF* hawajatimiza mambo fulani. *NSSF* wanasema sisi tuko tayari.

Kuna mambo yanayotakiwa na Wizara, *NSSF* wanasema hawawezi kuyafanya mpaka wapate *clearance* kutoka Wizara ya Miundombinu, kuwa kweli watajenga wao. Kwa sababu hayo waliyoyataka Wizara ya Miundombinu yana gharama.

Basi tunaiomba Wizara hii wakae, ninaelewa tarehe 8 Julai, 2006 watakaa Watendaji, tarehe 10 watakaa ngazi ya Makatibu Wakuu na baadaye ngazi ya Mawaziri. Ninaomba wazungumze kwa undani utata uliopo, hatimaye tuweze kulijenga daraja letu hili. Ninaamini inawezekana. Nimepitia nyaraka zote mbili za Miundombinu na za *NSSF* imefikia mahali sasa ninawaomba kwa heshima na taadhima tuelewane, wananchi wa Kigamboni na wananchi wa Dar es Salaam watafaidika. Ni *public interest.* Kwa hiyo, ninaomba pande zote mbili mkae pamoja kama mlivyoandaa Mikutano hii tuziondoe hizi kero, tuondoe maneno madogo madogo ili Ilani yetu iweze kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la UDA. UDA sijui kama ipo! Lakini kama ipo kweli, nimeona kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri. Tuna matatizo ya wanafunzi Dar es Salaam. Hiki ni chombo cha Serikali, sijui mtatusaidiaje. Ninaomba Wizara ya Miundombinu iandae utaratibu maalum kuondoa kero za wanafunzi Dar es Salaam. Ukikaa vituoni, kwa kweli utatamani kulia. Wanasukumwa sukumwa ovyo sana! Mtoto badala ya kufika Shule saa 1.00 mpaka saa 2.00 yuko barabarani, kumbe UDA ipo. Naomba liboreshwe Shirika hili ili iwe manusra ya watoto kwenda Shule kwa wakati na kurudi Shule kwa wakati. *(Makofi)*

Katika hotuba ya Waziri Mkuu, katika hotuba ya Wizara ya Fedha, katika hotuba ya Mipango nilizungumzia suala la fidia kwa wale waliobomolewa nyumba zao barabara ya *Kilwa Raod.* Kwa bahati mbaya sana Mheshimiwa Waziri Mkuu hakunijibu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha hakunijibu na Mheshimiwa Waziri wa Mipango hakunijibu. Tukaambiwa tusubiri Miundombinu. Ninaamini Miundombinu mna jibu la hili.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuelewa waliobomolewa barabara ya Kilwa fidia yao ikoje? Kama watalipwa, watalipwa lini? Ni wangapi? Ili wananchi wa Kigamboni tuweze kuwapa jawabu muafaka. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri kwenye majibu yako hili liwemo na kama wapo watakaolipwa tupate orodha yao ya watakaolipwa. Maana yake tumeambiwa tungojee Wizara husika na Wizara yenyewe kwa hili ni Wizara hii ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la *route* za magari ya daladala. Tumeongea sana kwenye ngazi ya Mkoa. Kwa mfano, kuna tatizo kubwa *route* ya Posta - Mbagala - Mangaya. Ni jambo dogo lakini sijui kwa nini haiwezi kutekelezeka. Tunaomba Wizara kwa nguvu yenu mtusaidie. Wananchi wanateseka sana, mtu anashuka pale Mbagala kwenda Mangaya ndani kule jasho linamtoka. Akiwa mtu mzima tena ndiyo haisemeki. Tuna tatizo la Posta - Mbagala - Mbagala Kuu - Mgeninani. Tunaomba pia *route* hiyo.

Tuna tatizo Tandika - Mangaya, Tandika - Mbagala, Tandika -Mbagala Kuu. Haya ni madogo sana. Namwomba sana Waziri wa Miundombinu atusaidie kwa kupitia Taasisi yake ina Mamlaka ya kutoa Leseni Dar es Salaam. Nimekwishakwenda

kuzungumza mara nyingi, tumeshaandikiana lakini hamna utekelezaji. Tusaidieni hili jamani, wananchi wanateseka sana.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *SUMATRA*. Ninaomba *SUMATRA* ivuke Kigamboni. Wananchi wa Kigamboni hakuna bei ya uhakika kule ya nauli. Ninaomba Taasisi hii iliyoko chini ya Wizara ya Miundombinu ivuke Kigamboni kuja kupanga bei maalum ya Serikali, itambulike. Leo nauli ni Sh.500/=, kesho utasikia nauli ni Sh.1,000/=, leo nauli Sh.1,000/=, kesho Sh.1,500/=. Sasa haya ni matatizo. Kwa heshima na taadhima, ninaomba mvuke Kigamboni, *SUMATRA* waje kuangalia hali ya nauli, wakae na wenye vyombo vya usafiri wakubaliane na hatimaye ijulikane kwa kila eneo nauli yake ni kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika mawasilisho yaliyowasilishwa na Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nichukue nafasi hii nimpongeze Waziri wa Miundombinu kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha katika Bunge hili asubuhi ya leo. Lakini ninayo mawili, matatu ambayo nilikuwa napenda nami niyaeleze.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama hautazungumzia barabara, basi watu wa Rukwa hawawezi kukuelewa. Rukwa ni Mkoa miongoni mwa Mikoa iliyomo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Rukwa ina matatizo makubwa sana ya usafiri. Nakumbuka hapo nyuma wakati wa mfumo wa Chama kimoja, Marehemu Kinyonto aliisimamisha Wizara ya Ujenzi kuhusu barabara ya Tunduma - Sumbawanga. Hali ni ile ile. Kila Mbunge anayetoka Rukwa anazungumzia suala la barabara. Hali ya usafiri katika Mkoa wa Rukwa ni mbaya sana, ni Mkoa ambao uko pembezoni, ni Mkoa ambao umesahaulika, ni Mkoa ambao wala haumo katika mipango ya kufikiriwa kwamba na wenyewe unaweza ukachangia katika kukuza uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana, Mkoa wa Rukwa hauna njia za kuweza kuunganisha na Mikoa mingine. Wakati Waziri anazungumzia masuala ya kuunganisha Mkoa na Mkoa kwa lami, Mkoa wa Rukwa hauwezi kufikika kwa barabara za changarawe. Hakuna barabara inayounganisha Tabora na Rukwa, hakuna barabara inayounganisha Kigoma na Rukwa. Hiyo barabara ya kutoka Sumbawanga kwenda Mbeya na yenyewe ni matatizo. Inasikitisha sana. Leo miaka 45 baada ya uhuru, katika Mkoa wa Rukwa wananchi bado wanaweza kufuata *Kit* ya dawa, sanduku la dawa, kwa baiskeli kwa kilometa 80. Hali hii wananchi wa Rukwa wataivumilia mpaka lini? *(Makofi)*

Mkoa wa Rukwa, hususan Wilaya ya Mpanda, wanazalisha tumbaku, tena kwa wingi tu na nilifarijika sana wakati. Napenda pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mtazamo wake na dhamira yake ya kutaka kuiondoa

Tanzania hapa ilipo. Ameitisha Mikutano mbalimbali na wadau wa mazao ambayo tunaweza tukauza nje, tumbaku ikiwa ni mojawapo, ikiwemo kahawa, korosho na kadhalika.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, anaitazama Tanzania hii, ni namna gani ataiondoa hapa ilipo. Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu bado safari ni ngumu. Huwezi kutuondoa hapa kama miundombinu yetu haijaimarika. *(Makofi)*

Miundombinu yetu ni dhaifu Mheshimiwa Waziri Mkuu. Inyonga na Ilunde wanazalisha tumbaku zaidi ya kilo milioni moja na nusu. Hii ni takwimu ya msimu uliopita. Wamejiingizia zaidi ya bilioni moja na nusu wananchi wale. Wananchi wale hawana barabara. Kutoka Inyonga kwenda Ilunde kilomita 80, wanalazimika wakati wa mvua kufuata sanduku la dawa kwa baiskeli. Watumishi hali kadhalika kutoka Kijiji hicho cha Ilunde mpaka kufika Makao Makuu ya Wilaya ni kilometa 210. Inyonga ni katikati ya Mpanda na Tabora, hakuna barabara ambayo inaunganisha Kijiji hicho ama na Tabora, ama na Mpanda, kama barabara hii ingeweza kuimarishwa pamoja na kwamba imo ndani ya Ilani ya CCM, Ipole - Mpanda. Ingeweza moja, kupunguza gharama za kufikisha pembejeo katika Vijiji vilivyopo katika Tarafa ya Inyonga.

Pembejeo zote zinalazimika ama zisafirishwe kwa treni mpaka zifike Mpanda kisha kwa magari mpaka kufikisha katika Vijiji husika. Wakati pembejeo hizo zingeweza kutoka Tabora na kufika katika Vijiji ambavyo vinazalisha tumbaku kwa gharama nafuu. Pengine ingekuwa ni sababu ya kupunguza gharama kwa Makampuni na wakulima wetu wakanufaika kwa kupata bei ya kuridhisha. Lakini kama hatutaimarisha miundombinu, bado tuna matatizo makubwa.

Tatizo la maeneo ambayo wanalima tumbaku, inasikitisha sana. Sio Wilaya ya Mpanda tu, hata jirani zetu. Wilaya ya Mpanda inapakana na Urambo. Bulyankulu wanazalisha tumbaku nyingi, kilomita 60, wanazalisha tumbaku. Lakini hakuna barabara! Leo huwezi kwenda ukajivunia kwamba kuna barabara inayoweza kukufikisha katika maeneo yanayozalisha mazao ambayo yanasaidia kuongeza pato la Taifa la nchi yetu. Inasikitisha sana, Kanda ya Magharibi ina uchumi ambao bado umekandamizwa, umefunikwa haujaibuliwa. *(Makofi)*

Leo tunapoitazama Kanda ya Kaskazini, pamoja na vivutio vyake vilivyopo, vivutio hivyo hivyo vinapatikana Kanda ya Magharibi. Kanda ya Magharibi ina hifadhi za Taifa tatu. Kuna Gombe, kuna Mahale na Katavi. *(Makofi)*

Watalii watafikaje Katavi? Watafikaje Gombe? Watafikaje Mahale? Hakuna miundombinu ya kuwafikisha wageni katika Kanda ya Magharibi. Uchumi tunaendelea kuulalia siku hadi siku. Ipo haja na ulazima na naiomba Serikali itazame kama kweli tunadhani kwamba uchumi ambao bado umefichika na Kanda ya Magharibi unaweza kuibuliwa, basi naamini kabisa utasaidia kuongeza pato la Taifa hili. *(Makofi)*

Moja, nilikuwa nashauri kwamba, kiwanja cha Kigoma ni muhimu sana kikaimarishwa. Kiwanja cha Ndege Tabora ni muhimu vikaimarishwa kwa kuwawezesha watalii wakaweza kufika Kigoma kisha wakapata usafiri ambao utawazungusha katika hifadhi hizi tatu, kama wanavyofanya huko Kaskazini na kusema kweli inasikitisha.

Mheshimiwa Spika, ili uweze kutoka Mpanda uende duniani, utoke ndani ya kaburi uende duniani, ni lazima utumie reli. Reli iko wapi? Reli ya Mpanda inakumbukwa wakati wa shida ya njaa, wakati kuna matatizo ya chakula. Lakini Mkoa wa Rukwa unasaidia kupeleka chakula kwa zaidi ya Mikoa sita ambayo iko Kaskazini ya Rukwa, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Mara, pengine na Dodoma. *(Makofi)*

Wote wanategemea kupata mahitaji ya chakula kutoka Mpanda. Kutoka Mkoa wa Rukwa, ili chakula hicho kiweze kutoka hakiwezi kuzunguka kupitia Mbeya, ni lazima kiletwe Mpanda. Barabara ya Mpanda - Sumbawanga, imepewa uzito unaostahili, imetengewa fedha? Kwa nini barabara hii haitengenezwi? Ni barabara muhimu sana. Barabara hii ni barabara ya changarawe, inapata matengenezo madogo madogo, lakini magari yanayotumia barabara hii na hasa katika kipindi hiki ambacho Taifa lilikuwa na matatizo ya chakula, makumi ya magari yalikuwa yakisafiri kila siku yakibeba zaidi ya tani 50 yakipita kwenye barabara ya changarawe kuleta mahindi Mpanda.

Sasa kama Serikali inaweza kudhibiti barabara za lami zisiharibike zikaweka kiwango cha uzito wa magari kutumia katika barabara za lami, hizo barabara za kokoto ambazo zinaweza kupitisha magari ya tani 10 magari ya tani 50 yanapita katika barabara hizo. Matokeo yake barabara zinaharibika. Tufanye nini? Lakini barabara ya Sumbawanga Mpanda ni barabara ambayo inapaswa iangaliwe. Hata wakati wa neema tusitazame njaa tu, hata wakati wa neema chakula cha ziada tunachokizalisha Rukwa tutakiletaje katika soko, kama barabara ya Mpanda - Sumbawanga haijatengenezwa? Lakini suala la reli na lenyewe linapaswa litazamwe.

Mheshimiwa Spika, nashindwa kufahamu, nitapenda Mheshimiwa Waziri anifahamishe, toka nimekua nikianza kupata fahamu na kwenda Shuleni, nilikuwa nikijua Reli ya Kati ni kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma. Leo naambiwa Reli ya Kati ni kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza. Ni kipi ambacho kimekifanya Kigoma isiwe katika mfumo wa Reli ya Kati? *(Makofi)*

Wameelekeza nguvu zote katika reli ambayo inatoka Tabora kwenda Mwanza badala ya Tabora kwenda Kigoma. Sasa kuna mpango wa kubinafsisha au kukodisha Shirika la Reli. Napenda kupitia katika Bunge hili nipate maelezo yafuatayo: Nini hatima ya usafiri wa Tabora - Mpanda? Sio Tabora - Mpanda peke yake! Manyoni - Singida, Ruvu - Tanga na Tabora - Kigoma. Ni lazima tuambiwe kama njia hizi za reli zitaendelea kutumika na kama zitatumika zitatumika katika utaratibu gani? Mabehewa halikadhalika hayatoshelezi.

Mimi kwangu bado nasema kwamba, pamoja na umuhimu wa kujenga mahusiano kati yetu sisi na Rwanda, lakini bado sifikiri kwamba sasa hivi ni wakati muafaka wa

kufanya *feasibility study* ya reli kati ya Isaka na Kigali wakati mfumo wa reli yetu hapa ndani ni mbaya sana, hatuna mabehewa, hatuna injini za kutosha. Leo gari moshi linaishia Dodoma badala ya kufika Dar es Salaam. Tatizo ni nini? Tuambiwe ni mabehewa, ni reli, ni kitu gani ambacho kinawafanya wasafiri wanapata adha namna hii? Serikali ni lazima iseme.

Mheshimiwa Spika, nadhani ipo haja, kwa unyenyekevu kabisa tukajaribu kuboresha miundombinu tuliyonayo sasa hivi kabla ya kutazama hayo maeneo mengine. Sidhani kwamba Rwanda wana tatizo kubwa sana la kuhitaji hiyo reli haraka sana. Kwa sababu mizigo yao hailundikani pale Isaka, usafiri wa barabara umeimarishwa kwa kiwango cha lami, mizigo inasafiri bila matatizo. Hebu tutazame, reli yetu tunaimarisha namna gani. Bado nadhani kwamba, kwa kuendelea magari ya Rwanda kuja kuchukua mizigo Isaka angalau na watu wa Isaka wanapata fedha. Watu wanalala pale, wananunua mafuta pale na wanakula kwa akina Mama Lishe.

Kwa hiyo, sidhani kama tuna uharaka sana wa kiasi hicho wa kushughulikia suala la reli ya kwenda Kigali. Tunajifunza na reli ya kwenda Zambia. Tunapenda kuwasaidia majirani zetu, lakini tunapata matatizo makubwa sana kwa kuwasaidia majirani. Nguvu chache tuliyonayo, rasilimali ndogo tuliyonayo tunaiwekeza katika kuwasaidia majirani zetu wakati wananchi wetu wanaendelea kupata matatizo makubwa hususan matatizo ya usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani ipo haja sasa hivi tukabadilika, tukajaribu kuangalia kero za wananchi wetu. Matatizo ya watu wetu, unakwenda kujenga kwa jirani, kwako kunavuja. Tunahitaji kuwasaidia ndugu zetu wa Rwanda, tunahitaji kuwasaidia ndugu zetu wa Zambia, lakini matatizo yetu tumeyapa kipaumbele cha kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, la mwisho, pengine wataalam watanichukia sana, lakini wakati nachangia hoja ya Waziri Mkuu nilizungumza suala la wataalam. Narudia tena kwa wataalam, hivi kweli inawezekana hayo mnayoyafanya hata mtu ambaye hana utaalam, anaona kwamba kazi hii inafanyika bila utaalam!

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna ukarabati mdogo katika barabara ya kutoka Mpanda kwenda Sumbawanga. Katika hifadhi ya... *(Hapa kengele ililia)*

**SPIKA:** Kengele ya pili Mheshimiwa Mbunge. Basi, ahsante sana.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Peter Serukamba, ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Tulikuwa tumekubaliana na Mheshimiwa George Simbachawene aongee kesho, lakini amepata udhuru, kuna ugeni katika Jimbo lake. Kwa hiyo, nitampa haki hiyo kabla ya Mheshimiwa Jackson Makwetta. Sasa namwita Mheshimiwa Peter Serukamba. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nami nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu. Nilitaka nianze na mambo, sijui nikusahihishie hiki kitabu ama ni kuacha. Ni jambo dogo tu. Ukurasa wa 22 kwenye kitabu hiki malengo ya Sekta kwa mwaka 2006/2007. Ukurasa wa 22 pale *bullet* ya pili: "Kukamilisha ukarabati unaoendelea wa barabara zote kwa kiwango cha lami katika barabara kuu zifuatazo:" Zimetajwa pale, lakini ningependa waiondoe barabara ya Tabora, Kaliua na Malagarasi, kwa sababu barabara hii hakuna lami inayojengwa huko sasa. Baada ya kusema hayo, labda na mimi nitoe mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, kama umesikiliza Wabunge wote, kilio chetu ni barabara na kwa kweli ukiangalia *network* ya nchi hii kwa maana ya barabara zote zinazosimamiwa na *TANROADS*, barabara zote ziko chini ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Ni asilimia tano ya barabara feki ndizo ambazo zimewekwa lami katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unaweza ukaona tunayo kazi kubwa sana mbele yetu, sasa tunafanyaje? Mimi nimuombe Mheshimiwa Waziri, umefika wakati sasa atutengenezee vipaumbele vya barabara zetu. Aje hapa na mkakati wa kutuambia tunaanza na barabara hii tunaishia na barabara hii na mikakati hiyo na vipaumbele hivyo vijengwe kufuata kule ambako tukienda ku-*invest* tutapata *return* haraka. Lazima tujenge uchumi wa jiografia, tunao mkakati wa kuhakikisha nchi hii imeendelea tunapofika mwaka 2025, moja ya vigezo ili tuweze kuendelea lazima tuwe na miundombinu imara. Sasa lazima tuangalie ni wapi tuweke pesa zetu kidogo tulizo nazo ili ziweze kuleta matunda, tunamuomba Mheshimiwa Waziri aje na *priority list* yake na atuambie kwanini tunaanza huku na sio huku.

Mheshimiwa Spika, mimi napata taabu sana ukiangalia Kanda ya Magharibi, sio tu kwa sababu natoka Kigoma, ndio maana nasema tupeleke barabara huko lakini naangali tukijenga barabara hizo tutapata nini kama nchi. Leo ukifungua *corridor* hiyo unao uhakika sasa ya mizingo yote kutoka *Eastern Congo* itapita Tanzania. *(Makofi)*

Hizi dola tunamwachia nani? Lazima tujenge barabara hizi ili dola hizi zikija tutumie kujenga barabara nyingine sasa. Ukiangalia kitabu hiki cha njano kama walivyokuwa wanasema wenzangu mambo mengine unasema tunyamaze tu. Kuna barabara ambazo leo tunazijenga na ukijiuliza hivi wakati wanapanga walikuwa huku wanafuata nini? Tunasema yale yamepita lakini sasa tunaanza upya hapa tunakwenda sasa tuanze kwa kupanga kufuata uchumi uliko. Mimi niliamini kabisa haiwezekani barabara ya Manyoni, Itigi, Tabora mpaka Kigoma isiwe *priority*. *(Makofi)*

Lakini leo kwenye bajeti hii, barabara ya Manyoni, Itigi, Tabora, hakuna hata senti tano. Kweli kweli tunataka kufungua nchi hii lakini unajiuliza barabara ya kutoka Tunduma, Sumbawanga, Sumbawanga, Mpanda, Kigoma angalau Sumbawanga mpaka Tunduma kuna mipango inayoeleweka, sasa wanamalizia *design,* ninahakika ujenzi wa lami utaanzaa, sina tatizo nalo hilo. Lakini unapotoka Sumbawanga kwenda Mpanda wanamaliza *feasibility study* mwezi wa nane, lakini hakuna pesa humu za *design*, kwa hiyo, maana yake wakimaliza tutakaa mwaka mwingine tukisubiri. Tunachelewe muda hautusubiri huu, barabara ya kutoka Kigoma mpaka Nyakanazi, wanamaliza *feasibility*

*study* mwezi wa nane. Lakini hakuna hela za *design,* maana yake tunaenda kukaa mwaka mwingine,barabara ya kutoka Tabora mpaka pale mpakani mwa Kigoma wanamaliza *design,* lakini pesa za kujenga hazipo sasa kwa hiyo, maana yake kuna mwaka mwingine tunakaa. Kweli tunao mpango mkakati wa kufungua nchi hii, ukitoka Sumbawanga kwenda Kasanga, maana huko ndio kwenye uchumi lazima ufungue bandari ya Kasanga ujenge lami uje Tunduma, unahakika watu wa Rubumbashi wote watapitishia mizigo yao Kasanga, watalileta Tunduma, lakini huwezi kuona tunapanga nini humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua ndio mwanzo wa bajeti ya mwaka huu, lakini nilitamani sasa ningeona *planning process* ituonyeshe kweli huko tunakokwenda hayo yatatekelezwa. Nilikuwa nasoma kitabu hiki hapa, kuna kwingine angalau kuna *language* nzuri kwamba anasema kuendelea kutafuta fedha, angalau unaonesha *commitment*. Lakini tunalo daraja la Maragalasi hata halijatajwa hapa, angalau haya mengine waliyoyataja kwamba tunaendelea kutafuta pesa, angalau unajua hata mtoto akilia ni rahisi, unajua nyamaza mama anakuletea kiti. Lakini basi humu hata wangetuambia hayo hayamo humu ndani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, mimi naomba sana kama kweli tunataka kuendeleza nchi hii tutengeneze *priority list,* bila hivyo siku zote tutakaa humu ndani kama tunapiga kelele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sasa mimi nilitaka kuomba mambo mawili yafuatayo, ukiangalia Ilani ya Uchaguzi ya chama chetu, ukaangalia ahadi za Rais, tumewaahidi Watanzania kujenga lami kilometa 5,000 kwa miaka kumi ndicho tulichowaahidi Watanzania kwamba kwa miaka kumi hii tutajenga barabara kilometa 5,000, naweza nikawatajia barabara zote na ikafika kilometa 5,000, hii ndio ahadi yetu.

Je, ukiiangalia ahadi yetu ukaangalia na bajeti hizi maana yake katika miaka kumi hii tunapunguza miaka miwili tayari maana hayamo kwenye mipango. Hizo barabara ambazo ni kilometa 5,000 maana yake ni barabara zote mpya sio zinazoendelea, kama ni barabara mpya, maana yake hazimo kwenye mpango wa mwaka 2006/2007, muda hautusubiri huu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukizubaa tutamaliza miaka kumi hatujafikia hili lengo na sidhani kama ndio nia ya Serikali yetu, nia ya Serikali yetu ni kutimiza ahadi zake. Sasa wenzetu mtusaidie kuonyesha mpango wa kutimiza ahadi zetu, lakini mimi nikajiuliza tatizo ninaloliona kubwa hapa ni la pesa, sasa tunafanyaje, siku ile wakati nachangia Wizara ya Fedha nilisema, maisha ni kuchagua, kupanga ni kuchagua, tupange na tuamue sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba sasa Waziri aje na mkakati, tunapataje fedha za kujenga barabara zetu, si hivyo, humu ndani tunakuwa tunapiga kelele kila siku. Mimi nilikuwa nasema wenzetu Ethiopia wameamua pesa zote zinazotokana na kodi ya mafuta wanajengea barabara, sisi tuondoke kwenye *level* hiyo tunazo *exercise duty* tumeweka kwenye mafuta, ili hela yote ambayo kwa mwaka ni karibia shilingi bilioni 207, tuziingize kwenye barabara nakuhakikishia tukifanya hivyo nchi hii tutai-*turn around* watu watashangaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuamue tu hata kwa miaka kumi kwamba miaka kumi hii kila pesa inayopatikana kwenye mafuta kwa maana ya kodi, tunaenda kujenga barabara zetu. Maana yake unapata shilingi bilioni 207 chukua shilingi bilioni 90 fanya *maintenance,* shilingi bilioni 110 jenga barabara mpya, unahakika kwa mwaka unaweza ukajenga kilometa 300. Kwa miaka kumi ni kilometa 3,000 hizo ukichanganya na pesa utakazopewa na wahisani, 5,000 tumefika.

Kwa hiyo, tusipoamua leo tukajua maana kwamba hatuna mjomba sisi, mjomba tuminyane wenyewe, tulale njaa, lakini tujenge hizi barabara. Bila hivyo hizi barabara tutapiga kelele, mbona kwako umeweka nyingi kwa fulani umeweka nyingi, tutaenda na lugha hiyo hiyo kila miaka. Maana mimi nilikuwa najiuliza na nilikuwa naangalia kitabu cha njano hiki, kama suala ni kwa nani umeweka nyingi, naweza nikawataja ni wengi sana kwao wemeka nyingi. Lakini ni zingine ni *project* zilikuwa zinaendelea tu, ungefanyaje sasa. Kuna wakandarasi wako barabarani, utaacha kuweka pesa, lazima uweke pesa Waheshimiwa Wabunge, hasa ninachosema sasa tutafute pesa za barabara mpya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nilitaka kusema kwamba sasa umefika wakati na baada ya hapo tukishasema tumeamua tunatumia pesa za mafuta, barabara zetu tuzi-*package,* tujue barabara ipi tutajenga wenyewe, barabara ipi tutatafuta mtu wa kutusaidia, tuzijue na tukishatoka hapo tukishalifahamu hilo vizuri tutapunguza muda kama tunatumia hela zetu unafanya *feasibility study* ya nini? Umeshaamua unajenga Mtwara kwenda Songea mpaka *Mbamba Bay* unahitaji *feasibility study* ya nini na ni hela zako. Unaaza na *design straight* maana *feasibility study* maana yake unataka ulinganishe *project* ipi ni *valuable* kuliko nyezake, *for the meaning,* tukishaamua kwamba barabara hii tunajenga kwa hela zetu, unaachana na *feasibility study* tunakwenda kwenye *design* tutakimbia, maana Rais amesema tuende kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeamua unajenga barabara ya Magazo kwenda Bariadi kwenda mpaka Lamadi, unataka *feasibility study* ya nini unaanza *design* unajenga. Kwa hiyo, mimi nilitaka kusema tuzi-*package* barabara zetu na tuamue sasa tujue ipi inajengwa na nani, ipi inajengwa ili tuweze kwenda.

La mwisho nilitaka kuongelea reli yetu ya kati, ninaamini mchakato unaendelea vizuri, lakini ningeomba Serikali ihakikishe kwenye huyo anayekuja kuendesha reli na sisi asilimia yetu iwemo. Ziko faida za sisi kuwemo, faida ya kwanza tukishakuwemo huyu bwana hatofanya kazi ya kutafuta faida tu akitaka kwenda kutafuta mikopo ya maendeleo tutakwenda wote, kwa hiyo tutapata mikopo ya riba nafuu na mikopo hii maana yake reli itakuwa *competitive*. Lakini pia tuanzishe reli *fund*, ili hii reli tuweze kuijenga hii, tusipoanzisha *fund* ya reli, reli hii itakuwa kila siku na huyu akiwa anaangusha matreni yake kila siku atakuwa anatukata kwenye *fee* zetu kila siku.

Kwa hiyo, tujipange namna ya kuingia kutafuta huu uchumi wa nchi hii, lakini pia tuongeze latria ya reli yetu, tuondoke kwenye 80 twende 100 mpaka 120 tusiogope, ndio dunia ya kisasa hatuwezi kushindana kama reli yetu bado inaenda kwenye latri 80 hatuwezi kushindana. Wakenya wanaenda 120 sasa na tuongeze upana wa reli yetu ili

siku moja mambo yetu yakiwa mazuri na sisi reli yetu tuweke umeme. Lakini mambo haya ni *process* kwa hiyo lazima tujipange tujiandae.

Mheshimiwa Spika, mimi nilisema leo niongee mambo haya makubwa mawili. La mwisho nilikuwa nasoma ripoti ya *FAO,* ripoti ya *FAO* inasema kwa Tanzania kwa upande wa chakula mikoa ambayo ina uhakika wa mvua kwa miaka mingi ijayo ni Kigoma, Rukwa, Ruvuma ni Lindi na Mtwara na Tabora na Kagera. Kwa maana yake mikoa hii ndiko ambako itatuletea chakula pamoja na Mbeya, sasa hiki chakula kitakujaje huku? Umuhimu wa kujenga miundo kwa maeneo haya sasa unakuwa sio wa kubishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na mimi nimeanza kuzoea zoea naomba nisigongewe kengele naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Miundombinu, nakiri kwamba asubuhi sikuwa hapa nilikuwa kwenye kikao kingine, lakini nimejaribu kuipitia hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri haraka haraka na mimi naomba niridhike kwamba ni hotuba nzuri na hotuba hii naiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita, Chama cha Mapinduzi kilifanya *conference* yake, tulikuwa na *congress* na katika *congress* ile baada ya kumaliza, *National Executive Committee* ilikutana ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye ni Mwenyekiti wa Chama changu alipeleka jina langu katika Halmashauri Kuu ya Taifa, nikateuliwa kuwa mjumbe wa kikao kile muhimu katika uhai wa chama chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete ambaye ni Mwenyekiti wa chama changu, hakuishia hapo aliniteua kuwa Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama cha Mapinduzi na kwa msingi huo nikapata nafasi ya kuingia katika Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nitakuwa *frankly* na wewe leo nimekuomba nafasi ya kuzungumza hapa *partly because* nilifikiri kwamba ninawiwa na ninayohaja ya kumshukuru kiongozi wetu huyu mkuu kwa heshima aliyonipa katika chama changu na kwa heshima aliyoitoa kwa wananchi wangu wa jimbo la Siha ambao ndio walionileta hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikitaka kumshuru kiongozi wako, humsubiri mmekaa mahali unasema mkuu asante, unamshukuru mbele ya watu, nasimama hapa kumwambia Rais wangu na Mwenyekiti wa Chama changu cha Mapinduzi, ahsante sana na Mungu ambariki sana. Nachoweze kuahidi hapa ni kwamba nitatoa kila aina ya ushirikiano kwake wanachama wenzangu kuhakikisha kwamba tunakiendeleza chama chetu na tunaiendeleza Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepokea pia pongezi nyingi kutoka kwa Wabunge wenzangu, wamenipongeza kwa nafasi hii niliyoipata, Wabunge wenzangu nawashukuru wote. Wote kabisa na *opposition* wamesimama hapa na wao wamenipongeza, Wabunge wenzangu nataka niwaambieni kwamba nilifurahi sana, uniwie radhi, nilifurahi sana kwa sababu nimejua nimepata nafasi ya kutoa mchango wangu katika Taifa hili, sitawaangusha wote, sitawaagusha narudi tena kusema ahsanteni, namshukuru Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu uko karibu na Rais nakuomba umwambie ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya ya shukrani naomba na mimi sasa niingie katika mada hii ambayo imetolewa hapa. Kipindi cha miaka mitano Wizara hii mimi nilikuwa naiheshimu na sasa kipindi hiki naendelea kuiheshimu, kwa maana yake ni Serikali ile, ni Wizara moja ambayo imefanya kazi kubwa katika nchi yetu na matokeo yake sisi wote tumeyaona. Nataka niseme hapa kwamba Wizara hii ina majukumu makubwa na kipindi ambacho wamekaa hao waliokaa, ni kipindi kifupi cha ku-*access* kwamba wamefanya nini? Lakini nataka tu niridhike haraka haraka kwamba kazi ambayo imefanyika hata kwa kipindi hiki kifupi ambacho wenzetu wamekuwapo pale ni kazi nzuri. Kinachozungumzwa hapa nini tatizo kubwa unalolipata hapa nataka niwe *clear*, ni aina ya uchumi na aina ya nchi na hali tuliyonayo ya kiuchumi katika nchi yetu. Uchumi tulionao katika Tanzania unaitwa uchumi duni, wa nyuma na wa kikoloni mamboleo, narudia, uchumi tulionao ni uchumi wa nyuma, duni na wa kikoloni mamboleo.

Mheshimiwa Spika, ni uchumi ambao *pump* yake haimo humu ndani iko nje. Tanzania uchumi wa kwetu huu wa *developing countries is a dependent economic* ni uchumi ambao unaotegemea nje zaidi kuliko ndani na ndio maana Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wetu wa Fedha, anatuambia 39% ya bajeti inatoka nje. Uchumi tulionao hapa unashindwa kubeba majukumu ya kisasa, dola unayotaka kuindesha, ni dola ya kisasa, inatakiwa iendeshwe na uchumi wenye nguvu, unazungumza mambo hapa juu hapa chini panakataa.

Mheshimiwa Spika, Karl Max alisema *always the economic base determine the super structure,* unayozungumza hapa, hapa chini patakuambia hapana huna uwezo wa kufanya haya mambo. Nenda mbele zaidi katika *developing countries* mgongano ulioko pale nini, mgongano uliopo katika nchi zinazoendelea ni kati ya nguvu kazi na kiwango cha vitendea kazi, ni kati ya *labour* na *delivery of the product of forces* ndizo hizo zinazungumzwa hapa ndio *problem* yako kubwa, unataka utatue hilo tatizo unasema tuanze kuangalia kule na kule u-*solve problem*.

Mheshimiwa Spika, Marehemu Mause Ntumu, alisema maneno yafuatayo, alisema ukiwa na tatizo *resolve the primary contradiction first the second one we go automatically*. Tatua tatizo la msingi kwanza matatizo mengine yote yanaondoka, yako matatizo ya msingi ambayo ukishayaondoa yale matatizo mengi huna haja ya kuyafanyia kazi kwa sababu la msingi limeondoka, utatatua matatizo yako. *(Makofi)*

Tatizo la msingi la kwetu tulilonalo katika Tanzania ni umaskini, usipoondokana na umaskini kelele hii iliyoko humu ndani haitakwisha, itaendelea tu. Unazungumza MKUKUTA utawaambia watu walime korosho, utawaambia waende watu wakavue samaki, huna barabara za kupitishia samaki, korosho, watabakia maskini tu hawa, utakuwa na mali pale haina thamani. Ukitaka kupata thamani lazima uwe *constant capital*

na *valuable capital* na *surplice labour* ndio inayokupa *total value*. Huna, una matunda kule Muheza yamekaa kule unataka kuyapeleka yanaoza pale huna barabara za kupeleka. Tatua tatizo la msingi kwanza matatizo mengine yote yataondoka, hapa ndani mzee wangu tukianza kuzungumza kila mtu na kwake, na mimi takwambia kule kwangu Siha ni maskini sana pale. Nenda fika mahali tamka kama Taifa na Serikali ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba *priority* katika nchi yetu ya Tanzania ni mambo ya mawasiliano kwa maana ya barabara, hapo ndio hatutagawanyika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hela yote tutakayopata, peleka kwenye miundombinu, kwa *formula* ambazo utajitafutia, mwenzetu wa Kigoma hapa amezungumza, amesema chukula hela yote ile unayochukua kwenye *fuel* peleka kwenye barabara. Unaweza ukasema Wizara ya Maliasili na Utalii chukua hela unayopata kule ambayo inaingia kama *Government revenue* yote peleka pale. Nitatoa mfano, kule nyuma tulikubaliana hapa wakati Mheshimiwa John Pombe Magufuli, alipokuwa Waziri wetu, tukasema kwamba kila bajeti tutakuwa tunatenga shilingi 1.8 bilioni, ndipo tulipoanza kutenga tukaanza kusikia na wahisani nao wanasema sasa tunakuja, tutakuja kuwasaidia. Kwa sababu hawa jamaa wanataka tubakie hivi tulivyo, na ukiendelea kuwa maskini hivi kama ulivyo, ni nzuri kwao maana yake ndio unatawalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiaanza kuwa na nguvu hivi una mabarabara hivi, una reli hivi, una simu, mambo yanakwenda vizuri, watoto wanakula, wanakunywa, unasomesha watoto, utatawalika wewe, utamwambia kwenda zako mimi nakula kwako usinibabaishe akili. Kwa hiyo, tubakie hivi hivi na kazi yako ni kuendeleza hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukianza hapa kuzungumza kila mtu lake tukaacha kulitazama Taifa kama Taifa, tumekwisha. Kwa sababu nani atakayesimama huku ambaye ameletwa hapa amechaguliwa na wananchi ambaye ataacha kulizungumza jimbo lake, nani? Nani ambaye ataacha kuzungumza hapa watu wote watazungumza tu kila mtu atazungumzia jimbo lake lakini kila mtu atazungumzia hilo, lakini *the end of the day* lazima tuangalie matatizo ya msingi. Kwa mfano wale watu wa Mtwara pale, wale watu wa Lindi pale na watu wa Kigoma pale tusipowasaidia zile barabara nakwambia hawatoki kwenye umaskini pale watabaki palepale, lazima uwasaidie hii ni ukweli mtupu, wale usipowasaidia watabaki wanabeba mizigo pale, hakuna maendeleo yatapatikana pale. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wakizungumza mimi naielewa hii, narudi jimbo langu la Siha, kwa maana yake muda unakwisha, mimi nimekuja hapa jimbo langu la Siha. Tunayo barabara inatoka kutoka pale Boma ya Ng'ombe inakwenda mpaka pale Sanya Juu inakwenda mpaka pale Garei, Nairobi, inakwenda mpaka pale Kamonga inaishia pale. Barabara hii kila siku naizungumza naambiwa *feasibility study* unajua kule tutakuja tu usiwe na wasiwasi, rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, tulikuwa tunakaa wote hapa umesogea huko, *feasibility study* kila siku mpaka nauliza maswali siku hizi naanza kusema ukiacha suala la upembuzi yakinifu, je, ni hatua gani zinazofanyika pale ili kuzuia nisijibiwe hilo hapo? Bado mpaka leo naambiwa kwamba ile barabara bado haiwezi kufanyiwa.

Kule kuna Mlima Kilimanjaro, nilisema hapa nikasema Mlima Kilimanjaro ule ungekuwa uko *South Africa 50%* ya *Government revenue* kwa maana ya bajeti 50% yake ingekuwa inatoka kutoka kwenye mlima Kilimanjaro, mlima wa Kilimanjaro haukai Kilimanjaro, unakaa Tanzania, wenzetu. Wakenya wamekuwa matajiri pale wamepiga hatua kubwa pale kwa kusingizia tu kwamba Mlima Kilimanjaro uko kwao, halafu leo wameukata uko pale. Anakuja mtalii kutoka Ujerumani anakuja pale anakuta wingi limeingia pale anakaa siku tatu, nne hoteli ili pambazuke auone mlima Kilimanjaro, ule Mlima Kilimanjaro kuna sehemu unaonekana kama ng'ombe, kuna sehemu unaonekana kama sufuria, kuna mahali unaonekana kama *landrover* anataka azunguke barabara yote ile Mlima Kilimanjaro auone, kuna *pontetials* pale kibao. Pale pana umaskini wa kunuka, kuna utajiri wa kunukia palepale, *this is a contradiction. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuomba, naiomba Serikali tusaidieni ile izunguke pale, hii kelele yoyote inayopigwa hapa itakwisha. Kenya wamepeleka nyumba zao nzuri zote za mahoteli wamapeleka pale, barabara nzuri zote zimepeleka pale wamesingizia, mlima Kilimanjaro, wanasema mlima Kilimanjaro uko Kenya na hauko kule, angalia shilingi ya kwetu, angalia na shilingi ya kwao wao wamepiga hatua wamekwenda pale, hatuishi hapo, Mheshimiwa Zakia Meghji, unafahamu habari, mbao zote za Tanzania zinatoka *West Kilimanjaro* katika Jimbo la Siha, viazi vinatoka Siha pale *West Kilimanjaro,* ngano, shairi zote zinatoka pale *West Kilimanjaro,* viazi vinatoka pale, matunda ya kila aina, ng'ombe, maziwa, kahawa kila kitu kinatoka pale, unawezaje ukawa na eneo ambalo ni *so potential* ukasema hili siwezi kuliendeleza halafu unasema sina hela, *this is a contradiction* maeneo ya aina ile unayapa kipaumbele unapeleka pale, unajua hii ikitoka hapa itasukuma maendeleo mengine ya Tanzania nzima. Nasima hapa kuiomba Serikali itusaidie barabara ya kutoka Boma ya Ng'ombe kwenda Sanya Juu, kwenda Garei Nairobi, kwenda mpaka Kamonga. Maamuzi haya yalishafanyika Mheshimiwa Pombe Magufuli ni mshahidi, ulikuwepo Serikali ilitamka siku mnaweka jiwe la msingi, mkasema barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, leo tunapozungumza watu wanafika nyumba namba moja pale pana *stop* pale hawawezi kwenda mpaka Sanya Juu pale kwenye soko, kwa sababu barabara ile haipitiki. Mheshimiwa Waziri Mkuu barabara ile na wewe Mzee wangu huwa unapita pale, unapigwa na vumbi pale wakati unakwenda zako kule si unisaidie tu mzee wangu hapa wewe ukisema neno ni mtu mkubwa. Mimi najua wewe ni mtu mkubwa, ukisema kitu hapa watu wote watasikiliza, tutaachaje kukusikiliza, unisaidie mzee wangu, hilo tu unisaidie na kule na Wamasai wamejaa kule unajua 50% pale ni Wamasai ndio mimi nawaongoza pale. Sasa leo mkinisaidia mnajua kule wamepiga hatua tutawaacha hivi hivi, sasa ndio tumeketi pale jumla mzee wangu, kule kuna binadamu tusaidie chonde chonde nawaombeni wazee wangu barabara ile tusiangalie tukasema mimi kule katika nimekaa kule huku ni Arusha, huku ni Kilimanjaro wamenikaa hapo nikafukiwa wakanisahau moja kwa moja. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba mtusaidie, barabara ya kutoka Boma ya Ng'ombe kwenda Sanya Juu mpaka *West Kilimanjaro* pale, iweze kupitika na iweze kuwekwa kwa kiwango. Hivi sasa hivi nimesoma huku wamesema imewekewa *feasibility study,* ndio inaendelea inaendelea hapo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo narudia kusema kwamba kwa niaba ya wananchi wa Siha naunga mkono hotuba hii na bajeti hii. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, barabara sasa inakuwa ni siasa, imekuwa ni siasa na sasa ni siasa inayozungumziwa kwa Kanda, wamesema wa Magharibi, watasema wa Mashariki, ninaanza kuona dalili sasa ya hatari na mimi niseme na mimi sitaacha kuzungumzia barabara ya kwa maana sasa sijui ni Kanda ipi. Maana nataka kuzungumzia jimbo langu la Kibakwe tu, matatizo yangu bado ni makubwa sana, kwa hiyo, nizungumzie Kanda ya Kati, maana ndio siasa sasa.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze tu na *road fund*, pesa ya barabara kwa Wilaya zetu, inayotolewa kimsingi ndio inayotufanya sisi wengine tukawa na matatizo ya barabara mpaka leo lakini ndio inayotufanya sisi wengine tukaweza kuingia Bunge na ndio itakayotufanya tukaweza kutoka Bungeni. Pesa hii inayozungumzwa kama pesa ya barabara inayotolewa kwa Halmashauri ni ndogo sana, kimsingi ni ndogo kwa sababu haiwezi ikatengeneza barabara kwa kiwango cha changarawe na mimi nasema hapa Serikali tu ni kwamba kwa vile Serikali sijui haipati hasara, ukifanya hesabu, maana tengeneza kitu ambacho *you don't achieve anything* hufanikiwi chochote, unatengeneza barabara leo, mwakani mvua ikinyesha ile ya kwanza tu kunakuwa hakuna barabara, unafikiria kuweka pesa nyingine kutengeneza mahala pale pale, hii ni hasara.

Mimi nilidhani ni vema nikakubaliana na hotuba aliyoitoa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, kwenye ukurasa wake wa kumi, mimi nimefurahi sana kwamba ni vizuri sera hii ya barabara, ikaangaliwa upya ili barabara za Halmashauri hizi zinazoitwa barabara za *district road* ama za vijijini, zikatengenezwa na *TANROAD* na hapa ndipo ambapo mimi naona ni pendekezo zuri sana na Kamati mimi naipongeza kwa kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Wilaya ya Mpwapwa katika mwaka 2003/2004 ilipata pesa ya barabara shilingi milioni 147, mwaka 2004/2005 ilipata shilingi 153, mwaka 2005/2006 imepata shilingi milioni 157. Sasa ukipiga mahesabu shilingi milioni 147 kwa mwaka mzima unategeneza barabara gani?

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri hiyo barabara itakuwa ni ya kama kufagia na haitaweza kudumu na hivyo tatizo linabakia pale pale. Pamoja na Ilani yetu ya Uchaguzi kusema kwamba pesa hii ya *Road Fund* itaongezwa lakini mimi sijaona dalili hizo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwamba ni vema tukaiangalia upya sera nzima hii kama kwa kweli tunataka kuondokana na matatizo ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu Mikoa mingine wanasema tuangalie suala la barabara kwa *priorities*. Mimi nasema barabara ni *basic needs* kila mtu anahitaji barabara kwa ajili ya uchumi. Kama tunazungumzia MKUKUTA, jambo la kwanza la kuondokana na umaskini ni suala la barabara. Barabara ni hitaji muhimu kwa kila mtu. Tukisema

tunataka kuangalie *impact* yake itakuwaje, itatulipaje tukitengeneza barabara kwa pesa hii maana yake maeneo mengine nchi hii hayatapata barabara na hii ni hatari.

Naiomba Serikali pesa ya barabara inayotolewa kwa Halmashauri ya Wilaya iongezeke ama utaratibu ule mzima ubadilike ili barabara hizi zitengenezwe na *TANROADS* yaani ziwe *Regional Roads*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi katika Mkoa wa Dodoma tulipokaa kwenye kikao cha *RCC* tulitoa mapendekezo yetu na mimi naiomba Serikali iyachukue mapendekezo haya ya ombi la kuomba barabara zifuatazo ziwe barabara za Mkoa ili zitengenezwe na Wakala wa Barabara. Barabara hizo ni barabara ya kutoka Gulwe - Kibakwe - Rudi - Chipogolo, barabara ya kutoka Njiapanda - Malolo - Idodoma, barabara ya kutoka Mpwapwa - Godegode - Lumuma na barabara ya kutoka Gulwe - Mima - Seluka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kimsingi kama hizi barabara zitakubalika ziwe za Mkoa maana yake Halmashauri zitapunguziwa mzigo. Kwa sababu sio rahisi kwa Halmashauri kuweza kutengeneza barabara kwa kiwango kinachofaa, zitakuwa zinaguswaguswa tu lakini haziwezi kusaidia kitu chochote.

Mheshimiwa Spika, iko barabara muhimu sana ambayo mimi naamini Jimbo la Kibakwe na Jimbo la Mpwapwa tungeweza kufungua njia tukaenda kuunganisha hii barabara ya kutoka Njiapanda - Malolo - Ruaha Mbuyuni pale kwenye daraja pale ndipo hii barabara inatakiwa kutokea pale, kama tutafungua ile barabara uko uchumi mkubwa sana kule na watu wetu wataondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, kule kunalimwa viazi mviringo, vitunguu, vitunguu swaumu lakini haijulikani kama katika Jimbo la Kibakwe, Wilaya ya Mpwapwa unaweza kupata vitunguu swaumu lakini nawaambia tunalima vitunguu swaumu na Wapemba wamekuja kule wanatusaidia, tunaendesha kilimo cha vitunguu swaumu milimani kule lakini hakuna barabara. Hali ya leo hii unapozungumzia mtu anabeba mzigo wake kwa punda sijui kama huyu yupo kwenye mkakati huo wa MKUKUTA, nadhani sisi wengine hatupo hata kwenye MKUKUTA. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, siku moja nilizungumza hapa kuhusu barabara za Milimani Kibakwe. Nikaambiwa barabara hizo ni za vijiji, barabara hizo ni za nini, haya maneno maneno haya, mimi nasema Serikali ni moja kule Kibakwe hakuna mtu anayejua barabara hii ni ya ya kijiji wanajua barabara zote ni za Serikali hii. Sasa unapokwenda kumwambia mtu wa kawaida kule na mimi wananituma na nitaendelea kusema hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu watu wako milimani. Nimesema hapa toka wamepata Uhuru hawajawahi kutengenezewa barabara. Vijiji vya Rufu, Gwamungile sana sana tu Padri anapokwenda kusoma misa pale anafyekafyeka anapitisha gari yake na yeye mara anashindwa lakini Serikali haijawahi kufanya chochote, unaambiwa barabara

hii ni ya kijiji. Hasa tukamwambie nani, Halmashauri ndio hii inapata milioni 147 kwa mwaka itatengeneza barabara hizo za milimani, tukaseme wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndio maana nasema sera hii iangaliwe upya. Hii barabara ya kijiji, hii barabara ya wapi, mimi naona kwa kweli wengine tutaumia hapa.

**MBUNGE FULANI:** Kweli!

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, unaponiambia *regional roads,* ni maaumizi kwa watu wa kule. Naomba Serikali iliangalie suala hili. Suala la barabara ni siasa, suala la barabara linaleta msukumo mkubwa na watu wetu waliotuchangua wanatusubiri tutasema nini, maana yake kero yao kubwa ni hiyo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuzungumzia masuala ya barabara, wenzangu wengine wamesema wataacha kula, mimi sitaacha kula, nitaendelea kula ili nipate nguvu ya kusema zaidi lakini hii haimaanishi kwamba shida yangu ni ndogo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu wetu ambao hawajawahi kupanda gari. Mtu wa kutoka Rufu, Gwamungile, Matonya hajawahi kupanda gari. Nimekwenda kwenye kampeni kule unaenda na gari watoto wanakimbia wanaingia msituni. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mmh!

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Gari hiyo ukipanda nayo huko ukirudi huku huna gari. Mimi hata magari mapya watu wanunue, mimi siwezi kununua gari mpya, nitatembelea wapi? Bora iwe mbovu itakuwa haiyumbi sana hii inasikitisha.

Mimi nasema pesa za Halmashauri ama ziongezeke na ziangalie uwiano. Sisi hatuna madini, wenzetu wanazungumzia Halmashauri zao zitaongezewa mrahaba milioni sijui mia mbili na ngapi sisi huku hatumo tutasemea wapi? Nadhani pakusemea ni hapahapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nimalizie na jambo langu la mwisho kwa kutoa pongezi kwa mawasiliano ya simu za mkononi angalau hawa *Celtel* tunapowafuata tukiongea nao kwa kweli mimi naridhika na nimeona wana-*respond* haraka…

**MBUNGE FULANI:** Kweli! *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Kipindi cha miezi yangu sita ya kuwepo hapa Bungeni tayari nimefanya makubaliano nao na wameshajenga mnara mmoja pale Kibakwe, wameongeza mwingine kwa ajili ya kuutia nguvu ule pale uko Lukole, ninaamini hata makubaliano niliofanya nao kwamba waongeze mnara mwingine Pwaga na Chipogolo watatekeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo basi ningependa nitumie nafasi hii niliyopata ndani ya Bunge lako Tukufu kuwapongeza sana *Celtel,* wanafanya kazi nzuri

pamoja na kwamba wanafikiria faida lakini pia wanafikiria suala la simu kama huduma muhimu kwa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingependa niongeze mengi, napenda haya haya tu niliyoyasema Serikali iyachukue na itusaidie kwa kuangalia hasa suala la barabara la vijijini ambazo hatuwekwi katika fungu lolote na ambazo Halmashauri hazina uwezo wa kuweza kuzijenga, ikazipa kipaumbele kinachostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambao wamekubali kutoa pesa kwa ajili ya daraja la Chitala ambalo wananchi kule kwa kweli wanamsubiri Waziri Mkuu wampongeze sana, kwa kweli wamefurahi na wameahidi kwamba ukifika watakuchinjia ng'ombe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na kwamba daraja lile mkandarasi ameshaanza kulijenga, lakini naamini ile pesa ni ndogo haitaweza kukamilisha lile daraja la Chitala na watu wale wameanza kufanya sherehe, lakini isije ikafika baadaye lisikamilike ikawa kwa Serikali kitu ambacho sio kizuri. Napenda kuiomba Serikali ione namna ya kuweza kuongezea kwa sababu nina hakika sijui kama lile daraja litaweza kukamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa ushauri wangu kwa Wizara hii ya Miundombinu. Kabla ya yote, napenda kusema wazi kwamba naunga mkono hoja ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kutoa pongezi kwanza kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge nyote mliopo hapa ndani na nje, kwa kuchaguliwa kwenu na wananchi kuja kuwawakilisha ndani ya Bunge hili. Ninyi ni sauti ya watu na kwa sababu ni sauti ya watu naamini kwamba Serikali kamwe haiwezi kupuuzia sauti ya watu kwa sababu kuongoza watu ni kuongozwa na watu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa ushindi wa kishindo kwa nafasi zote mbili ile ya Urais na ule ya Uenyekiti wa Chama aliyoipata hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda nitumie nafasi hii kukupongeza wewe kwanza kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Urambo Mashariki na vile vile kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili. Sisi wenzako wa rika lako na *college mates* tunaona fahari kujihusisha na wewe kutokana na utendaji bora wa kazi yako, tunasema *keep it up.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya salaam hizo, vile vile napenda kutoa salaam za pongezi kwa Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kazi nzuri anayofanya ya kusimamia Serikali ndani na nje ya Bunge hili. Mheshimiwa Edward Lowassa, anaamua haraka na kwa usahihi na anafuatilia utekelezaji na hili ndio tatizo la Watanzania, tunaamua mengi lakini hatufuatilii utekelezaji unaweza kuwa ni kuangalia barua tu lakini Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kipindi hiki ambacho umesimamia Serikali hii kwa kweli tumepata faraja. Tunaomba Mungu akuzidishie afya ili uweze kusukuma gurudumu hili, unastahili pongezi za sisi sote tuliopo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya yote kwa kuwa leo ukumbi huu wa Bunge umejaa, nadhani ni vizuri kuwashukuru kwa kuwemo humu ndani na kutusikiliza sisi wengine tunaoongea. Ni vizuri tukae humu ndani na tuchangie mawazo ili lengo la wananchi la kuwachagua liweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu kwa wapiga kura wa Jimbo langu kwa imani yao waliyoionyesha kwangu. Imani huzaa imani. Imani yao kwangu ndio iliyoniwezesha kuwa hapa. Ni matumaini yangu kwamba kwa kipindi hiki nitatekeleza imani yao kwa njia ambayo watashuhudia vizuri zaidi kuliko njia nyingine ile ambayo ilijionyesha wakati ule wa kindumbwendumbwe cha uchaguzi. Kwa wagombea wenzangu nasema yaliyopita si ndwele tugange yajayo.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe shukrani kwa wenzangu wengine wa ngazi zote, vijiji, Kata, Tarafa, Wilaya walioshiriki kufanikisha ushindi wangu. Kwa upande wa Kitaifa, ningependa nimshukuru Mama Salma Kikwete, Mheshimiwa Zakia Meghji, Mheshimiwa Hulda Kibacha, Mama Ukiwaona Ditopile, Mheshimiwa John Malecela, Ndugu Philipo Mangula, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge na wale wengine wote ambao walifanya mafanikio yangu kuwa bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda sasa niende kwenye Wizara. Kabla ya kwenda kwenye uchaguzi wa kipindi hiki, mimi na wenzangu baada ya kutembea Mikoa ya Magharibi tuliandika barua kwa Serikali kuwaomba wenzetu waifumue ile Mikoa ya upande wa Magharibi, Rukwa, Kigoma, Kagera ili iwe ni kitovu cha kupatia uchumi hata bila kujali kilimo. Barua ile iliandikwa na Mheshimiwa John Malecela, ikapelekwa kwa Wizara zote muhimu pamoja na Wizara ya Fedha ambayo Mheshimiwa Basil Mramba, alikuwa kule sasa yuko Wizara ya Miundombinu lakini tuliwaomba watekeleza mambo ambayo yalikuwa yameambatishwa kwenye barua hii pamoja na michoro hii na kitabu ambacho mimi mwenyewe nikiwa kiongozi wa Kamati ile niliandika na kupendekeza kwamba tunaweza tukapata uchumi wa nchi hii vizuri kama tutachukua uchumi wa Kongo, Burundi, Zambia, Malawi, Msumbiji kuliko huko kwingine ambako tayari tunapata matatizo tu. Lakini inaelekea labda hatukupata muda wa kusoma kama hamna nakala hizi nadhani tutampatia Waziri wa Miundombinu wa sasa ili kusudi aweze kufuatilia kwa sababu tayari tunayaona haya na wale wanaojua *geopolitics, geo-economics* tunadhani kwamba tuna-*potential* kubwa kwa kuunganisha bandari zetu na hizi nchi za Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa lile ambalo wenzangu mmelisema juu ya Wizara hii labda mwenzenu niwasaidie tu ili tumhukumu mtu kwa makosa yake. Kile kitabu cha manjano kinaonyesha kwamba shilingi bilioni 17 zimetengwa kwenda barabara ya Tarekea – Rongai na kuendelea na nyingine zimetengwa mahali pengine. Lakini historia inaonyesha kwamba zile barabara mwaka 2000 wakati Rais alipokuwa anafanya kampeni na wakati huo kulikuwa na upinzani mkali kweli aliwaambia wananchi kwamba mimi mwenyewe nitahakikisha kwamba barabara hii ya Tarekea inajengwa wakati wa utawala wangu. Mwaka 2004 ndipo mkataba ukawekwa wa kujenga barabara hii kama barabara nyingine ambazo ningependa kusema lakini sio vizuri kwa sababu lengo ni kuwaelimisha. Katika hizi shilingi bilioni 17, shilingi bilioni 10 ni za nje na shilingi 7 ndio za ndani.

**MBUNGE FULANI:** *Reverse*.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** *Ok,* wanasema za nje ni shilingi bilioni 7. Hata uki-*reverse* hoja ni ile ile. Ukiangalia barabara za mahali pengine ambapo tusingependa kuzisema kwa sababu tusingependa kufufua hoja ambayo inaleta mawazo mabaya kwa mfano barabara ya Geita - Bwanga - Kalimilwa ni shilingi bilioni 24 nayo ilikuwa *on going* na mkandarasi yuko barabarani ingekuwa vigumu kwa Serikali kutotenga fedha.

Mheshimiwa Spika, mimi sisemi kwamba huyu mtu asisemwe lakini asemwe kwa makosa yake kwamba Rais amesema hii Mikoa ya pembeni tuitazame na kama alivyopendekeza na mwenzetu pale ni vizuri kuwe na *vision* tunaelekea wapi maana ukitazama hata hii hotuba kwa kweli haina *direction* ni *description* ya mambo tu yanayofanyika lakini tunakwenda wapi kwa kweli huoni licha ya kwamba hatuna fedha. Kwa hiyo, pendekezo la mwenzetu pale kwamba fedha hatuna lakini basi tuonyeshe tunaelekea wapi, ukipewa pesa unaelekea wapi? Ukisema siwezi kuchora ramani mpaka nipate pesa nadhani hiyo ni *vision* ambayo sio nzuri. Nadhani pendekezo hilo zuri litatusaidia hata wakati huu tukiwa Bungeni kwa kipindi chetu tukapata mapendekezo yanayoonyesha mwelekeo wa barabara katika nchi yetu kwa sababu bila barabara hatuwezi kufika popote pale. *Without vision the people perish* kwa hiyo, nadhani ni pendekezo zuri alitoa mwenzetu Mheshimiwa Peter Serukamba pale.

Mheshimiwa Spika, pia amependekeza tujifunge mkanda, hatuna fedha hatuwezi kuendelea kupiga kelele tu. Mheshimiwa John Magufuli aliwahi kupendekeza wakati wake na tukaanza kuchangia fedha na tunachopendekeza hapa sisi wenyewe tujipange, tujifunge mkanda tutafute njia za kutafuta fedha ili tuweze kuendeleza barabara zetu, vinginevyo miaka na miaka tutabaki tunalia na hatuendi mbele. Kujitawala ni kujitegemea na bila kujitegemea hatuwezi kufika popote pale. Mimi nadhani lile pendekezo tungeli-*pick up* na tukaanza kulifuatilia.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kuipongeza Wizara, Waziri na wataalam wake kwa kazi nzuri wanayoifanya na hasa ya kutoa hotuba hii ambayo iko mbele yetu. Lakini mapendekezo niliyonayo hapa ni kwamba Mheshimiwa Waziri asikilize mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge hii ni *key point* kama anataka kwenda

na sisi wenzake hapa kwa sababu ukiangalia hii hotuba hapa sio ya Mheshimiwa Basil Mramba ninayemjua. Mheshimiwa Basil Mramba ni *dynamic* na *visionary* lakini hii hotuba hii mimi sikuelewa vizuri. Nitamgawia kitabu hiki ambacho nimeelezea mawazo haya nayoyasema lakini kwa hapa *I am being polite, he is my friend,* nisingependa kusema mengi zaidi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninachopendekeza hapa Mheshimiwa Basil Mramba, ukurasa wa nane wa kitabu hiki ambacho nitakugawia nasema kwamba unganisha nchi hii, weka Tanzania kuwa Taifa moja kwa kujenga barabara kutoka Kaskazini mpaka Kusini. Kaskazini vituo vikubwa viwe Mtukura, Sirari, Namanga, Tarakea, Horohoro na upande wa Kusini kule vituo vikuu viwe Tunduma, Kyela, Mitomoni, Mtambaswala na Kalambo. Ukiunganisha hivi halafu upande wa Mashariki unganisha Tanga kuelekea Magharibi. Mbweni sasa Bagamoyo pale chini kuelekea Magharibi, Dar es Salaam kueleleka Magharibi, Mtwara kuelekea Magharibi ukifanya hivyo utakuza biashara kati ya Mkoa na Mkoa na utakuza Utaifa wetu na tutakuwa watu wamoja.

Mheshimiwa Spika, leo hii ingawa nchi hii moja kama wanavyosema *Vodacom* lakini *in practice* baadhi ya Mikoa iko mbali zaidi kuliko nchi za jirani. Nadhani kwa kufanya haya kutafanya nchi hii kuwa moja zaidi kwa kuunganishwa na barabara hizo. Hili ni pendekezo langu kubwa.

Mheshimiwa Spika, la pili kama ninavyosema hapa peleka barabara kwenye maeneo ambayo ni ya kiuchumi kwanza. *We are poor,* usiendeshe nchi hii kama *Holy Communion,* ukigawa hela za barabara kama *Holy Communion* hufiki mbali. *Holy Communion* nimalizie maana muda hauniruhusu maana yake ni kwamba Padri anapogawa chakula cha bwana kwa kawaida kama kimekwisha kale kipande kinakobaki anaamua kukakata vipande vipande halafu anawagawia tena inakuwa kamili kwa imani kwa imani yetu ya Kikristo. Sasa katika maendeleo haiwezekani ni lazima kama barabara inahitaji bilioni tano utaoe bilioni tano. Huwezi kuendesha barabara kama unavyopendekeza hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika kitabu chake kile ili kutufurahisha, umejaribu kufanya hayo ya *Holy Communion*. Kila barabara kidogo kidogo nchi nzima isipokuwa kule unakokupigia kelele kwako lakini hiyo haitasaidia na Wabunge lazima tulione hilo kwamba hii bilioni moja au bilioni mia tano itasaidia, lengo ni kutaka kutufurahisha tu. Mimi nadhani itabidi tukae kama Wabunge ili tuweze kuamua tunataka nini vinginevyo hii *appeasement approach* hii haitusaidii kabisa tutabaki maskini na nchi haitakwenda popote pale.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalopenda kumalizia ni kwamba ajenge barabara zinazounganisha Tanzania na nchi jirani, *this is our potential area* na itasaidia sana katika uchumi. Vinginevyo nakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri uliyofanya ya kuunganisha Njombe na Kilombero na vile vile kwa mashirika yako ya simu ambayo yanaunganisha nchi hii kuwa Taifa moja.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa jioni hii kunipa nami nafasi nichangie machache maana mengi yameshazungumziwa na Wabunge tangu asubuhi ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kukushukuru na kukupongeza hasa kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge letu. Wale tunaokuelewa tulikuwa hatuna wasiwasi wakati wa mchakato wa kumtafuta nani awe Spika. Lakini wale waliokuwa hawakukuelewi walikuwa wanatuuliza sisi je, vipi, tunawaambia aah, huo mwamba, huyo mwenyewe huyo na naona mambo umekaa kama ulivyo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda tu na mimi nianze kutoa shukrani zangu na kumpongeza Rais kwa ushindi aliopata. Kwa kweli ni ushindi mkubwa na umefungua ukurasa mpya wa historia ya Tanzania. Aidha, nimpongeze Rais wa Zanzibar na pia niwapongeze Mawaziri wote walioteuliwa na hasa mkuu wetu wa Serikali katika Bunge, Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee pia kumpongeza tena akiwa Mwenyekiti kwa ushindi aliopata kwa uchaguzi wa Chama uliofanyika hivi juzi na nimpongeze na timu yake aliyoiteua. Timu hii ya Chama iliyochaguliwa kuanzia Katibu Mkuu, Katibu Mtendaji na wengineo naiita ni sehemu ya *neuclear weapon* na naita hivyo kwa sababu najua Mwenyekiti akisema ana *press button* vyombo vile vitafanya kazi na Tanzania utapatikana ushindi wa CCM bila mashaka yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, hotuba mwanana ambayo imegusa maeneo yote. Katika Wizara kubwa mojawapo ni hii maana imegusa anga, bahari, imegusa ardhi, imeenea kote. Kwa hiyo, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake maana wana kazi kubwa kwa muda mdogo kuweza kutuletea hotuba nzuri kama hii ambayo kila mmoja anaipongeza.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie padogo hasa katika mambo haya ya uchumi. Uchumi wetu kama tulivyoelekezwa kwamba tuangalie barabara kwa sababu utakuja uchumi mkubwa na katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri aligusia namna ya kuimarisha bandari, viwanja vya ndege na kadhalika. Ni kweli tukitupia macho katika maeneo hayo naamini uchumi wetu utapanda.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba uniwie radhi sana na pia univumilie pale tunapokaa tukazungumza hasa Wabunge wa Zanzibar wanapokaa wakaizungumza Zanzibar, wanaizungumzia Zanzibar tena kwa zile Wizara ambazo hazimo katika Muungano, lengo letu kubwa ni kwamba muelewe matatizo au Bunge lako Tukufu lielewe matatizo ya Muungano upande wa pili.

Mheshimiwa Spika, tunampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa juhudi anayofanya kwa kujenga barabara tunazozungumzia hapa, anajitahidi sana lakini hebu tuingie upenzi wa muungano wetu na ujamaa hasa tuichukue barabara moja tu ya Dar es Salaam - Songea hebu tuwatupie macho Zanzibar tutizame kama hawatajenga mpaka juu ya mapaa ya nyumba, kanchi kale kadogo, watajenga Unguja nzima. Pamoja na hali hiyo nadhani kuna haja ya kuitazama Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar uchumi wake ni mdogo na umezidi kuwa mdogo ilikuwa ikitegemea karafuu tu. Soko letu kuu lilikuwa Indonesia hayo matatizo waliyonayo Indonesia si madogo dunia yote mnayatambua lakini Indonesia nao wamepanda karafuu sasa hawataki kabisa karafuu zetu, wapi tutazipeleka?

Mheshimiwa Spika, Tanzania inaingia katika Shirikisho la Afrika Mashariki kesho kutwa au kesho, tunapoingia huko, huko ndio kwenye huo utandawazi, haya itizame Zanzibar hali yake ilivyo. Tusipoikokota, tusipokuwanayo, tusipoikamata tutafika nayo wapi na kesho kutwa Afrika inaungana na inakuwa Jamhuri ya Afrika nzima, tutakuja kuipeleka wapi Zanzibar tusipoisaidia sasa hivi na kwenda nayo pamoja.

Mheshimiwa Spika, naliomba mapema suala hilo kwa sababu najua ninachokizungumza kikoje. Labda sasa nije katika hali ya uimarishaji wa usafiri wetu wa baharini. Tukitumia vizuri bandari zetu, nashukuru Mheshimiwa Waziri kasema atakavyoimarisha bandari ya Tanga, Dar es Salaam na kwingineko na naamini pengine sikusikia na Zanzibar anaweza kuisaidia kwa sababu nayo itachangia katika mchango wa Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule baharini tayari barabara zipo wala hakutaki kutumiwa gharama za barabara kule, barabara Mungu kashaitandika kazi iliyobakia sisi tujenge gati zetu, tukiimarisha gati ya Tanga, Dar es Saalam na hata gati ya Kigoma na Mwanza maana kote kule ni mahali ambapo kutatuletea uchumi mzuri tu, tukijipanga vizuri na tukiitumia vizuri. Nadhani kama Waziri hivyo alivyopanga atatekeleza mia kwa mia naamini uchumi wetu utakuja juu.

Mheshimiwa Spika, lakini tutazame pia maafa haya ambayo yanatokea katika maji yaani baharini na hata huko katika maziwa, hali sasa inatisha, inatisha kwa sababu bado vyombo vyetu tulivyovipanga kusimamia havijasimama imara. Ajali hizi zinafika kuwatishia watu hata kuogopa kupanda na kama wataogopa kutumia vyombo vile maana yake hawataweza kuiletea uchumi nchi hii, inafikaje meli zinabinuka ovyo ovyo? Watu wanakwenda tu.

Mheshimiwa Spika, nadhani chombo kile kinachoshughulikia ambacho hapa tumekitaja kinaitwa *SUMATRA*, nadhani kijipange vizuri tena kwa sababu meli yoyote hairuhusiwi kufanya kazi baharini bila kuhakikisha kwamba vyombo vyote vya usalama vimo lazima kila baada ya miezi sita ya mwaka lazima chombo kipandishwe *slipway* ili kiangaliwe na pale ndiyo kinafanyiwa s*ervice* zake zote. Inaangaliwa *life equipment* zote zipo kuanzia *life jackets* na vinginevyo mpaka life *boards* zinatazamwa za kumnusuru wakati inatokea ajali. Sasa vitu kama hivi vinaangaliwa vya kutosha? Meli inagongwa ikiwa juu na *surveyor* kwa sababu uzima na uhai wa chombo kile kinaweza kubeba abiria? Kinaweza kubeba na mizigo? Lakini vyombo hivi vinakwenda bila ya *checking* kama hakuna hilo kinagongwa chombo hicho ikiwa plate imekuwa nyepesi kwa sababu tukubali kwamba kawaida bahari inakula *plate* yoyote yaani inakula chombo, bahari inakula na maji ya chumvi yanakula.

Sasa kila baada ya muda inapopandishwa maana yake inaangaliwa usalama wa kile chombo kilivyo, *surveyor* anaeleza chombo hiki kinahitaji *plate* hii ikatwe na hii iwekwe chombo hicho inawekwa *plate* nyingine inapakwa rangi na kufanyiwa *ship husbandrie* na mambo ya kuwekwa rangi na kadhalika inateremka chombo kama kipya. Kama si hivyo tutaendelea kupoteza wananchi wetu bure.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia juu ya barabara, ajali za barabarani zimekuwa kubwa na zinatisha, zinatisha hakuna ajali hata moja inayokosa kosa watu 50 tutawamaliza nguvukazi yetu Tanzania. Sasa kuna haja nadhani chombo hiki hiki tunachokizungumza cha usafiri kiangalie hivi haya magari yanafanywa maangalizi yake kwa wakati unaopasa? Yanaangaliwa haya magari? Hawa madereva nao hizi leseni wanazozipata ni za uhakika?

Nadhani kuna haja tubadilishe mpaka sheria maana naona labda sheria ile inamfanya dereva afanye atakavyo tu na aende tu na aue watu tu na akienda Mahakamani anaambiwa basi, nadhani kuna haja tuitazame tena sheria, la sivyo tutamaliza Watanzania wetu na halafu lawama itakuja kwa uongozi wa Serikali kwa nini hatuyaoni haya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa na mimi sipendi nizungumze mengi baada ya haya niliyozungumza kwa sababu ya wakati nasema naunga mkono hoja hii kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa kulizungumza moja, naunga mkono kwa sababu wananchi wangu waaminifu wa Jimbo la Bumbwini, tena ni wakweli. Mwaka 1995 Jimbo hili lilichukuliwa na *CUF* walisema kwamba tunawaazima *CUF* kwenda kutazama, walirudi wenyewe mwaka 2000 hata kuaga kule hawakuaga walirudi huku huku CCM na mwaka 2005 wakajikita vizuri katika CCM na nina uhakika mwaka 2010 kutakuwa hakuna upinzani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia juu ya mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kwanza kumshukuru Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hii, Mheshimiwa Basil Mramba, Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari pamoja na Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, lakini pia niwashukuru sana watendaji wote wa Wizara na Kamati kwa ujumla ambayo inashirikiana na Wizara hii, Kamati ya Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mambo machache ya kuchangia, naipongeza sana Wizara, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mawaziri kwa hotuba yao nzuri lakini kuna mambo machache ambayo nilidhani kwamba nichangie katika kuungana na wenzangu kuweza kuishauri Serikali kuboresha Wizara yetu ya Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza ambalo ningependa kulisemea ni kuhusu kitengo cha Wakala wa Ufundi na Umeme *TEMESA*. Kule kwetu sisi Jimboni Sengerema na

Jimbo la Misungwi,Jimbo la Buchosa, Ukerewe kule, Pangani nafahamu, Dar es Salaam Kigamboni kuna maeneo katika Majimbo yetu haya au katika sehemu tunazotoka tunatumia vivuko, kwa kuongelea hoja yangu niongelee kivuko cha Kigongo - Busisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tulisikia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na mikakati iliyowekwa kuimarisha usimamizi wa mapato na uboreshaji wa utendaji kazi katika Halmashauri zetu na tukaambiwa taarifa ambayo imetufurahisha sana kimsingi ilishatoka kwenye vyombo vya habari siku nyingi kwamba Serikali Kuu sasa imeingia mikataba na Watendaji wa Halmashauri za Wilaya na hasa Wakurugenzi, lengo ni kuboresha utendaji wao lakini pia kuimarisha usimamizi wa mapato.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pendekezo kwa matatizo ambayo sisi tumekuwa tukiyapata hasa tunaotumia hivi vivuko nadhani kuna umuhimu wa kuangalia uwezekano na ninaiomba Serikali ifikirie na ijaribu kuangalia kama kuna uwezekano Serikali pia pengine kupitia Wizara ama Mawaziri wenye dhamana husika katika hizi taasisi iingie mikataba ya kiutendaji na wakala wa Serikali ama hizi *agencies* na moja wapo ikiwa *TEMESA*. Nasema hili kwa sababu sisi tuna kivuko pale kinaitwa *MV Sengerema* kipo pale tangu mwaka 1986 inasikitisha hali kiliyofikia kiutendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa wenzangu tunaotoka kule ukanda ule hasa Waheshimiwa wa Geita wanafahamu sehemu ambayo tulikuwa tukivuka kwa kutumia dakika 25 ama nusu saa, sasa hivi tunatumia saa moja na nusu na mara nyingine ni kwa sababu ya ubovu lakini ubovu huu si kwa sababu tumeshindwa kupata mapato ambayo yanaweza kugharimia matengenezo ya hivi vivuko hapana wakati mwingine ni usimamizi wa mapato.

Mheshimiwa Spika, kile kivuko cha Kigongo - Busisi kuna nyakati kilikuwa kinaweza kuingiza milioni 35 kwa mwezi na hiki ndiyo kiungo kikuu kwa shughuli kama za uchimbaji wa madini kule Geita, ninaamini Sengerema mwaka kesho kutakuwa na uchimbaji pia sehemu za Ngoma nafahamu utafiti uko katika kiwango cha juu sana. Lakini hiki kivuko ndiyo kinaunganisha nchi yetu ya Tanzania na nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda na Burundi, lakini pia kutoka Kenya kwa upande wa Mashariki lakini usimamizi pale wa mapato ni tatizo kubwa sana, ninaongea kwa uchungu sana.

Mheshimiwa Spika, wenzangu walisema hapa siku moja nadhani ilikuwa leo asubuhi huenda sisi tunatarajia kupata maafa, hatuombei Mwenyezi Mungu apishe mbali lakini hali kilichofikia kivuko cha Busisi na ninafahamu pia hali hiyo inakikumba kivuko cha Kome kule Jimbo la Buchosa, nafahamu kuna matatizo katika kivuko cha Sabasaba kule Ukerewe na yamesemwa hapa na Waheshimiwa wengine pale Pangani.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali wakala hizi tuingie nazo mikataba tuone *performance* zao zikoje na tuone matumizi yao.

Mheshimiwa Spika, sisi mwezi wa tano tulifanya kikao cha Bodi ya Barabara pale Mwanza, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mheshimiwa Dr. Alex Msekela yuko hapa

ananisikiliza. *TANROADS* kitengo cha Ufundi na Umeme kilileta hoja za kuongeza gharama, nauli za kuvuka kwa wasafiri katika kile kivuko, tukaomba jamani kweli katika hali hii mnaleta pendekezo la kupandisha gharama za kivuko kisingizio kwa sababu waliyoitoa wao pengine wao waliona inafaa. Walisema gharama za uzalishaji zimepanda, tukawauliza jamani tupeni basi mahesabu ya Mapato na Matumizi, hatujapewa mpaka kesho, tuliikataa ile hoja. Sasa mambo haya yanaturudisha sana nyuma zipo *resources* ambazo tunazo tukizi-*manage* vizuri zinaweza zikatufikisha mahali pazuri sana.

Mheshimiwa Spika, napendekeza hili jambo liangaliwe upya na ikiwezekana *agencies* hizi ziingie mkataba kama ambavyo tumefanya kwa Halmashauri ili tuweze kuratibu na ku-*manage* vizuri yaani kusimamia vizuri mapato na matumizi na hii itatusaidia vizuri sana kuokoa pesa nyingi na kufikia malengo ambayo tumejiwekea kwa kiango kikubwa kuliko ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambasamba na hilo niishukuru Serikali nafahamu sisi katika Kivuko cha Kigongo - Busisi, kivuko kipya kinajengwa Mwanza na tunajua mwezi wa 12 kwa ahadi ya Serikali kitakuwa kinafanya kazi, tunatoa shukrani kwa niaba ya wananchi wa Sengerema lakini pia kwa niaba ya wananchi wa Misungwi kwa sababu kile kivuko kinahusisha Majimbo haya nasema ahsante sana tunaishukuru sana Serikali kwa jitihada hizo na wananchi wamefurahishwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini niongelee suala la uwanja wa ndege wa Mwanza. Tunasema tuna tatizo la sungura kuwa mdogo na kweli ubishi unatokea na malalamiko mengi na hapa tunavutana. Kwa sababu *share* iliyopo mbele yetu haitutoshi lakini mojawapo ya njia za kuboresha jambo hili kutupunguzia matatizo haya tuliyonayo na kupunguza hizi lawama au shutuma ama majadiliano mazito tunayoongea hapa sasa ni kuendeleza kila ambacho tunacho na tunakitumia vizuri na kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najenga hoja kuhusu uwanja wa ndege Mwanza, taarifa ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege mpaka mwaka jana Desemba imeonyesha na vyombo vya habari vimeripoti jambo hili kwamba kiwango cha mizigo kwa maana ya tani *(tonage)* kwa viwanja vyetu vya ndege kwa kipindi hicho kimeshuka kwa kati ya 5% mpaka 7% lakini sababu kubwa ya kushuka kwa viwango vya mizigo katika viwanja hivi vya ndege ni kwa sababu ya kupungua kwa mizigo ya minofu ya samaki inayosafirishwa kutoka kiwanja cha ndege cha Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanasema wasafirishaji wamehamisha sasa ndege zinatua uwanja wa Jomo Kenyatta, Nairobi, Kenya kwa sababu uwanja wetu ni mbovu sana. Ninaamini tungekiboresha sasa baada ya kuona hayo mapungufu na kwa sababu mapungufu hayatokei siku moja *trend* unaiona tu kwamba aah, hapa sasa tunapoteza *track*.

Mheshimiwa Spika, kama tukiwa makini zaidi ya tulivyo sasa pengine na kukakiimarisha kiwanja hiki na hii siyo hoja ya ukanda ni hoja ya uchumi wetu kwa sababu pato lile siyo pato linaloingia katika Kanda ya Ziwa tu ya Mkoa wa Mwanza, hapana, ile inaingia katika pato la Taifa. Naomba Serikali ione kwamba kiwanja hiki

kinahitaji kiboreshwe kwa kiwango cha Kimataifa hata katika uchumi wa kijiografia uwanja wa ndege wa Mwanza unastahili kuwa kwa kiwango cha juu ili tuweze kufaidi kwa sababu tuki maintain hiyo itasaidia sana kuchangia katika pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matarajio yangu ni kwamba kilichosemwa hapa kwenye taarifa sidhani kama kitakuwa ni kutengeneza *run ways* ama kuziba viraka katika uwanja, nadhani ni katika kuinua hadhi ya kile kiwanja kiwe cha Kimataifa. Naiomba sana Serikali izingatie hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine naomba niishukuru Serikali, juzi tarehe moja tumesoma taarifa kwenye gazeti la *The Guardian* inawezekana kuna magazeti mengine lakini nililobahatika kulisoma ni hilo kwamba ile barabara ya Usagara - Geita imetangazwa *tender* ya kumpata mtaalam wa ku-*update documents* kuhusu ujenzi wa hiyo barabara kwa kiwango cha lami kwa ule utaratibu wa *Design and Build*.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa sababu barabara hii ya kutoka Usagara kwenda Geita ni kipande tu cha barabara kuu ambayo inazunguka Ziwa Victoria ukitoka Kampala unapitia kule Mtukula unakuja mpaka Sengerema unavuka unaanza hili Jimbo la Misungwi unakuja Mwanza, unakwenda mpaka Musoma ni kipande hicho tu ambacho kimebakia hakina lami lakini nafahamu kipaumbele katika hata ile *approach* ya Afrika Mashariki ni kwamba hii barabara lazima iwe ya lami. Kwa hiyo tunaishukuru sana Serikali na tunaamini kwamba kwa utaratibu uliowekwa nadhani ujenzi utaanza mapema iwezekanavyo pengine kabla ya mwaka ujao wa fedha, nadhani haya ndiyo matarajio yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilikuwa naomba niliguswa sana asubuhi na taarifa ya ndugu zetu upande wa pili wa upinzani hasa ule ukurasa wa nne. Ubinafsishaji wa Kitengo cha Makontena pale Dar es Salaam *(TICTS)*. Jambo hili lilisemwa ukisoma pale *paragraph* ya pili kuna swali limeulizwa hivi Serikali inakimbilia wapi? Hivi Serikali inakufa? Si ipo tu? Ya nini kufanya haraka yote hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani hapa tunashauriana pengine ni vizuri kuwekana sawa, taarifa tunazifahamu Serikali imekuwa ikifafanua inasema mojawapo ya sababu zilizosababisha Kitengo kile kibinafsishwe ilikuwa ni kuboresha na kweli baada ya kubinafsishwa tumeambiwa na taarifa ziko wazi kwamba malengo ambayo yalikuwa yametarajiwa kwa miaka 10 yalifikiwa kwa ndani ya miaka minne, sasa katika mazingira hayo unafanyaje? Serikali ikaona ni busara na sisi baada ya kubinafsishwa kile kitengo tunaambiwa mwaka 2001 hii bandari yetu ya Dar es Salaam ilikuwa ya kwanza kwa kigezo hicho Afrika na wala siyo Afrika Mashariki peke yake lakini kufikia mwaka 2004 ikaanza kushuka ufanisi kwa sababu ya *congestion* ya makontena kwa sababu sasa baada ya kuwa ya kwanza makampuni mengi ya meli yakawa yanapitisha mizigo hapa sasa ufanisi ukashuka malengo yaliyokuwa yanatarajiwa yakafikiwa ndani ya miaka 10.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo la kukumbushana kwamba kulikuwa na sababu za msingi na tushukuru lakini cha msingi hapa ni kuishauri Serikali izidi kuboresha mkataba huu na mwendeshaji huyo ili kwamba ufanisi anaoupata basi na sisi

tunachokipata kiendane na ufanisi anaoupata yeye nadhani tukifanya hivyo tutakuwa tunafaidika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni huu mpango wa ujenzi wa barabara kupitia huu ufadhili wa Benki ya Dunia, mradi wa *Performance Based Management and Maintanance (PMMR).* Najua Mkoa wa Mwanza, Tanga pamoja na Rukwa tumo katika mpango huu, naiomba Serikali itusaidie kufafanua kwamba sisi ambao barabara zetu sasa zimo kwenye bajeti kwa sababu zitafaidika na huu mradi utaanza lini hasa ili wananchi wajue na hii itatusaidia sana kujipanga kwa sababu hatujatengewa fedha za barabara hizi ziko ndani ya uhudumu wa *Regional Roads* lakini sasa hivi zimeondolewa hazijapewa fedha.

Mimi nina barabara ya kutoka Katunguru kwenda Sengerema, kutoka Katunguru kwenda Nyamazugo na pia kwa mwenzangu Buchosa kule na sehemu nyingine za Mkoa wa Tanga na Rukwa. Kwa hiyo, naomba wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri atufafanulie.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa kuahirisha Bunge umekaribia ni kama labda dakika moja hivi . Matangazo, kesho tutamaliza uchangiaji kuhusu hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu saa 11.30 jioni kwa maana hiyo nitaweza tu kuwapokea wachangiaji 13 kati ya hawa nilionao hivi sasa ambao ni 23, kwa hiyo 10 watakosa nafasi ya kuchangia kwa kuongea.

Kwa hiyo, orodha mpya tuliyoipanga imezingatia sasa wale ambao hawajazungumza na kwa hiyo, kesho baadhi wamezungumza lakini hawa walikuwamo kwenye orodha tayari Mheshimiwa Richard Nyaulawa, ataanza saa nne tutaendelea sasa na Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa John Cheyo na tukibahatika Mheshimiwa Manju Salum Msambya, ndiyo tutakuwa tumemaliza kwenye saa 11.00 jioni.

Kwa hiyo, hali ndiyo hiyo Naibu Waziri wa kwanza ataanza kujibu hoja saa 11.30 jioni atachangia kwa robo saa, Naibu Waziri wa pili atachangia kwa robo saa na baada ya hapo mtoa hoja atachangia kwa nusu saa na kwa hiyo saa 12.30 tutaingia katika Kamati ya Matumizi, msisahau vile vitabu vyetu nadhani bado vipo.

Baada ya kusema hivyo sasa naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.47 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, tarehe 04 Julai, 2006 saa tatu asubuhi)*